# TOFAUTI ZA MTINDO KATIKA RIWAYA YA UPELELEZI YA KISWAHILI: ULINGANISHO WA MOHAMED SAID ABDULLA NA ERICK JAMES SHIGONGO

**Getruda Alex Chagaka**

**Tasnifu Imetolewa kwa Ajili ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Jamii Katika Fasihi ya Kiswahili**

**Chuo Kikuu cha Dodoma**

**Oktoba, 2014**

# ITHIBATI

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma na anapendekeza kuwa tasnifu hii inayoitwa **'Tofauti za Mtindo Katika Riwaya ya Upelelezi ya Kiswahili: Ulinganisho wa Mohamed Said Abdulla na Erick James Shigongo'** itumike kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Jamii katika Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

…………………………

Dkt. E.M.Songoyi

(Msimamizi)

Tarehe:…………………

## IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi **Getruda Alex Chagaka** ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu asilia, na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili au Shahada nyingine yoyote.

Saini ………………………………………

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili, wala kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa namna yoyote bila kibali cha maandishi kutoka kwa Mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia uhai, afya ya roho na mwili na ufahamu wa kuniwezesha kufanya kazi hii. Kuna michango na miongozo ya watu mbalimbali walioniwezesha kukamilisha tasnifu hii. Ninawashukuru wote walionisaidia mpaka kufikia hapa. Ningependa niwataje wote, lakini nitawataja baadhi tu ambao michango na miongozo yao imejitokeza zaidi.

Dokta Elias M. Songoyi anastahili kupewa kipaumbele miongoni mwa watu walioniwezesha kufanya kazi hii. Huyu ndiye msimamizi wa utafiti wangu. Licha ya kukabiliwa na majukumu mazito ya kiofisi na kifamilia, ninakiri kwamba alinionesha ushirikiano wa hali ya juu katika maandalizi ya tasnifu hii. Aliweza kusoma kwa wepesi sehemu mbalimbali za tasnifu, kufanya marekebisho kwa upendo, staha na heshima nilipokosea. Kwa hakika, upendo wake ulinisaidia kunipa nguvu na ari ya kuendelea na kazi japokuwa kazi ilionekana kuwa ni ngumu.

Aidha, nawashukuru wahadhiri wote tuliokuwa nao pamoja wakati wa masomo kwa misaada yao ya kitaaluma, maelekezo na ushauri kwa muda wote wa darasani ulioniwezesha kukamilisha mafunzo haya. Miongoni mwao ni Prof. J.S. Madumulla, Prof. V. Lakshmanan, Dkt. M. S. Khatibu, Dkt. R. Y. Sebonde na Bwana A. Ponela.

Ninaushukuru pia uongozi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kupitia Kurugenzi ya Masomo ya Uzamili kwa kunidahili na kunipa kibali cha kufanya utafiti katika maktaba za Vyuo Vikuu vya Mt. Augustino, Dodoma na Dar es Salaam.

Shukrani zaidi ziende kwa Prof. Mugyabuso Mulokozi na Bwana Wanjala ambao walikuwa ni wakuu wa idara za Kiswahili katika asasi za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mt. Augustino kwa ushirikiano mkubwa walionipa wakati wa utafiti

wangu. Hawa walinisaidia bila hiana nilipowaomba ridhaa ya kutumia makavazi ya idara zao kwa ajili ya unukuzi na udurusu.

Vilevile ninawashukuru wanafunzi wote wa Chuo Kikuu cha Dodoma wa shahada ya uzamili mwaka 2012/2014 na hasa wale wa Fasihi ya Kiswahili kwa ushirikiano na upendo walionionesha tangu mwanzo hadi mwisho wa mafunzo haya.

Mwisho kabisa naishukuru familia yangu kwa ushauri na misaada yao ya hali na mali waliyonipa katika kipindi chote kigumu cha masomo tokea mwanzo hadi mwisho. Bila kumsahau dada yangu mpenzi Suzana Alex Chagaka aliyechukua jukumu la kunilelea watoto wagu kwa kipindi chote nilipokuwa masomoni. Mungu aliye mkarimu awazidishie roho ya ukarimu na upendo.

# TABARUKU

Kwa marehemu wazazi wangu Bw. Alex James Chagaka na Bi. Hellena Mathias Mazuge ninaowakumbuka kila wakati. Hii ni tunu kwenu kwa madhila na shida mlizozipata katika kipindi cha uhai wenu kwa kunilea na kunihudumia kimwili na kiroho ipasavyo.

## IKSIRI

Tafiti zilizotangulia zimeonesha kuwajadili wanafasihi hawa wawili, Muhamed Said Abdulla (MSA) na Erick James Shigongo kwa upekee. Mambo kadhaa yamekuwa yakidondolewa katika kazi zao ili kukidhi mahitaji ya tafiti za wakati huo. Kazi nyingi za MSA na Shigongo zimeshughulikiwa ingawa ni kwa viwango mbalimbali. Utafiti huu una jumla ya sura tano ukijaribu kujadili hoja kuwa waandishi wa riwaya ya upelelezi ya Kiswahili wanatofautiana kimtindo. Hivyo, tumejaribu kubainisha tofauti za kimtindo katika riwaya ya upelelezi ya Kiswahili kwa kufanya ulinganisho wa riwaya za Muhamed Said Abdulla (MSA), *Mzimu wa Watu wa Kale* (1957) na *Kosa la Bwana Musa* (1984) na riwaya za Erick James Shigongo, *Damu na Machozi* (2005) na *Kifo ni Haki Yangu* (2012). Utafiti umebainisha tofauti za kimtindo hususani vipengele vya matumizi ya lugha vilivyojitokeza katika riwaya hizi kwa kuangalia namna walivyotumia vipengele hivi kuumba fani katika kazi zao. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya elimumitindo.

Utafiti huu ulijikita zaidi maktabani kwa kudurusu riwaya mbili zilizoteuliwa na mtafiti kwa kila mwandishi, pia kupitia majarida na makala za waandishi mbalimbali walioandika juu ya mtindo na riwaya ya upelelezi. Mbinu iliyotamalaki kutoa matokeo ya utafiti huu ni ya kiufafanuzi katika kuwasilisha mchakato wa data zilizokusanywa maktabani. Njia ya maelezo ndiyo imetumika kutokana na asili ya utafiti wenyewe ulivyo. Hakuna data zilizowasilishwa kwa tarakimu. Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa mtindo wa fasihi hutofautiana kati ya mwandishi mmoja na mwingine kutegemeana na jamii, makuzi na mazingira yaliyomzunguka mwandishi. Shabaha mojawapo ya tasnifu hii ni kuhimiza utafutaji katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili.

# UFUNGUO WA VIFUPISHO

MSA = Mohamed Said Abdulla

http = Hyper Text Transfer Protocol

www = World Wide Web

com = Communication

CD = Compact Disk

VCD = Video Compact Disk

DVD = Digital Video Disk

VHCD = Vertical and Horizontal Coordinates Data

Mt = Mtakatifu

Uk = Ukurasa

n.k = na kadhalika

TEHAMA = Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

TV = Television

SMG = Sub Machine Gun

SAR = Shooting Automatic Ranges

TT = Tetanus Treatment

BP = Blood Pressure

**YALIYOMO**

ITHIBATI ....................................................................................................i
IKIRARI NA HAKIMILIKI ........................................................................... ii
SHUKRANI ................................................................................................. iii
TABARUKU ..................................................................................................v
IKSIRI .........................................................................................................vi
UFUNGUO WA VIFUPISHO ..................................................................... vii
YALIYOMO ............................................................................................... viii

SURA YA KWANZA ....................................................................................1
UTANGULIZI ................................................................................................1
1.0 Utangulizi .................................................................................................1
1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti ...........................................................................1
1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti ..........................................................................2
1.3 Malengo ya Utafiti ......................................................................................3
1.3.1 Lengo Kuu ...............................................................................................3
1.3.2 Malengo Mahsusi .....................................................................................3
1.4 Maswali ya Utafiti .......................................................................................3
1.5 Umuhimu wa utafiti .....................................................................................4
1.6 Mawanda ya Utafiti .....................................................................................4
1.7 Kiunzi cha Nadharia ....................................................................................5
1.7.1 Nadharia ya Elimumtindo ..........................................................................6
1.8 Hitimisho ....................................................................................................9

SURA YA PILI ............................................................................................10
MAPITIO YA MAANDIKO ..........................................................................10
2.0 Utangulizi ..................................................................................................10
2.1 Dhana ya Mtindo Katika Kazi za Fasihi ......................................................10
2.1.1 Maandiko Kuhusu Mtindo Katika Kazi za Fasihi .......................................16
2.2 Riwaya ya Kipelelezi kwa Ujumla ...............................................................18
2.3 Riwaya ya Upelelezi ya Kiswahili ...............................................................18
2.3.1 Maandiko Kuhusu Riwaya ya Upelelezi ya Kiswahili ..................................21
2.4 Bwana MSA na Kazi Zake ..........................................................................22

2.4.1 Wasifu wa MSA ....................................................................................23
2.4.2 Kazi za MSA ........................................................................................25
2.4.3 Maandiko Kuhusu Kazi za MSA...........................................................27
2.5 Bwana Shigongo na kazi Zake ...............................................................31
2.5.1 Wasifu wa Shigongo ..............................................................................32
2.5.2 Kazi za Shigongo....................................................................................32
2.5.3 Maandiko Kuhusu Kazi za Shigongo ....................................................34
2.6 Mapengo Yaliyojitokeza .........................................................................35
2.7 Hitimisho ................................................................................................36

SURA YA TATU...........................................................................................37
MBINU NA ZANA ZA UTAFITI..................................................................37
3.0 Utangulizi ...............................................................................................37
3.1 Mpango wa Utafiti...................................................................................37
3.2 Ukusanyaji wa Data.................................................................................37
3.3 Walengwa wa Utafiti...............................................................................38
3.3.1 Jamii ya Watafitiwa...............................................................................38
3.3.2 Sampuli ya Kazi Tafitiwa......................................................................39
3.4 Eneo la Utafiti .........................................................................................40
3.5 Zana na Njia za Kukusanyia Data ...........................................................40
3.6 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhibiti Wake.............................41
3.6.1 Uchakataji na Uunganishaji wa Data ....................................................41
3.7 Changamoto za Utafiti.............................................................................42
3.8 Hitimisho .................................................................................................42

SURA YA NNE .............................................................................................44
UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA .........................................44
4.0 Utangulizi ................................................................................................44
4.1 Kazi Teule za MSA ..................................................................................44
4.1.1 Mzimu wa Watu wa Kale: Mawazo ya Jumla........................................45
4.1.2 Kosa la Bwana Msa: Mawazo ya Jumla.................................................48
4.1.3 Matumizi ya Lugha Katika kazi za MSA ...............................................50
4.1.3.1 Uteuzi wa Msamiati.............................................................................50

4.1.3.2 Matumizi ya Sinonimu ....................................................................53
4.1.3.3 Matumizi ya Antonimu ...................................................................54
4.1.3.4 Matumizi ya Tamathari za Semi ...........................................................54
4.1.3.4.1 Tabaini.......................................................................55
4.1.3.4.2 Sitiari .......................................................................57
4.1.3.4.3 Tashihisi .....................................................................59
4.1.3.4.4 Tashibiha .....................................................................59
4.1.3.5 Matumizi ya Mchezo wa Maneno ..........................................................59
4.1.3.6 Matumizi ya Vilugha.....................................................................61
4.1.4 Uumbaji wa Wahusika Katika Riwaya za MSA ...............................................63
4.1.5 Msuko wa Matukio Katika Riwaya za MSA....................................................66
4.1.6 Mandhari Katika Riwaya za MSA ..........................................................67
4.1.7 Dhamira Katika Riwaya za MSA ...........................................................68
4.2 Kazi Teule za Shigongo ..................................................................69
4.2.1 Kifo ni Haki Yangu: Mawazo ya Jumla.....................................................70
4.2.2 Damu na Machozi: Mawazo ya Jumla ........................................................75
4.2.3 Matumizi ya Lugha katika Riwaya za Shigongo.............................................77
4.2.3.1 Matumizi ya Tafsiri ....................................................................77
4.2.3.2 Matumizi ya Rejesta ....................................................................79
4.2.3.3 Matumizi ya Dhana za Sayansi na Teknolojia ..............................................81
4.2.4 Uumbaji wa Wahusika Katika Riwaya za Shigongo.............................................83
4.2.5 Mtiririko wa Matukio Katika Riwaya za Shigongo ..........................................85
4.2.6 Mandhari Katika Riwaya za Shigongo.....................................................86
4.2.7 Dhamira Katika riwaya za Shigongo......................................................87
4.3 Tofauti za kimtindo Kati ya MSA na Shigongo..............................................88
4.3.1 Matumizi ya Lugha ......................................................................88
4.3.2 Ujenzi wa Taharuki .....................................................................90
4.3.3 Uumbaji wa Wahusika .....................................................................91
4.3.4 Utumiaji wa Dhana za Kisayansi na Teknolojia ...........................................93
4.3.5 Mtiririko wa Matukio ....................................................................94
4.3.6 Uumbaji wa Mandhari......................................................................94
4.3.7 Uwasilishaji wa Dhamira .................................................................94
4.3.7.1 Dhana ya Mapenzi na Ngono ..............................................................94

4.3.7.2 Malezi ....................................................................................... 95
4.3.7.3 Nafasi ya Mwanamke ....................................................................... 96
4.3.7.4 Suala la Dini ....................................................................................... 97
4.4 Sababu za Kutofautiana Kimtindo Kati ya MSA na Shigongo ........................ 98
4.4.1 Athari za Wakati ..................................................................................... 98
4.4.2 Athari za Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia ......................................... 99
4.4.3 Athari za Mmomonyoko wa Maadili ........................................................ 100
4.4.4 Athari za Kimazingira ............................................................................ 101
4.5 Waandishi Walioathiri Uumbaji wa Fani Katika Kazi za MSA .................... 102
4.6 Waandishi Walioathiri Uumbaji wa Fani Katika Kazi za Shigongo .............. 103
4.7 Hitimisho .................................................................................................. 104

SURA YA TANO ............................................................................................ 105
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ................................................................... 105
5.0 Utangulizi ............................................................................................... 105
5.1 Muhtasari wa Tasnifu ................................................................................ 105
5.2 Utoshelevu wa Nadharia ........................................................................... 107
5.3 Mchango Mpya wa Utafiti Huu .................................................................. 109
5.4 Maoni na Mapendekezo ............................................................................ 110
5.4.1 Maoni ................................................................................................... 110
5.4.2 Mapendekezo Kuhusu Tafiti Zijazo ......................................................... 111

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii imezungumzia juu ya usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, lengo kuu la utafiti na malengo mahususi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti pamoja na nadharia ya utafiti iliyotumika imefafanuliwa.

## 1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Shigongo na MSA wameandika riwaya za upelelezi ambazo kwa hakika zimewavuta sana wasomi na wasomaji wengi hususani wa fasihi ya Kiswahili. Tafiti na chambuzi mbalimbali za MSA na Shigongo zimeshughulikiwa sana na wataalamu kadhaa kila mmoja kwa upekee wake. J.S.William 1972, anafafanua kuwa uelewekaji wa kazi za MSA unawapa shida wasomaji kutokana na mtiririko wa hadithi ulivyo. Kwa mfano, hadithi huanzia mahali isipotakiwa kuanzia na utatuzi wa tatizo umeonekana ni wa kimaajabu hadi kufikia hatua ya kumuona mpelelezi kuwa ni jini kutokana na anavyoweza kutatua tatizo. Zaidi ya hayo, kuna hoja kwamba mpelelezi kazidishiwa akili ya kutatua tatizo katika riwaya ya upelelezi ya Kiswahili (S.A.Mohamed, 1973). Namna ya utatuzi wa tatizo katika riwaya ya upelelezi ya Kiswahili huonekana ni wa kimaajabu na kushangaza kwani msomaji asipokuwa makini hupata shida kuelewa mpelelezi kamng'amuaje aliyetenda kosa. Madumulla (2009), Hamad (2011), na Khamis (2011) wanaelezea kazi za MSA kwa namna mbalimbali kutegemeana na mtazamo wa kila mmoja.

Hata hivyo, mapitio mengi yaliyopitiwa na mtafiti yanaonesha wazi kuwa kazi nyingi za Shigongo hazijafanyiwa uhakiki na utafiti wa kutosha. Reuster (2008), anamwelezea Shigongo kama mwandishi anayekusudia kubadili mitazamo ya

wasomaji wake. Sehemu kubwa ya uhakiki uliofanywa imezihusisha kazi za MSA na uhalisia. Uhalisia huu haujaweza kuunganishwa bayana na baadhi ya mawazo ambayo pengine ndiyo yamekuwa chachu ya kuweza kuonesha tofauti za kimtindo katika kutumia lugha ili kuumba fani ya waandishi hawa.

Kwa hiyo, mtafiti ameamua kufanya utafiti kwa kusoma na kuchambua kwa makini riwaya za MSA na Shigongo, kisha kufanya ulinganisho wa mitindo waliyoitumia katika kazi zao. Ingawa kazi za watunzi hawa zimeandikwa katika vipindi na miktadha tofauti, mtafiti ameshawishika kuzishughulikia kwa lengo la kulinganisha mitindo wanayoitumia katika kazi zao. Vilevile, mtafiti ameamua kushughulikia utanzu wa riwaya kwa sababu anaamini kuwa utanzu huu humpa mwandishi nafasi ya kutumia lugha kwa mapana yake. Lengo hasa ni kuona namna waandishi hawa wanavyoweza kutofautiana kuonesha ubunifu katika kazi zao na sababu zinazowafanya watofautiane.

**1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti**

Msanii ni mali ya jamii na sanaa aifanyayo ni kwa ajili ya jamii pia. Hivyo, fikra na tabia yake ni zao la jamii yake. Msanii anaandika kwa ajili ya kufikisha ujumbe kwa jamii ambao hutokana na uzoefu alionao kupitia jamii yake. Japokuwa hutoa mawazo yake, lakini nyuma yake kuna jamii na mazingira yaliyomsukuma. Kwa hiyo, licha ya mwandishi kutoa mawazo yake kupitia uandishi, mtindo anaoutumia hupata athari kutokana na jamii na mazingira yanayomzunguka.

Ikumbukwe kwamba historia ya maisha ya mwandishi ina mchango katika mtindo wa mwandishi. Hii ina maana kwamba namna msanii anavyoweza kuumba fani ya kazi yake hutegemea historia ya maisha yake aliyoishi. Mtindo katika riwaya hutofautiana kati ya mwandishi mmoja na mwingine. Hii husababishwa na mambo kadhaa yanayomzunguka mwandishi husika. Mambo haya ni pamoja na mazingira

yanayomzunguka, jamii, kiwango cha elimu, wakati, itikadi na mengine mengi. Mambo haya yote humfanya mwandishi kuwa na mtindo wa kipekee tofauti na mwandishi mwingine.

Tatizo la utafiti huu ni kutokushughulikiwa kazi za waandishi MSA na Shigongo kwa kufanya ulinganisho wa mtindo katika riwaya zao, ili kuona na kuonesha namna na sababu zinazowafanya waandishi hawa watofautiane kimtindo katika uumbaji wa fani katika riwaya zao kutegemeana na jamii na mazingira yaliyowazunguka.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

### 1.3.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kutalii na kuchambua kinagaubaga mtindo wa riwaya za MSA na Shigongo walioishi katika jamii, mazingira na nyakati tofauti, na kubainisha namna na sababu zinazowafanya watofautiane kuumba fani katika kazi zao.

### 1.3.2 Malengo Mahsusi

i. Kubainisha ni kwa namna gani waandishi MSA na Shigongo walioishi katika jamii na nyakati tofauti wanatofautiana kimtindo katika kuumba fani katika riwaya zao.
ii. Kubainisha sababu zinazochangia kutofautiana kimtindo kati ya waandishi MSA na Shigongo katika uumbaji wa fani katika riwaya zao.
iii. Kubainisha waandishi wa riwaya ya upelelezi wanaowaathiri MSA na Shigongo katika uandishi wa riwaya zao.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Katika kufanya utafiti huu mtafiti aliongozwa na maswali yafuatayo:

i. Ni kwa namna gani MSA na Shigongo walioishi katika jamii na nyakati tofauti wanatofautiana kimtindo katika uumbaji wa fani katika riwaya zao?
ii. Ni sababu zipi zinazochangia kutofautiana kimtindo kati ya waandishi MSA na Shigongo katika uumbaji wa fani katika riwaya zao?
iii. Ni waandishi wapi wanaoathiri uandishi wa riwaya za MSA na Shigongo?

### 1.5 Umuhimu wa utafiti

Matokeo ya utafiti huu yalitarajia kuleta manufaa yafuatayo:

i. Kukamilika kwa utafiti huu kumeongezea marejeleo muhimu kwa watafiti, walimu na wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili na fasihi kwa ujumla.
ii. Utafiti huu umetoa mchango katika kukuza na kuendeleza uhakiki katika fasihi ya Kiswahili.
iii. Utafiti huu umetoa changamoto kubwa kwa watafiti watakaofuatia kufanya utafiti zaidi, hasa katika uga huu wa riwaya.

### 1.6 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita zaidi katika kuchambua tofauti za kimtindo katika riwaya za MSA na Shigongo, waandishi ambao huandika riwaya za upelelezi. Hivyo mtafiti alilinganisha tofauti za kimtindo katika riwaya za waandishi hawa walioishi katika jamii na nyakati tofauti na kuona namna wanavyotofautiana katika kuumba fani katika kazi zao.

## 1.7 Kiunzi cha Nadharia

Kuna nadharia nyingi zitumiwazo na wachambuzi mbalimbali katika kuzielewa kazi za kifasihi. Nadharia za kufikia malengo haya zimekuwa zikiongezeka kutokana na mawazo mapya na juhudi za wanafalsafa kujaribu kuuelewa ulimwengu na kila kimzungukacho mwanadamu. Kwa mfano, historia inatukumbusha kuwa hapo awali nadharia za umithilishaji, uasilia na urasimi zilifanywa kuwa njia pekee katika kuhakiki kazi za kifasihi (Pizer, 1993). Baada ya muda, nadharia za uhalisia, uhalisia wa kijamii na ulimbwende zilionekana kuwa ni njia bora za kujielimisha juu ya ufasili wa kazi za kifasihi. Hata hivyo, huu haukuwa mwisho wa kuibuliwa kwa nadharia, kwani ulimwengu umeshuhudia kuibuka kwa nadharia kama; elimumtindo, umuundo, uhakiki-saikolojia, uhakiki mamboleo, ufeministi na uhakiki mpya (Ntarangwi, 2004). Hizi ni baadhi tu ya nadharia kati ya nyingi, kwani kila mara nadharia mpya hujitokeza au kuboreshwa zile za awali.

Uchaguzi wa nadharia itakayoongoza mawazo katika uchambuzi wa kazi ya kifasihi huwa ni suala gumu kidogo, kwa sababu pana nadharia na mitazamo mingi inayoweza kutumika. Kwa mfano, katika nadharia ya uhalisia peke yake, kuna uhalisia wa kiuhakiki, uhalisia wa kibwanyenye na uhalisia wa kijamaa. Suala la uchambuzi wa kazi ya kifasihi hali kadhalika ni lenye utata, kwa sababu mpaka sasa hakuna nadharia hata moja inayoweza kuchukuliwa kama ndiyo yenye kueleza kikamilifu uchambuzi wa kazi za kifasihi. Yaani, kila nadharia ina ubora wake, pamoja na upungufu wake. Isitoshe, hapana njia yoyote iliyo bora na halisi ya kuihakiki kazi ya fasihi. Jambo la muhimu ni kuzingatia lengo la uchambuzi na mambo bayana yanayokusudiwa katika uchambuzi huo. Hata hivyo, mchambuzi yafaa kuonesha ubora wa nadharia iliyochaguliwa katika kuelezea dhima ya uchambuzi ili kutoa mwanya wa mawazo mbadala.

Kutokana na unyeti wa dhima ya utafiti huu, nadharia ya elimumtindo imetumika. Nadharia hii ni muhimu kutokana na ubora wake utakaoelezwa hapo chini, kwamba, mhimili mkuu wa nadharia ya elimumtindo ni ubunifu katika matumizi ya lugha, hususani mitizamo ya uteuzi na tofauti katika matumizi ya lugha katika kazi ya fasihi. Kwa hiyo, msisitizo unawekwa katika kuisoma kazi inayohusika kwa undani ili kuweza kuvipambanua vipengele mbalimbali vya lugha na kuvielezea.

Pili, nadharia hii inasisitiza kuchagua zana na mbinu zipi za kiisimu zitumike kufuatana na mazingira, mada, lengo na njia zitumikazo katika mawasiliano husika kutegemea na shughuli za kijamii.

Tatu, elimumtindo huangalia matumizi ya lugha, nafsi alizotumia msanii, maelezo au masimulizi, matumizi ya mbinu nyingine za fasihi simulizi ndani ya riwaya na namna alivyoitumia lugha katika kuwachora wahusika na mandhari.

Changamoto inayoikabili nadharia hii ni pamoja na fani kupewa kipaumbele zaidi ya maudhui. Mbili, nadharia ya elimumtindo inatenga kazi ya kifasihi na wakati pamoja na muktadha unaoizaa kazi hiyo. Ndiyo sababu, wahakiki wengine wanaiona nadharia hii kama ufafanuzi wa matini tu.

Mtafiti amehamasika kuongozwa na nadharia hii kutokana na mihimili yake kama ilivyoelezwa hapo juu ingawa zipo changamoto kadhaa zinazoikabili.

### 1.7.1 Nadharia ya Elimumtindo

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya elimumtindo. Hivyo, ukusanyaji wa data, uchambuzi na uwasilishaji wa data ulifanywa kwa kuzingatia misingi ya nadharia hii.

Nadharia hii ilihusishwa na rhetoric (balagha), ambalo limetokana na neno la ki-Giriki '*rhetorike'* lenye maana ya sanaa ya usemaji (Richard 1997). Sanaa inayojishughulisha na uhutubiaji kama mbinu ya kushawishi. Taaluma hii ilianza

kufundishwa kama somo tangu karne ya 15 na masetra wa ki-Giriki. Iliwafundisha wanafunzi namna ya kuunda hoja na kutumia tamathali za usemi katika uzungumzaji na maandishi. Ilichukuliwa kuwa ni sanaa muhimu kwa sababu ilitumika katika siasa na sheria juu ya migogoro ya ardhi na haki za uraia. Mwasisi wa kwanza kueneza na kuhubiri maadili na manufaa ya sanaa ya uzungumzaji ni Socrates akifuatiwa na Plato na Aristotle.

Elimumtindo ni nadharia ambayo hutumia njia na utafiti wa sayansi ya lugha kuchambua kazi za fasihi. Nadharia hii ilianzishwa katika karne ya ishirini kwa lengo la kuonesha namna mbinu za lugha zinavyotumiwa katika kazi za fasihi na athari katika maana ya kazi hizo. Pia inayohusu matumizi ya zana za kiisimu (msamiati na mpangilio wake katika sentensi) na namna zana hizo zinavyoweza kusababisha maudhui tofauti. Uchaguzi wa zana mbalimbali za kiisimu hufanyika kutegemea mambo yafuatayo: kwanza, lengo la mzungumzaji au mwandishi. Uchaguzi wa zana za kiisimu unatofautiana kutegemeana na lengo la mzungumzaji au mwandishi. Kwa mfano, kama mzungumzaji au mwandishi ana lengo la kuelimisha atatumia zana za kiisimu tofauti na mwenye lengo la kuchekesha.

Pili, sifa za mzungumzaji au mwandishi. Kwa mfano, umri wake, elimu yake, utamaduni wake, tabaka lake katika jamii, mambo anayopendelea, hali yake kisaikolojia.

Tatu, sifa za mtu unayewasiliana naye. Kwa mfano, elimu yake, umri wake, ujuzi wake, hali yake kisaikolojia.

Nne ni mada ya mawasiliano. Je wazungumzaji wanaongea kuhusu jambo gani? Lenye kuhuzunisha ama kufurahisha? Je wanazungumzia siasa, uchumi, utamaduni ama sayansi? Mada hizi zote hutofautiana katika uteuzi wa zana za kiisimu zitakazotumika.

Msingi wa elimumtindo ni uchambuzi wa nyanja zote za muundo wa lugha katika usemaji na uandishi. Huhusika na uwezo wa lugha wa kuibua miguso mbalimbali na kanuni za utendaji kazi wa zana za kiisimu katika mazingira yanayotofautiana. Huchagua zana na mbinu zipi zitumike kufuatana na mazingira, mada, lengo na njia zitumikazo katika mawasiliano husika kutegemea na shughuli za kijamii.

Kwa kuwa kazi ya fasihi husanwa kutegemeana na wakati, mahali, utamaduni na mazingira tofauti, kazi ya mtindo ni kueleza na kubainisha mambo yote haya katika kazi ya fasihi. Wahakiki hutumia mtindo kuchunguza lugha na hasa ubunifu katika matumizi hayo ya lugha. Mtindo pia huimarisha uwezo wetu wa kufikiri kuhusu lugha katika kuangalia uelewa wetu kuhusiana na kazi za fasihi.

Hivyo elimumtindo inahusiana na namna ambavyo maneno hupangiliwa ili kuelezea ubinafsi wa mzungumzaji au mwandishi katika kutoa hisia au mawazo yake. Pia inajishughulisha na matumizi ya lugha katika mawasiliano, yaani ubunifu katika utendaji kazi wa lugha. Kila mwandishi ana namna ya pekee katika kutoa mawazo yake tofauti na waandishi wengine. Hivyo kazi ya mtindo katika kazi ya fasihi ni kuelezea na kubainisha wakati, mahali, utamaduni na mazingira ambamo kazi ya fasihi imejitokeza kwa kutumia lugha yenye mvuto. Hii huhusisha matumizi ya tamathali za usemi, ishara na picha katika kuwachora wahusika, kuelezea mandhari ya hadithi, na namna anavyosimulia matukio ndani ya hadithi.

Baadhi ya waanzilishi wa nadharia ya elimumitindo ni Sidney, Lyly na Richard Ohmman katika kipindi cha ufufuo (renaissance period), ambao waliuona mtindo kama vazi la mawazo. Kwa maana kuwa mtindo hubeba mawazo ya mwandishi wa kazi ya fasihi (Leech na Short 1981:16-20). Kwamba mtindo ambao hubeba namna ya uwasilishaji wa kazi ya fasihi ndio humvuta zaidi msomaji wa kazi hiyo kuliko ujumbe uliokusudiwa na mwandishi.

Kwa hiyo, katika utafiti huu nadharia ya elimumtindo ilitumika katika kuchunguza tofauti za kimtindo katika riwaya za upelelezi za MSA na Shigongo. Kwa kutumia msingi wa elimumtindo ambao ni ubunifu katika nyanja za lugha, mtafiti alichunguza namna waandishi hawa walivyotumia ubunifu wa lugha katika kuwachora wahusika, kuelezea mandhari, kuelezea mtiririko wa matukio na dhamira ndani ya riwaya zao. Kisha kulinganisha mitindo yao na kuona ni sababu zipi zimesababisha watumie mitindo hiyo. Nadharia hii imesaidia kuonesha bayana tofauti za matumizi ya zana za kiisimu kati ya waandishi hawa na hivyo kuweza kutofautisha mitindo ya waandishi hawa.

### 1.8 Hitimisho

Baada ya kuangalia sura ya kwanza, iliyozungumzia usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, manufaa ya utafiti, mawanda ya utafiti na nadharia ya utafiti. Sura inayofuata itazumngumzia mapitio mbalimbali ya maandiko kuhusiana na utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya maandiko mbalimbali yanayohusu dhana ya mtindo na riwaya ya upelelezi pamoja na uchambuzi wa maandiko mbalimbali yanayohusu mada hii. Maandiko hayo yamegawanyika katika vipengele sita ambavyo ni maandiko mbalimbali yanayozungumzia, dhana ya mtindo, riwaya ya upelelezi kwa jumla, riwaya ya upelelezi ya Kiswahili, wasifu wa MSA na Shigongo, kazi zao pamoja na tahakiki za maandiko mbalimbali kuhusu mtindo katika riwaya za upelelezi za MSA na Shigongo. Machapisho hayo yametokana na tafiti na chambuzi zilizopatikana katika vitabu, tasnifu, majarida na mtandao (wavuti). Mapitio ya maandiko yanagusia riwaya ya upelelezi ya Kiingereza na riwaya ya upelelezi ya Kiswahili.

## 2.1 Dhana ya Mtindo Katika Kazi za Fasihi

Kwa kawaida kila mtu huwa na mawazo ambayo hupenda watu wengine wayafahamu. Katika kutimiza hili, zipo njia mbalimbali zinazoweza kutumika kufikisha mawazo hayo kwa watu au jamii inayokusudiwa. Njia hizo zitumikazo kufikisha mawazo hutofautiana kati ya mtu mmoja na mwingine na ndizo ambazo baadhi ya wachambuzi na watafiti huziita mtindo wa mwandishi au mzungumzaji. Kwa hiyo, tunaweza kumtofautisha msanii mmoja na mwingine kutegemeana na mtindo anaoutumia. Msanii mmoja anaweza kuwa na mtindo zaidi ya mmoja kutegemea mawazo anayotaka kuyawasilisha kwa hadhira yake.

Kazi ya fasihi iandikwapo hufanyiwa utafiti, uhakiki na kutolewa maelezo ya aina mbalimbali yanayoihusu kazi husika yakiwa na lengo la kusaidia uelewekaji wake.

Tasnifu hii inahusu tofauti za kimtindo katika riwaya ya upelelezi ya Kiswahili kwa kufanya ulinganisho wa MSA na Shigongo. Kipengele hiki kinatoa maelezo yanayohusu dhana za msingi katika tasnifu hii ambazo ni mtindo na riwaya ya upelelezi.

Enkvist (1973) anauelezea mtindo katika mitazamo mitatu. Kwanza, mtindo kama *ukiushi*, pili, mtindo kama *nyongeza* na mwisho, mtindo kama *kidokezo*. Katika kufafanua dhana ya ukiushi, anaona mtindo ni ukiushi wa kaida zilizowekwa au zilizopo. Hapa, uchambuzi wa mtindo hufanywa kwa kulinganisha nduni zilizo katika matini inayoshughulikiwa na zile ambazo zitarejelewa kama kaida. Kwa mfano, uandishi wa riwaya huzingatia lugha ya kinathari, pakitokezea mtunzi atakayeandika riwaya yake bila kuzingatia kipengele hicho, kwa mfano, matumizi ya ushairi ndani ya riwaya, huo utakuwa ni mtindo wa mtunzi huyo. Pia, kaida za ushairi wa kimapokeo sharti uzingatie urari wa vina na mizani, pakitokezea mtunzi atakayeandika ushairi wake wa kimapokeo bila kuzingatia kipengele hiki, huo nao pia utakuwa ni mtindo wa mtunzi huyo. Kimsingi, mwandishi anasisitiza ukiukaji wa taratibu zilizopo katika kusana kazi ya fasihi. Msanii hapa huenda kinyume na utaratibu uliowekwa katika kusana kazi ya fasihi.

Katika kuzungumzia mtindo kama nyongeza, anafafanua kwamba utunzi wa kazi yoyote huwa na vipengele vya msingi ambavyo ndivyo vinaifanya kazi hiyo iwe na hadhi fulani. Kwa mfano, uandishi wa riwaya kama unamtaka mwandishi sharti afikishe idadi fulani ya maneno, ikatokea mtunzi fulani akaandika riwaya yake yenye idadi ya maneno yanayotakiwa. Lakini akaamua kuongeza idadi ya maneno kwa kutumia mbinu nyingine kama nyimbo au ushairi ndani ya riwaya, huo utakuwa ni mtindo wake.

Hapa mtunzi huongezea vipengele vipya ambavyo hapo awali havikuwepo kulingana na kanuni zilizowekwa ili kuifanya kazi yake iwe na mvuto kwa wasomaji au wasikilizaji wake.

Mtazamo wa mtindo kama kidokezo unalenga kuangalia uhusiano uliopo baina ya vipengele mbalimbali vya kiisimu na mazingira halisi ambamo vinatumika. Kwa mfano, matumizi ya lugha zisizo rasmi yanaweza kumbainisha mhusika fulani na mahali au tabaka alilotoka. Hata hivyo mitazamo yote hii mitatu hukamilishana na kutegemeana. Hakuna mtazamo unaotumika peke yake katika mazingira yote. Mitazamo hii inaweza kutofautiana kimatumizi kutegemeana na aina za matini. Kimsingi mitazamo yote mitatu inafafanua dhana ya kwenda kinyume na kanuni zilizowekwa katika utunzi wa kazi za fasihi, kwa maana ya kuongezea vipengele vipya katika utunzi wa kazi za fasihi.

Leech na Short (1981:13) nao pia, wanafafanua dhana ya mtindo kwa kusema: *"style refers to the way in which language is used in a given context, by a given person, for a given purpose"*. Yaani "mtindo ni namna ambavyo lugha hutumiwa na mtu kutegemeana na muktadha kwa lengo maalum".

Mtindo hutumiwa katika mazungumzo na maandishi ya kifasihi na yale yasiyo ya kifasihi. Kihistoria, mtindo hutumika katika kazi za kifasihi. Kwa kawaida uzuri wa fani katika kazi ya fasihi humvuta msomaji kuliko maudhui yaliyobebwa na fani hiyo. Wanaendelea kufafanua kuwa mtindo huhusishwa zaidi na namna mifumo na kanuni za lugha zinavyofanya kazi kuliko mifumo na taratibu hizo. Pia mtindo hutegemea eneo la sanaa lililochaguliwa na msanii, pamoja na ujuzi na maarifa aliyonayo mwandishi kuhusu fani hiyo. Mtindo pia hutegemea ubunifu wa msomaji katika kuelewa matini anayoisoma.

Kimsingi, hapa mtindo hutegemea muktadha na malengo ya msemaji au mwandishi. Hivyo, uteuzi wa maneno huweza kutofautiana kutegemea na muktadha wa usemaji au uandishi na malengo husika. Kwa mfano, mwandishi kama amekusudia kuhuzunisha, uteuzi wa maneno utatofautiana na anapokusudia kuchekesha.

Senkoro (1982:88) anaelezea mtindo kuwa ni namna inayomsaidia msanii kuipa kazi yake ya fasihi sura ya kifani na kimaudhui tofauti na msanii mwingine hata kama jambo linalozungumziwa ni moja.

Mulokozi (1989:52) naye anaona kuwa, mtindo ni tabia ya utungaji ambayo humpambanua mtunzi mmoja na mwingine. Mtindo huumbika katika namna mtunzi anavyotumia maneno yake (kutumia maneno magumu na rahisi, kuchanganya lugha, kutumia methali), jinsi anavyozipanga semi zake (kama ametumia sentensi fupifupi au ndefu, takriri, vibwagizo) na namna anavyoumba tungo zake. Mtindo wa mtunzi humwezesha msomaji kubainisha upekee na uasili wa mtunzi huyo, na pia athari za watunzi wengine kwenye usanii wake.

Hapa mwandishi anasisitiza kwamba mtindo ni upekee wa msanii katika kutumia lugha wakati anapoelezea matukio katika kazi ya fasihi. Namna anavyochagua vipengele vya lugha katika kazi nzima, miundo ya tungo, msamiati na matumizi ya tamathali za semi kwa jumla.

Gibbe (1990), vilevile, anaona kuwa mtindo wa mwandishi ndiyo chumvi ambayo hukoleza na kuipa maonjo kazi yake kwa wasomaji. Zana ya pekee aitumiayo mwandishi kujenga mtindo ni lugha. Lugha ndiyo hujenga taharuki, taswira na mvuto wa kazi ya sanaa kwa wasikilizaji au wasomaji wake. Hivyo, uhakiki wa mtindo hurejelea vipengele vya uteuzi wa maneno katika kujenga taharuki, taswira, tamathali za semi na istiara. Kufanikiwa au kutofanikiwa kwa kazi ya msanii hutegemea namna alivyoitumia lugha katika kusana kazi yake.

Msokile (1992:53) anaelezea mtindo kuwa ni jinsi ya kueleza jambo na pengine aina ya jambo linaloelezwa. Anaendelea kusema kuwa ni vigumu kuona mtindo wa msanii katika kazi moja. Jumla ya usanii wa msanii huunda mtindo wa msanii.

Kwa mujibu wa Haynes (1995) anaelezea mtindo kama namna ya kuteua maneno au vifungu vya maneno kwa umakini katika mazungumzo au maandishi. Uteuzi huu huzingatia mazingira yanayomzunguka msemaji au mwandishi, pia mtazamo wa msemaji au mwandishi kuhusu maisha, maadili, hisia zake na falsafa yake. Hivyo, uteuzi wa maneno hutofautiana kutegemea mazingira yanayomzunguka mwandishi wa kazi ya fasihi, pia mtazamo, hisia na imani yake kuhusu maisha.

Mambo ya msingi yanayoangaliwa hapa ni mazingira na mtazamo wa msemaji au mwandishi. Hivyo, uteuzi wa maneno hutegemea msemaji au mwandishi anayatazama vipi maisha kwa jumla.

Kahigi (1997) kupitia mawazo ya wataalamu waliotangulia, wakiwemo G. Leech na M. Short (1981) ameangalia mtindo katika mitazamo miwili. Mtindo kama *uteuzi* na mtindo kama *tofauti.* Katika kuangalia mtindo kama uteuzi, anasisitiza kuwa mzungumzaji au mwandishi huteua vipengele maalum miongoni mwa vipengele vilivyomo katika lugha husika na kuvitumia katika kazi za fasihi. Mawazo haya katika mtazamo huu yanalingana na yale ya kina Crystal na Davy (1969:77) waliposisitiza kwamba, uchambuzi wa mtindo hauwezi kufanywa kwa kutumia vipengele vyote vya lugha, kwani lugha ni pana zaidi na mtindo ni sehemu tu ya matumizi ya lugha. Hivyo basi, uchambuzi wa mtindo unapaswa ujikite katika vipengele ambavyo vitamtofautisha msanii mmoja na mwingine.

Mtindo kama tofauti unachukuliwa kama ni yale mambo yanayovitofautisha vipengele vya lugha vilivyotumiwa katika kazi fulani na kaida zilizopo. Hapa ikumbukwe kwamba kila uwanja una kaida zake. Kwa mfano, kuna kaida za

uandishi wa barua, ushairi, tamthiliya, riwaya, kwa kuvitaja vichache. Hivyo, tunapochambua mtindo kwa kuzingatia mtazamo huu tunaangalia tofauti iliyopo ya vipengele vya lugha baina ya kazi tunayoichambua na kaida za kiisimu zilizopo. Kwa mfano, katika uandishi wa tamthiliya kuna kaida zake, akitokea msanii akaandika kinyume chake, huo utakuwa ni mtindo wake. Mtazamo huu unafanana na ule wa mtaalam Enkvist (ameshatajwa), unaouangalia mtindo kama ukiushi, kwa sababu kuna mtunzi wa aina hii anayefanya kitu ambacho ni tofauti na wengine, lakini pia anakiuka kaida zilizowekwa.

Njogu (1999:93) anafafanua kuwa hakuna njia moja ya kueleza neno mtindo, lakini kwa ujumla tunaweza kusema kwamba mtindo ni tabia ya utungaji inayompambanua mtunzi mmoja na mwingine. Anaendelea kueleza kuwa baadhi ya maswali ya kujiuliza kuhusu mtindo ni haya; mtunzi ametumia maneno magumu ya lahaja? Kwa nini?, mtunzi amechanganya lugha?, ameumbaje tungo zake? n.k.

Cuddon (1980) akinukuliwa na Oriedo (2000) ameelezea kuwa mtindo ni tabia au namna ya kujieleza katika kazi ya fasihi na jinsi mwandishi anavyosema au kuandika mambo yake. Hujumuisha mambo kama mbinu za matamshi, umbo la sentensi, umbo la aya na anavyotumia lugha kwa ujumla.

Aidha, Wamitila (2002:19) anaufafanua mtindo kama jumla ya mbinu zinazomwezesha msanii kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira. Mtindo huelezea jinsi msanii anavyoisana kazi yake. Pia anafafanua baadhi ya mambo ya msingi tunayopaswa kuyaangalia tunapotaka kubainisha mtindo; uteuzi wa msamiati, mpangilio wa matukio, tamathali za semi, taswira na jazanda, usawiri wa wahusika na mandhari.

Barry (2002) anafafanua dhana ya mtindo kuwa imetokana na taaluma ya ki-Giriki iliyoitwa '*rhetoric'* (balagha), ambayo iliwafundisha wanafunzi namna ya kuunda

hoja, namna ya kutumia tamathali za usemi katika mazungumzo au maandishi, na namna ya kutathmini mazungumzo au maandishi hayo. Wakati wa zama za kati balagha ilitumika kufundisha watu kanisani, sheria na siasa au maisha ya kidiplomasia. Lakini baadaye ikajikita katika lugha na hasa uainishaji wa tamathali za usemi katika matumizi ya lugha.

Hapa kinachosisitizwa ni kwamba mtindo unahusika na ubunifu katika matumizi ya lugha. Namna mzungumzaji au mwandishi anavyoteua maneno kutegemeana na wakati, mazingira, na utamaduni wa jamii husika. Kwa kuangalia fafanuzi za wataalam hao, tunaweza kusema kuwa, mitazamo yote ina mawazo yanayoingiliana na kutegemeana. Jambo la msingi linalosisitizwa hapa ni kuwa uchambuzi wa mtindo unajikita zaidi katika utumizi wa lugha na unapaswa kulenga tu vipengele ambavyo vinamtofautisha mtunzi mmoja na mwingine. Hii ni kwa sababu kila mtunzi anapoandaa kazi yake hulazimika kuteua vipengele fulani mahsusi ili kufikisha ujumbe wake kwa hadhira. Mtunzi huweza kutofautiana na wenzake kwa kutumia vipengele ambavyo havijatumiwa na watunzi wengine katika kazi za fasihi.

### 2.1.1 Maandiko Kuhusu Mtindo Katika Kazi za Fasihi

Zipo kazi mbalimbali zilizowahi kushughulikia kipengele cha mtindo, ikiwemo kazi ya Omari (2006) aliyeangalia mtindo katika nyimbo za *Bongo Freva*. Katika kazi hii amebainisha baadhi ya mitindo kama vile matumizi ya majigambo na kuchanganya lugha. Kutokana na uchunguzi wake alibaini kuwa nyimbo nyingi za *Bongo Freva* hutumia mbinu hizi mbili, yaani majigambo na kuchanganya lugha.

Mohamed (2006) akiangalia mtindo katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* amefafanua matumizi ya uwili na ameonesha kwamba baadhi ya maneno huenda sambamba pale yanapotumika. Kwamba neno moja likitumika tunajenga fikra kuwa kuna jingine. Baadhi ya wachambuzi hupenda kuyaita maneno tangamano. Maneno

haya huweza kutumika kuonesha umoja na mshikamano. Baadhi ya maneno aliyoyatumia kuonesha uwili ni msikiti na kanisa, pia Uislamu na Ukristo. Mwandishi anatumia Msikiti na Kanisa kuonesha namna taasisi hizi zilivyopoteza mwelekeo na malengo ya kuanzishwa kwake. Mbali na matumizi ya uwili, amefafanua pia matumizi ya mtindo wa ushairi kwa ajili ya kusisitiza jambo na matumizi ya vilugha.

Mwita (2009) ameangalia uhakiki wa mitindo na maudhui katika baadhi ya tamthiliya za Mlama na ameangalia tamthiliya ya *Hatia* (1972), *Pambo* (1975), *Tambueni Haki Zetu* (1975) na *Heshima yangu* (1974). Katika tamthiliya hizi amegundua mitindo kama matumizi ya nyimbo ambayo yamebeba maudhui ya kuonesha mjini na shamba ni tofauti. Matumizi ya mchezo ndani ya mchezo ambayo yalibeba maudhui ya kuwa wasomi wanapomaliza masomo hutarajia maisha ya raha na starehe, jambo ambalo hawafanikiwi na vyeti vyao kubaki pambo tu. Pia matumizi ya mandhari ya kuzimu yaliyobeba maudhui ya mtu kudai haki sawa.

Senkoro (ameshatajwa) amegusia matumizi ya mtindo katika kazi za fasihi kupitia dhana ya taharuki. Anasema:

> Taharuki ni hali ya kusisimshwa kwa hadhira kutokana na shauku ya kutakaa kujua jinsi mambo yatakavyojiri katika sura ama sehemu zijazo za kazi ya fasihi. Hali ya taharuki hujengwa makusudi na msanii ili kumfanya msikilizaji, mtazamaji au msomaji aendelee kusubiri litakalotokea.

Hapa Senkoro ametoa maelezo machache kuhusiana na matumizi ya taharuki katika kazi ya fasihi.

Kimsingi kazi za wahakiki hawa zimetoa mwanga katika kufanya utafiti huu kwa sababu zinaangalia namna vipengele vya lugha vinavyoweza kutumiwa na mwandishi katika kazi ya fasihi na kuleta upekee. Hata hivyo wahakiki hawa

hawajaeleza ni kwa namna gani wamevitumia vipengele hivi vya lugha kuumba wahusika na mandhari katika kazi zao pia ni sababu zipi zimewafanya watumie vipengele kama majigambo, nyimbo n.k.

## 2.2 Riwaya ya Kipelelezi kwa Ujumla

Edgar Allan Poe, mwandishi, mshairi, mhariri na mhakiki wa kazi za fasihi nchini Marekani kati ya miaka ya 1830 na 1840, aliweka misingi na mbinu za utunzi wa riwaya ya upelelezi. Misingi hiyo inajumuisha kuwepo kwa mtuhumiwa anayesingiziwa, kosa lililotendeka mahali palipojificha na utatuzi wa tatizo kwa njia isiyo ya kawaida. Kimsingi Poe anaona kuwa mambo hayo matatu yanatumika kama nguzo katika suala zima linalohusiana na utunzi wa riwaya ya upelelezi. Na bila kuzingatia mambo hayo riwaya ya upelelezi haiwezi kuwa imekamilika.

Ronald Knox (1929) katika makala yake ya *Description of the Genre* alizungumzia kanuni za kutunga kazi ya riwaya ya upelelezi. Baadhi ya kanuni hizo ni pamoja na mhalifu kutajwa tangu mwanzoni mwa hadithi, lakini msomaji asimtambue mapema, nguvu za asili hazitumiki na mpelelezi kutatua tatizo kwa kutumia akili na mbinu za hali ya juu sana, mpelelezi haruhusiwi kutoa madokezo anayoyagundua, na rafiki mjinga wa mpelelezi uelewa wake uwe ni mdogo kuliko wa msomaji.

Ikumbukwe kwamba kanuni hizi za riwaya ya upelelezi zilitolewa kipindi ambapo hapakuwa na riwaya ya upelelezi ya Kiswahili. Lakini ukizichunguza riwaya za upelelezi za Kiswahili utagundua kuwa zina sifa zinazotajwa na wataalam hao.

## 2.3 Riwaya ya Upelelezi ya Kiswahili

Riwaya ya upelelezi ya Kiswahili ni riwaya iliyopata mashabiki wengi tangu ianze kuandikwa hapa Tanzania tangu miaka ya 1960 na inajulikana kama riwaya pendwa kwa sababu inasomwa na watu wengi kuliko aina nyingine ya riwaya. Kazi ya

kifasihi kwa kawaida hujumuisha vipengele vyote vya kifani na kimaudhui vikiwemo; mtindo, muundo wahusika, mandhari, dhamira, matumizi ya lugha, ishara na taswira. Mtindo wa kazi moja ya fasihi huweza kutofautiana au kushabihiana na mwingine. Ubunifu wa mtunzi husababisha kuivuta hadhira na kuiweka katika hali ya kusoma kazi yake bila kuchoka.

Madumulla (1988) anaeleza kuwa riwaya pendwa ni:

> Riwaya inayojihusisha na masuala ya mapenzi, upelelezi na ujasusi, ambapo mara nyingine katika ufuatiliaji wake kuna mapigano makali ya kimwili au kiakili kati ya mtu mmoja au wachache na watu wengi. Matokeo yake ni kuwa mtu mmoja anawashinda walio wengi.

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996: 154), riwaya ya upelelezi ya Kiswahili ni hadithi ya kubuni yenye mpangilio na mtiririko wa kimantiki na visa na matukio yaliyotawaliwa na kisa cha upelelezi unaofanywa na polisi au mtu binafsi kwa kujitolea. Ujengaji wa visa unaoleta taharuki ni muhimu sana na ndio humfanya msomaji kutopumzika mara aanzapo kusoma riwaya ya upelelezi hadi amalize kusoma.

Anaendelea kueleza kuwa riwaya ya upelelezi ya Kiswahili huwa na mambo mawili ya msingi; kosa la uhalifu na mpelelezi wa uhalifu huo hadi mhalifu anapopatikana (uk: 161). Vitu hivi ndiyo msingi wa riwaya ya upelelezi na hadithi yenye kisa cha upelelezi. Uchunguzi hufanywa na mpelelezi anayelitafutia ufumbuzi tatizo kwa kufanya uchunguzi.

Wahakiki, wachambuzi na watafiti wa riwaya ya upelelezi ya Kiswahili wamekuwa na mitazamo tofauti juu ya riwaya hizi. Kuna mitazamo miwili iliyozua mjadala mrefu na imedumu hadi sasa. Riwaya ya upelelezi kwa upande mmoja inadaiwa kuwa inachangia kufundisha mbinu za kufanya uhalifu katika jamii na kwa sababu hiyo haifai kwani haioneshi matatizo yaliyomo ndani ya jamii. Kwa upande mwingine inaelezwa kuwa ni riwaya inayomulika matatizo katika jamii. Kwani

huifundisha na kuionya jamii kuwa uovu haulipi siku zote na mwisho wake ni mbaya. Mitazamo hii inatawala hadi sasa kutegemeana na mtazamo binafsi wa mhakiki, mchambuzi au mtafiti wa kazi ya fasihi.

Kimsingi, ni wazi kwamba riwaya ya upelelezi ya Kiswahili ina chukua sura hizo mbili kuwa ikitumiwa vibaya inaleta madhara katika jamii na ikitumiwa vizuri kama kazi nyingine ya fasihi huifunza na kuionya jamii.

Riwaya ya upelelezi ya Kiswahili ina sifa za msingi sana ambazo ni kuwa na tatizo linalotakiwa kupatiwa ufumbuzi na mpelelezi. Riwaya hizi huwa na kisa cha kusisimua ambacho msomaji huhitaji umakini na utulivu wa hali ya juu kwenda sambamba na mpelelezi ili aweze kung'amua aliyetenda kosa na kwa sababu gani anaona ndiye mkosaji. Kushindwa kwa msomaji kuunganisha matukio, wakati mwingine kupoteza visa vidogo vidogo vinavyoibuka na utumiaji wa wahusika wengi katika riwaya husika husababisha utata kwa msomaji kuelewa mpelelezi ametatuaje tatizo.

Matumizi ya mandhari zinazotisha kama 'mzimu' katika riwaya ya *Mzimu waWatu wa Kale*, wahusika wake wengi na hasa mhusika mkuu kutofafanuliwa kwa taarifa zake nyingi zinachangia kumtatiza msomaji kuelewa kwa urahisi. Ukwezwaji wa mhusika mkuu kwa kumpa akili zaidi ya wahusika wengine kunachangia kuwepo na mtazamo kuwa kuna maajabu yasiyoelezeka katika utatuzi wa tatizo. Kwa mfano, Willy Gamba ambaye ni mhusika mkuu katika riwaya za Elvis Msiba, Joram Kiango, mhusika mkuu katika riwaya za Ben Mtobwa na Bwana Msa katika riwaya za MSA ni mifano ya wahusika waliokwezwa. Pia utumiaji wa muundo rejeshi husababisha riwaya ya upelelezi kutofuatika vizuri kwani msomaji wakati mwingine hushindwa kuunganisha matukio.

### 2.3.1 Maandiko Kuhusu Riwaya ya Upelelezi ya Kiswahili

Zipo tafiti na tahakiki mbalimbali zilizofanywa kuhusu riwaya ya upelelezi ya Kiswahili.

Kezilahabi (1976: 36-37), alihakiki riwaya za upelelezi za *Mzimu wa Watu wa Kale, Kisima cha Giningi, Duniani Kuna Watu, Siri ya Sifuri, Simu ya Kifo na Mbojo Simba Mtu*. Alieleza kuna mambo matatu muhimu yasaidiayo katika uandishi wa riwaya hizi. Mambo hayo ni pamoja na mwandishi awe na uwezo wa kutumia hali nzuri ya hewa na mazingira katika kujenga hali, yaani muoano mzuri wa kueleza mazingira au kitu kilivyo, yaani kishabihiane na matendo afanyayo au tabia yake. Mwisho ni uwezo wa kuficha sababu za tukio linalofanyiwa uchunguzi. Ujanja wa kutoa habari kidogo kidogo hutumika na utumiaji wa wahusika wengi ambao sisi wasomaji tutawatilia mashaka kama kweli wanahusika na tukio hilo au la.

Kuficha sababu za tatizo ni muhimu ili kujenga taharuki na kusaidia riwaya ilete mvuto na kumfanya msomaji asitumie akili kung'amua nani aliyetenda kosa na kwa sababu gani.

Vilevile, Kezilahabi (1980) katika makala yake ya *Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi* amezungumzia riwaya ya upelelezi na mauaji kama matatizo ya kimaudhui. Anadai kuwa wapo wahakiki wanaoona zinafaa kwa sababu humsaidia mtu kuwa mwangalifu na yatendekayo. Aliona waonao hivyo hawazingatii athari mbaya zinazoletwa na maandishi ya aina hii kwani hayawapatii wananchi picha iliyo sahihi kuhusu ukweli wa maisha yao.

Wazo hilo liliungwa mkono na Madumulla (1987) aliyeenda mbali zaidi kwa kuona kuwa zinastawisha uhalifu kwa kuwafundisha wahalifu njia mpya ya kufanyia uhalifu. Kezilahabi aliona ni riwaya moja tu ya *Kufa na Kupona* illiyotetewa kwa dhati kwa kuweka misingi mipya ya upelelezi katika fasihi ya Kiswahili. Anatumia

mawazo ya mwanafasihi Senkoro aliyeona kuhalalishwa kwa matumizi ya nguvu kuhusu suala la kupigania uhuru.

Kimura (1991) alifanya utafiti kuhusu mabadiliko ya kijamii na riwaya ya upelelezi Tanzania. Katika utafiti huu aligusia riwaya ya upelelezi ya Kiswahili iliyoanza kuandikwa wakati wa ukoloni. Aliona kuwa kwa Tanzania baada ya mfumo wa polisi na mahakama kuanzishwa, mbinu za upelelezi za kimagharibi zilianza kutumika kumpata mhalifu. Hivyo, imani za kijadi zilizokuwa zinatumika kufichua aliyetenda kosa hapo kabla katika hadithi zenye kisa cha upelelezi, zilianza kufifia na kuachwa kutumika kumpata mhalifu. Anataja matumizi ya simu katika *Simu ya Kifo* ya Faraji Katalambulla, ambayo mhalifu alitangaza matendo yake kwa polisi kwa njia ya simu.

Hapa wahakiki na watafiti wamezungumzia maudhui ya riwaya ya upelelezi na kuona kuwa inastawisha uhalifu katika jamii. Mtafiti anaona kuwa riwaya ya upelelezi ina nafasi kubwa ya kuibua uozo unaofanyika ndani ya jamii ikitumiwa vizuri kwa sababu inafafanua mambo yanayoikumba jamii iliyoandikiwa kazi hiyo.

Watafiti pia wamezungumzia vipengele mbalimbali vinavyoitambulisha riwaya ya upelelezi ya Kiswahili na hivyo vimemsaidia mtafiti kuitambua riwaya ya upelelezi ya Kiswahili na hivyo kumsaidia kuweza kulinganisha mtindo wa waandishi MSA na Shigongo ili kubaini tofauti za kimtindo katika kazi za fasihi.

## 2.4 Bwana MSA na Kazi Zake

MSA ni mwandishi mwanzilishi wa riwaya ya upelelezi ya Kiswahili nchini Tanzania hata wachambuzi na wataalamu wengine wanamchukulia kama baba wa riwaya pendwa. Kimsingi alianza kuandika kazi zake miaka ya 1950, kabla ya uhuru.

### 2.4.1 Wasifu wa MSA

Kwa mujibu wa Mjawiri (2011), MSA alizaliwa mnamo tarehe 25 mwezi wa pili mwaka 1918 katika mtaa wa Funguni, Malindi, Mji Mkongwe, Zanzibar. MSA alizaliwa peke yake katika familia ya Bwana Said Abdulla mwenye asili ya Yemen. Bwana Abdulla alifanikiwa kupata watoto wanne ambao ni Bi Salma, Bwana Said, Bwana Massad na Bi Mgeni. Bi Salma alibahatika kupata watoto wawili nao ni Bi Sheikha na Bi Khadija ambao kwa mujibu wa taratibu za dini ya Kiislamu, ndiyo warithi halali walio hai. Bwana Said Abdulla alizaa mtoto mmoja tu kama ilivyoelezwa hapo juu. Mtoto wa tatu wa Bwana Abdulla ni Bwana Massad ambaye hakujaaliwa kupata watoto na wa mwisho ni Bi Mgeni ambaye alizaa mtoto mmoja tu aitwaye Mahfudha. Mama wa MSA aliitwa Bibi Anoi binti Mselem wa ukoo wa Al- Khalas kutoka Maskat, Uarabuni. Katika maisha yake ya ndoa, MSA alibahatika kupata watoto wanne; Abdulrahman, Khadija, Fatma na Saide.

Mjawiri anafafanua kuwa raha ya ndoa ni kupata watoto. Ikiwa hivyo ni sawa basi MSA aliishuhudia na kuwalea vyema watoto wake kwa kuwapeleka shule kujifunza elimu ya magharibi. Kwa mujibu wa Khamis (2011), anadaiwa kuwa Khadija na Fatma walikuwa mfano wa kuigwa shuleni na hata mitaani. Mauti yaliwakuta wakati wakijitayarisha kuendelea na masomo ya juu. Inasemekana watoto wake wote wa kike walifariki pamoja na mama yao wakati wa Mapinduzi ya mwaka 1964. Huu ulikuwa ni mtihani mkubwa kwa mwandishi huyu. Hata hivyo, aliweza kusubiri na kumeza machungu hatua kwa hatua hadi kiwewe kikapotea. Aidha, mtoto wake Abdulrahman alikuwa fundi mitambo katika '*Sauti ya Tanzania Zanzibar*' na mwimbaji katika kikundi cha *Naad Ikhwan Saffaa* cha Malindi Zanzibar hadi mauti yanamfika. Abdulrahman alikuwa na uwezo na kipaji cha kuimba nyimbo za Kiarabu.

Katika utoto wake, MSA alikuwa anapenda kucheza michezo mingi ya kitoto kama vile kuokota vitu majaani, kuogelea, kucheza kandimu, foliti, ukuti, kuvua, mbio na kufukuzana. Hakuwa na tabia tofauti na watoto wengine katika mitaa yake ya Malindi na Kokoni. Katika enzi za utoto wa msanii huyu, mitaa hiyo ilikuwa kitovu cha ustaarabu wa kisasa na elimu ya dini na dunia. Hivyo, athari za ustaarabu huo zilianza kumjenga na kumlea mapema. Itakumbukwa kuwa mwanzoni mwa karne ya ishirini, mitaa hiyo ya mji Mkongwe ilikuwa kituo na kilele cha ubora wa elimu ya dini ya Kiislamu na kituo cha elimu ya magharibi. Mambo yaliyomjenga MSA kifikra, kimawazo na kifalsafa.

MSA alizaliwa enzi za ukoloni, wakati ambapo elimu rasmi ya kimagharibi ilikuwwa ikitolewa katika misingi ya ubaguzi. Hata hivyo, alibahatika kupata fursa ya kusoma katika mifumo yote miwili, madrasa kujifunza kusoma Kuran ambapo mwalimu wake alikuwa Bwana Saleh bin Ali na shuleni alijifunza masuala ya kidunia. Alijiunga na shule ya serikali mwaka 1928 kwa masomo ya msingi. Kutokana na uhodari wake na umakini katika kuzingatia masomo yake, alifanikiwa kuendelea na masomo ya sekondari mwaka 1938 katika shule ya serikali ingawa mitihani ilikuwa na ushindani mkubwa. Inadhaniwa kuwa msingi alioupata katika kujifunza elimu ya magharibi ndio uliomfanya kwanza kujua kusoma na kuandika hati ya kirumi, kujua kiingereza, historia, fasihi, geografia, falsafa na uwezo wa kufahamu masuala kadhaa ya kiulimwengu kupitia maandishi ya kizungu. Masuala haya yanajidhihirisha waziwazi katika kazi zake za kifasihi, na hata maongezi yake kwamba alisoma na kufahamu kutumia elimu ya magharibi katika maisha yake ya fasihi na maisha yasiyo ya kifasihi kwa jumla. Aidha, athari za elimu ya dini ya Kiislamu zinajitokeza katika maisha ya MSA wakati wa uhai wake lakini pia katika riwaya zake. Jambo hili linashadidia kuwa msanii huyu amesoma vitabu kama; *fiqhi,*

*tawhid, sira, tarikh*, na *tafsiri ya kuran*. Hivyo, jambo hili linaashiria kuwa ameisoma dini ya kiislamu kwa mapana yake.

Baada ya kuhitimu masomo ya sekondari, MSA aliajiriwa katika idara ya Afya kama Afisa Afya hadi mwaka 1958 ajira yake ilipokatishwa kwa sababu ya kutozingatia nidhamu ya kazi. Hata hivyo, baadaye alifanya kazi nyingine katika gazeti la *Mkulima* akiwa mhariri. Mkosi uliendelea kumsakama kwani mnamo mwaka 1968 aliachishwa kazi ya uhariri. Mjawiri (ameshatajwa) anadai kuwa MSA hakuwa mtu wa kukata tamaa ingawa alikuwa na sababu ya kufanya hivyo. Hatimaye alifanikiwa kupata kibarua cha kutayarisha kipindi cha redio kilichoitwa *Sadiki Ukipenda* katika Sauti ya Unguja. Kazi hii aliimudu vyema na kupata ufanisi wa hali ya juu katika kukiendesha kipindi hiki, jambo ambalo lilimfanya pia kupanua tajriba yake ya masuala ya maisha ambayo yalimsaidia kupevusha kazi zake za sanaa. MSA aliaga Dunia mwaka 1992 Kikwajuni na akazikwa katika makaburi ya Mwanakwerekwe Zanzibar.

### 2.4.2 Kazi za MSA

Katika miaka 74 aliyoishi katika uso wa Dunia, MSA alipitia ngazi mbalimbali za maisha. Alitumia muda wake mwingi katika kushughulikia sanaa na kufanikiwa kubuni sanaa iliyopevuka. MSA alifanikiwa kutunga kazi nyingi ikiwemo miswada ambayo hakuwahi kuichapisha. Hadi kifo chake, MSA aliweza kutunga riwaya saba na hadithi fupi moja na insha kadhaa: *Mzimu wa Watu wa Kale* (1957). *Kisima cha Giningi* (1968), *Duniani Kuna Watu* (1973), *Siri ya Sifuri* (1974), *Mke Mmoja Waume Watatu* (1975), *Mwana wa Yungi Hulewa* (1976), na *Kosa la Bwana Msa* (1984). Aidha, insha ni pamoja na *Bwawani Hoteli Utukufu wa Funguni na Mchuchu si Mchumba*. Kutokana na ukomavu wa usanii wake, mwandishi alifanikiwa kupata

tuzo. Miongoni mwa riwaya zilizompatia tuzo ni *Mzimu wa Watu wa Kale* na *Kisima cha Giningi*.

Kwa mujibu wa Khamis (ameshatajwa) "MSA ni mwalimu wa waandishi wa Zanzibar". Dai hili limepata mashiko kwa sababu ni miongoni mwa waandishi wa awali wa Zanzibar walioandika kazi zao tangu katika kipindi cha ukoloni. Anaendelea kufafanua kuwa, miongoni mwa mambo aliyojifunza kwa kazi za sanaa za MSA ni pamoja na uchoraji wa wahusika, mazingira, malezi, masuala ya dini, dunia, utamaduni na uhusiano wa watu. Mwandishi anaendelea kusema kuwa MSA amejengeka vizuri sana katika ujana wake kama walivyojengeka kwa nyakati na maeneo yao tofauti waandishi wengineo. Kauli ya Khamis inathibitisha kuwa mtindo anaoutumia MSA unatokana na athari za kimazingira, maumbile ya vitu, mitindo mbalimbali katika dunia ambayo MSA hakuweza kuepukana nayo na hasa maisha ya jamii aliyoishi. Kwa mfano, namna anavyochanganya lugha kwa kutumia wahusika katika riwaya zake inaonesha mazingira halisi yaliyomzunguka mwandishi, mwingiliano wa tamaduni katika kipindi alichoishi na maisha ya watu wanaomzunguka kwa ujumla.

Kisanii, MSA ameathiriwa sana na waandishi wa Ulaya kama vile Arthur Conan Doyle. Khamis anaamini kuwa athari za Holmes ni jambo lililo dhahiri. Jambo hili halikutokea kwa bahati mbaya bali lilikusudiwa baada ya MSA kuathiriwa na kazi za Edgar Allan Poe na A.R. Freeman ambao ni waandishi mashuhuri wa riwaya za upelelezi. Mjawiri (ameshatajwa), akimkariri Ghassany (2003), anasema kwamba unapovutiwa na mtu ni wazi kuwa unaathiriwa naye na unapoathiriwa naye huwa unataka uwe kama yeye. Kwa kupitia athari hizo ndipo Khamis (ameshatajwa) alipoandika kuwa Bwana MSA ni Sherlock Holmes wa Afrika. Kwa mujibu wa Mjawiri tabia za kuigana, kufanana na kuathiriana kimtindo katika fasihi ya

Kiswahili zinadhihirika kwa waandishi weingine. Said Ahmed Muhammed, kwa mfano ameathiriwa kwa namna fulani na Muhammed Suleiman Muhammed na MSA kwa kuwataja wachache. Lakini kuigana haimaanishi kunakiliana, bali chochote kinachoigwa hufanyiwa mabadiliko na mageuzi ili kifanane na vionjo vya jamii husika. Hivyo, mtafiti amedhani kuwa mitindo ya waandishi wa kazi za fasihi inatofautiana hasa kwa kuegemea kigezo cha matumizi ya lugha katika uumbaji wa fani katika kazi za riwaya kwa kuwachunguza MSA na Shigongo ambao hawajafanyiwa ulinganisho bado.

Tukiangalia kwa ujumla historia ya MSA, tunaweza kuona kwamba ina athari kubwa katika uumbaji wa fani katika riwaya zake. Kwa mfano, mandhari anayoitumia inaonesha mazingira ya Zanzibar sehemu aliyoishi muda mwingi katika uhai wake. Pia namna anavyotumia lugha, uteuzi wa maneno; ametumia maneno mengi ambayo yanaonesha athari za dini ya kiislamu, dini ambayo imetawala eneo kubwa la Zanzibar. Uteuzi wa majina ya wahusika katika riwaya zake pia umeathiriwa na itikadi ya kiislamu. Hivyo imemsaidia mtafiti katika kupambanua ni kwa sababu zipi mwandishi MSA ametumia mtindo anaoutumia katika kazi zake zote za riwaya.

### 2.4.3 Maandiko Kuhusu Kazi za MSA

Riwaya za upelelezi za MSA zinaonekana kufanyiwa tafiti zaidi kwa vipindi tofauti. J.C.William (1972-73) katika jarida la *Mulika* namba 3, alihakiki riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Aliona muundo wa hadithi hii unatatanisha wengi kidogo (uk: 33-36). Anaendelea kueleza imekuwa hivyo kwa sababu hadithi imeanzia mahali ambapo haikupaswa kuanzia, kwani muundo uliotumika ni ule wa rejea. Alimpongeza MSA kwa ufundi wake, namna alivyoanza na kuimalizia hadithi hii, alivyochora picha za wahusika hata msomaji akapata picha zao. Anaeleza migogoro michache iliyopo katika hadithi hii ikiwa ni pamoja na mwandishi kumzidishia

mpelelezi uwezo wa kufahamu mambo mpaka msomaji kujiuliza kama Bwana Msa ni mpelelezi au ni jini?

Ni makala hiyo ya J.C.William iliyomsukuma S.A.Mohamed kuandika makala ya "Bwana Msa Si Jini" katika jarida la *Mulika* namba 5 1973. Yeye anaona kuwa Bwana Msa hakuzidishiwa uwezo wa kufahamu mambo na si jini. Anaona kuwa labda alichozidishiwa ni uwezo wa kudadisi, kupima na kuweza kuyanyambua na kutoa uwezekano kutokana na mazingira. Bwana Msa anaonekana alikuwa na upeo mkubwa wa kufikiri na kuelewa mambo, ila ilikuwa ni vigumu kumpata mtu kama yeye Unguja (S.A.Mohamed 1973:41-47). Mawazo kama hayo yanajitokeza kutokana na namna mwandishi alivyoitumia lugha kuelezea matukio yanayofanywa na wahusika katika kazi zake.

Mfamau (2007) ameandika tasnifu yake kuhusu ukweli na uhalisia wa kazi za fasihi za Bwana MSA. Hapa ametumia riwaya za MSA kuangalia namna gani mawazo anayoyajadili na ujumbe anaoutoa vinavyousawiri uhalisia wa jamii aliyoiandikia. Hivyo, tumeona ni vema kwenda mbele zaidi kwa kuangalia kipengele cha mtindo kwa kumlinganisha na Shigongo ambaye ni mwandishi wa riwaya za kihalifu na kipelelezi na anayeishi wakati na mazingira tofauti.

Madumlla (2009) aliandika kitabu kiitwacho *"Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi."* Mojawapo ya mambo aliyoyazungumzia ndani ya kitabu hiki ni mikondo mbalimbali ya riwaya ya Kiswahili. Katika kufafanua mikondo hii anamuelezea MSA kama mwandishi mwanzilishi wa riwaya pendwa nchini Tanzania katika karne ya 20. Alifungua mlango kwa kuandika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* (1957). Pia anausifu umahiri wake, hasa ufundi wake katika kuitumia lugha na umakini katika matumizi ya muktadha, kwa maana ya udadisi alionao katika kuchunguza na kufuatilia matukio kwa karibu sana. Hata

hivyo, maelezo katika kitabu hiki bado yanatuachia pengo kubwa ambalo tunapaswa kuliziba kwa kulinganisha mitindo wanayotumia waandishi wengine, hususan Shigongo.

Hamad (2011) aliandika makala inayoitwa *"Matumizi ya Lugha katika Riwaya za Muhammed Said Abdulla."* Kwa jumla, aliangalia namna MSA alivyomahiri katika kutumia lugha aandikapo riwaya zake. Katika makala haya ameeleza namna MSA alivyotumia lugha vizuri katika riwaya zake zikiwemo *Mzimu wa Watu wa Kale* na *Kosa la Bwana Msa*. Akiendelea kujadili riwaya hizi, Hamad anatueleza kuwa kazi hizi zina matumizi mazuri ya visawe, tamathali za semi, upangiliaji mkubwa wa maneno, methali, misemo, tanakali za sauti na lahaja. Kwa mfano, anafafanua vizuri namna MSA alivotumia vizuri visawe au maneno yanayofanana na yanayokaribiana kimaana katika riwaya zake. Kwa kutumia maneno haya bila kuyachanganya, ameweza kueleza kwa ufasaha jambo lililokusudiwa. Kwa mfano, katika *Kosa la Bwana Msa* mwandishi ametumia visawe kwa mpangilio mzuri wenye kuleta maana kulingana na mazingira ya utokeaji wa matendo ya wahusika. Kwa mfano, mwandishi anapoelezea kitendo cha Jamila kuondoka Chwaka kwa haraka na wasiwasi kwenda mjini kwa Mwatenga anasema: "Jamila alisahau kuchukua alipoondoka kwake kwa *haraka* na *wahaka*, hasa chupa ya maziwa na podari ya mtoto" (uk: 49). Utafiti huu umeona ni vema kulinganisha mtindo wa mwandishi huyu na waandishi wengine ili kubaini tofauti na sababu zinazosababisha tofauti hizo.

Hamad anaendelea kufafanua kuwa MSA katika uandishi wake anapenda kukamilisha usanii wake kwa kutumia mbinu mbalimbali za lugha. Anatumia tamathali za semi, methali, misemo, takriri za maneno, tanakali za sauti na lahaja. Vyote hivi huvijenga kwa maneno teule yenye kusadifu maudhui na kumpa sifa ya

kuandika lugha inayobadilikabadilika na isiyomchosha msomaji. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* (uk: 35) anasema: “Kichwa cha Seti B. Sumatra kilikuwa na kipara, hakioti nywele kama jangwa la Sahara.

Issa (2011), kwa namna fulani ameangalia riwaya za MSA zinavyomchora mwanamke. Mwanamke anachorwa kwa namna mbalimbali kutegemeana na maumbile yake kibaiolojia, itikadi na mila zinazomzunguka. Anaendelea kufafanua namna taswira ya mwanamke inavyochorwa katika riwaya za MSA. Katika *Mzimu wa Watu wa Kale* kwa mfano, mwanamke anachorwa kama pambo. Hapa mwandishi anatumia lugha ya mguso kumwelezea mhusika Kipwerere. Anamuelezea mwanamke huyu kimaumbile kwa kumfananisha na vitu vyenye kuvutia macho, mguso na mnuso. Mwandishi anasema:

> Kipwerere alikuwa ni mwanamke wa Kishirazi, mweupe na nywele zake za singa. Nyusi zake nyembamba za upinde zimetulia juu ya macho mawili manene yenye kope laini na ndefu; kwa hivyo kila ukiyatazama utayaona kama yanasinzia.

Maumbile ya mwanamke yanachorwa kuwa ni kivutio kinachopendezesha macho na kuburudisha moyo hasa wa mwanaume. Mwandishi anayaonesha haya kwa sababu katika jamii yetu wanaume wengi wanadhani kuwa mwanamke mweupe na mwenye nywele za singa ndiye mwanamke mzuri na ni kigezo kitumikacho kutafuta mke.

Pia katika *Kosa la Bwana Msa* wasifu wa Jamila unaonesha mwanamke kama pambo kwa mwanamume. Mwandishi anasema:

> Azizi tangu amekuona roho yake yote iko kwako wala hajamiliki nafsi yake… Azizi ni mgonjwa hasa kwa namna nimwonavyo mimi na dawa yake hakuna ila ni wewe …

Hapa mwandishi anaonesha namna anavyoweza kuelezea wasifu wa mhusika katika katika riwaya zake.

Mjawiri (2011) ameandika makala inayoitwa "Muhammed Said Abdulla, Jamii, Maisha Yake na Utajiri wa Kazi Zake." Mojawapo ya mambo aliyoyazungumzia katika makala hiyo ni kwa nini MSA alijikita katika kuandika riwaya za kipelelezi na kukwepa mambo ya msingi kama ya kiuchumi, ukombozi, haki za binadamu na demokrasia. Sababu alizozitoa Mjawiri ni pamoja na kuwa na hadhari ya ulimi wake, kalamu yake na hata vitendo vyake. Kwani, waandishi wa fasihi waliohoji mwenendo na mtizamo wa tabaka tawala katika enzi hizo, waliingia matatani, kwa mfano, Ngugi wa Thiong'o wa Kenya na Wole Soyinka wa Nigeria katika miongo ya awali ya uhuru wa kisiasa. Jambo la pili ni kwamba inawezekana uzoefu na hata elimu yake juu ya masuala mengine ya kijamii haikuwa ya kiwango cha juu. Hivyo, aliona ni bora kuandika mambo ambayo anayafahamu kwa undani kuliko kurukia mambo kijuujuu na hatimaye kufedhehesha sanaa.

Khamis (2011), katika makala yake inayoitwa "Muhamed Said Abdulla: Mwalimu wa Waandishi wa Zanzibar", anamwelezea MSA anavyoweza kutumia lugha kujenga riwaya zake kwa umahiri mkubwa. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale,* ametumia lugha yenye kunata utamu isiyomchosha msomaji, Khamis anasema:

> Katika *Mzimu wa Watu wa Kale* kila neno limewekwa limewekeka, limepangwa limepangika, limesheheni maana na taathira ilivyotakikana. Kila neno limewekwa kusadifu vyema muktadha. Kusadifu maana na ujumi. Kila neno linatumika kuunda sentensi sahili, lakini sentensi sahili isiyo ya kawaida, iliyoshiba upya na mvuto wa kisanaa.

**2.5 Bwana Shigongo na kazi Zake**

Shigongo ni mwandishi chipukizi wa riwaya ya upelelezi ya Kiswahili ukimlinganisha na MSA. Ameanza uandishi wa riwaya miaka ya 2000, riwaya zake zimetokea kupendwa sana na wasomaji hususani wanawake na vijana. Hii ni kwa

sababu zinazungumzia mapenzi, matatizo anayokumbana nayo mwanamke na matatizo mengine mengi yanayojitokeza ndani ya jamii.

### 2.5.1 Wasifu wa Shigongo

Shigongo alizaliwa katika kijiji cha Bupandwamhela Wilayani Sengerema mkoani Mwanza. Kwa sasa anaishi Jijini Dar es Salaam ambapo shughuli yake ni uandishi wa vitabu vya riwaya, hadithi katika mitandao na magazeti mabalimbali. Pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Global Publishers and General Interprises Ltd. (Reuster 2008:25-50)

Wasifu wake kifasihi, Shigongo alianza kazi ya uandishi wa hadithi kwa mara ya kwanza mwaka 1998 kwa kuchapisha hadithi zake kwenye gazeti la *Uwazi*. Shigongo ni miongoni mwa watunzi mahiri wa fasihi pendwa nchini Tanzania. Kwa mujibu wa Madumulla J.S (2009), riwaya pendwa ni riwaya ambayo inajihusisha na masuala ya mapenzi, upelelezi, na ujasusi ambapo kuna mtafaruku mkubwa wa kimwili, au kiakili kati ya mtu mmoja na wengine. Matokeo yake ni kwamba mtu mmoja anaibuka mshindi dhidi ya wengi aliokuwa akipambana nao. Hivyo, Shigongo amekuwa mahiri katika uga wa fasihi pendwa; anaonekana kufuata waandishi wa zamani waliojikita katika riwaya za namna hii, akiwemo Elvis Musiba, Hammie Rajabu na Faraji H.H Katalambula ambao anawaita "*wazee wetu*". Pia ameathiriwa na mwandishi wa Marekani aitwaye Sidney Sheldon. (Reuster 2008)

### 2.5.2 Kazi za Shigongo

Shigongo amekuwa mbobevu na mahiri katika uga wa fasihi pendwa katika uandishi, uchapishaji na usambazaji wa vitabu. Ameandika vitabu vitatu mpaka sasa ambavyo

ni: *The Presedent Loves my Wife (Rais Anampenda Mke Wangu) (*2003*), Damu na Machozi (*2005*),* na *Kifo ni Haki Yangu (*2012*).*

Shigongo amejiwekea utaratibu wa kutoa sehemu ya mapato yake yatokanayo na mauzo ya vitabu na kusaidia makundi maalumu yenye uhitaji ili kujenga uhusiano mzuri na jamii yake. Kwa mfano, katika kitabu cha *Rais Anampenda Mke Wangu*, 5% ya mauzo aliahidi kuwasaidia wajane, pia 5% nyingine ya mauzo aliahidi kusaidia familia zenye watoto wenye matatizo ya Ugonjwa wa kujaa maji kichwani. Halikadhalika, katika kitabu cha *Machozi na Damu*, mtunzi aliahidi kutoa 10% ya mauzo yake kwa ajili ya watoto yatima waliotokana na gonjwa hatari la UKIMWI. Vilevile, katika *Kifo ni Haki Yangu*, 10% ya mauzo hayo ameahidi kuchangia maendeleo ya Shule ya Sekondari Buchosa iliyoko Sengerema Mwanza. (*Tanzania Daima* 30 Januari 2013 na Reuster J. (ameshatajwa)

Shigongo amekuwa akitunga vitabu, hadithi zenye mwendelezo katika magazeti na wavuti. Kwa mfano, hapo nyuma kulikuwa na mtiririko wa hadithi katika magazeti ya *Uwazi, Ijumaa, Ijumaa Wikienda, Risasi, na Amani.* Hivi sasa kuna mwendelezo wa hadithi mbalimbali katika mtandao wa http://www.globalpublisherstz.com. Kupitia mtandao huu hadithi hizo husambazwa ndani na nje ya Tanzania. Baadhi ya hadithi zinazoendelea hivi sasa katika wavuti hiyo ni: *True Memories of My Life (Kumbukumbu za Kweli za Maisha ya Shigongo), Heart Attack (Shambulio la Moyo), Termination of the World (Kuangamia kwa Dunia), Raymond and Stephanie (Raymond na Stephanie), The Rotten Deal (Mpango Ulioharibika), The End of Torture (Mwisho wa Mateso), Queen of the Gorillas (Malkia wa Masokwe)* kwa kuzitaja baadhi.

Kutokana na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, Shigongo anatumia filamu kueneza na kusambazia kazi zake, kwa mfano hadithi ya *From China with True*

*Love (Kutoka China na Penzi la Kweli*), *Rais Anampenda Mke wangu, Damu na Machozi,* na *Kifo ni Haki Yangu.* Hadithi hizo zimerekodiwa katika nyenzo mabalimbali za kisasa kama; CD, VCD, DVD, VHCD (mikanda) na nyenzo nyinginezo zinazoendana na hizo. Mbali na kujiongezea kipato msanii huyu pia anapanua wigo wa wateja wake katika makundi mabalimbali, yaani wasomi na wasio wasomi.

Kupitia historia ya mwandishi, tunaweza kuona kwamba mtindo wa mwandishi huyu umeathiriwa na mazingira na jamii inayomzunguka. Kwa mfano, matumizi ya lugha ya Kiingereza kama upekee wa mwandishi yanathibitisha kwamba jamii ya sasa ina wasomi wengi na mwingiliano mkubwa na mataifa ya nje hususan yanayotumia lugha ya Kiingereza. Uteuzi wa majina ya wahusika katika riwaya zao una uhusiano mkubwa na itikadi zao za dini pamoja na mazingira yaliyowakuza. Pia, utumiaji wa maneno yanayoashiria dhana za kisayansi yanaashiria namna utandawazi ulivyoshamiri kwa sasa.

### 2.5.3 Maandiko Kuhusu Kazi za Shigongo

Reuster (2008), anamwelezea Shigongo kama mwandishi mashuhuri wa riwaya katika magazeti ya kila siku ya wiki kama *Uwazi, Championi, Ijumaa, Amani, Risasi* na *Ijumaa Wikienda* ambayo hulenga watu wa rika zote, yaani vijana, wanaume na wanawake wa matabaka yote. Riwaya hizi huzungumzia mambo yanayojitokeza katika maisha ya kila siku ya binadamu, kwa mfano, upelelezi, mapenzi, uhalifu, ubakaji, athari za madawa ya kulevya, dhuluma, usaliti, n.k.

Pia anaendelea kumwelezea Shigongo kama mwandishi ambaye haandiki kwa ajili ya kuwaburudisha wasomaji wake tu, bali anakusudia kubadili mitizamo ya wasomaji wake. Hasa swala zima la kujitambua na kujiamini. Katika mahojiano yake na Reuster yaliyofanyika tarehe 25 Agosti 2008, anasema:

> Naandika riwaya za kumtia nguvu mtu mweusi. Kumfanya – akisoma mpaka mwisho aamini kwamba kila mtu ana nafasi ya kufanikiwa. Bila kujali rangi yako, bila kujali dini yako, bila kujali kabila. Kila mtu anaweza, akiamua. Kwa hiyo tunaandika riwaya ambazo ukizisoma, ukifika mwisho, utakuwa umejengwa, kwamba "yes, I can do it".

Mawazo haya yamekuwa yakitolewa na watu wengi ambao wanamtetea na kumtia nguvu mtu mweusi. Kwa mfano, rais Barack Obama katika kampeni za uchaguzi wa rais wa Marekani alitumia kauli mbiu ya *"Yes we can!"* (Ndiyo, tunaweza!). Ben Mtobwa katika mahojiano na Milkhail Gromov aliwahi kutoa kauli kama hiyo (*Swahili Forum* 15: 135-140). Japokuwa ameathiriwa sana na kauli za mwenyekiti wa IPP Reginald Mengi, ambaye amekuwa chachu katika kuwahamasisha watu kujitambua na kujiamini kuwa wanaweza kufanikiwa katika maisha.

## 2.6 Mapengo Yaliyojitokeza

Kimsingi kazi za wataalamu hawa zimetoa mwanga mkubwa sana kwa mtafiti, kwani zimemsaidia kuelewa dhana ya mtindo, kuielewa riwaya ya upelelezi na vijenzi vyake pamoja na vipengele vilivyojadiliwa kuhusu mtindo katika riwaya ya upelelezi ya Kiswahili ya waandishi MSA na Shigongo. Hata hivyo kazi zao bado zimeaacha mapengo kadhaa kuhusu kipengele cha tofauti za mtindo katika kazi zao. Mapengo hayo yanajitokeza katika hoja zifuatazo: kwanza, baadhi yao wamezungumzia riwaya ya upelelezi kwa ujumla wake bila kumtofautisha MSA na Shigongo. Wengine wamezungumzia kipengele cha maudhui na kuacha kipengele cha fani ambacho ndicho kinabeba mtindo wa kazi ya fasihi. Pili, kwa walioshughulikia kipengele cha mtindo katika kazi za MSA wametoa mawazo ya jumla tu kuhusiana na vipengele walivyovichambua na hawajafanya ulinganisho kati ya mtindo wa MSA na waandishi wengine. Tatu, hawajafafanua sababu zilizosababisha mwandishi kama MSA atumie mtindo alioutumia katika kuwasilisha

mawazo yake kwa hadhira tofauti na waandishi wengine. Nne, hawajabainisha wazi nani ameathiri mitindo ya waandishi hawa na kwa nini.

Utafiti huu umejaribu kuziba mapengo yaliyodhihirishwa hapo juu kwa kuchunguza tofauti za kimtindo zilizojitokeza katika riwaya ya upelelezi ya Kiswahili, kwa kufanya ulinganisho kati ya MSA na Shigongo. Pia umejadili sababu zilizowasukuma waandishi hawa kutumia mitindo waliyoitumia, bila kusahau athari za waandishi wengine kwa waandishi hawa.

## 2.7 Hitimisho

Baada ya kuangalia machapisho mbalimbali yaliyohusu dhana ya mtindo, riwaya ya upelelezi, wasifu wa MSA na Shigongo pamoja na tahakiki na chambuzi mbalimbali za kazi za MSA na Shigongo, sehemu inayofuata tutaangazia mbinu na vifaa vilivyotumiwa na mtafiti kufanya utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU NA ZANA ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inafafanua mpango wa utafiti, eneo la utafiti, jamii ya watafitiwa, zana na mbinu zilizotumika kukusanyia data, mchakato wa kukusanya data pamoja na uchambuzi wa data.

## 3.1 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Data zilikusanywa kutoka katika kazi mbalimbali zilizoandikwa na MSA na Shigongo pamoja na zile zilizoandikwa na wataalamu mbalimbali kuhusu maisha ya waandishi hawa au kazi zao. Utafiti ulifanywa kwa kutumia mbinu ya ufafanuzi iliyoangalia thamani ya matini iliyopatikana katika riwaya. Data mbalimbali zilizokusanywa zimehakikiwa, kuchambuliwa, na kufafanuliwa kwa kina ili kutoa majibu ya maswali ya utafiti kutimiza malengo ya utafiti huu.

## 3.2 Ukusanyaji wa Data

Data ni mali ghafi ya utafiti kama ilivyo lugha kwa mwanafasihi. Licha ya kuongozwa na nadharia ya elimumtindo, data zilihitajika kukusanywa ili nadharia iweze kutumika kutimiza lengo la utafiti. Ni katika msingi huo mbinu ya kujisomea mwenyewe ilitumika kukusanya data, kwa sababu utafiti uliofanyika ni utafiti wa maktabani. Data zilipatikana kwa kusoma vitabu teule vya riwaya ya upelelezi ya Kiswahili na kisha kuzichunguza ili kubaini tofauti za kimtindo zilizojitokeza katika riwaya hizo. Mbinu ya kujisomea ilituwezesha pia kusoma makala, majarida, wavuti

na vitabu vilivyotupa mwanga wa kuelezea tofauti za kimtindo katika riwaya ya upelelezi ya Kiswahili kati ya waandishi MSA na Shigongo.

Data zilizokusanywa na kutumika katika utafiti huu ni data za msingi na data za upili. Data za msingi ni data zilizokusanywa na mtafiti mwenyewe kutoka maktabani kwa lengo au madhumuni ya kujibu maswali ya utafiti. Data hizi ni taarifa ambazo ni mpya na za awali katika tarehe ya kuchapishwa (Jamal: 2008).

Data za msingi katika tasnifu hii zilipatikana kwa kusoma na kuchambua vitabu teule vya riwaya ya upelelezi ya Kiswahili vya MSA na Shigongo ili kubainisha tofauti za kimtindo katika riwaya hizo.

Kuhusu data za upili, Jamal (uk: 14) anaeleza kuwa ni data zilizokusanywa na watu wengine na kwa madhumuni mengine na katika vyanzo vya kifasihi. Huwa zimetokana na humilikiwa na mtu mwingine na si za mwandishi wa sasa. Hutokana na majarida au nyaraka zingine. Maandiko na machapisho mbalimbali kutoka kwa wataalam na wachambuzi wa kazi za fasihi zihusuzo riwaya ya upelelezi na kwa jumla, yalisomwa na kutupatia data za upili. Pia matini mbalimbali zinazohusu taaluma ya elimumtindo zilitumika katika kuchunguza na kueleza ulinganisho wa mtindo katika riwaya ya upelelezi ya Kiswahili.

## 3.3 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti huu wamegawanyika katika makundi mawili. Kwanza, tumeitazama jamii ya watafitiwa katika ujumla wake na pili, tumebainisha sampuli tuliyoshughulika nayo.

### 3.3.1 Jamii ya Watafitiwa

Jamii iliyolengwa ni riwaya mbalimbali za MSA na Shigongo. Hizi zimesaidia kubainisha mitindo waliyotumia waandishi hawa, hususani matumizi ya lugha katika

kuumba wahusika, mandhari, mtiririko wa matukio na dhamira katika kazi zao. Mtafiti aliamua kutumia riwaya kwa sababu aliamini kuwa utanzu huo wa fasihi humpa uhuru mtunzi kufafanua kusudio lake kwa kutumia lugha ya mjazo na mbinu nyingi za kisanaa.

### 3.3.2 Sampuli ya Kazi Tafitiwa

Riwaya ya upelelezi ya Kiswahili imesheheni vitabu vingi, hivyo ilimlazimu mtafiti kuchagua vitabu vichache vilivyowakilisha vingine kwa kila mwandishi ili kufanya ulinganisho wa kimtindo. Hii ilitupelekea katika uchaguzi wa sampuli. Sampuli ni sehemu ya idadi ya vitu. Idadi ya vitu ni jumla ya vitu vyote vinavyochunguzwa (Jamal 2008:19). Idadi ya vitu vyote vinavyochunguzwa katika utafiti huu ni vitabu vyote vya riwaya ya upelelezi ya Kiswahili na sampuli ni riwaya teule za MSA na Shigongo.

Ili kupata riwaya teule, uchaguaji wa sampuli ulitumia sampuli lengwa. Hii ni aina ya sampuli ambapo inapanga kazi tafitiwa kulingana na vigezo vilivyochaguliwa vinavyoendana na maswali ya utafiti. Kiasi cha sampuli ambacho kinaweza kuwekwa au kutowekwa kabla ya ukusanyaji data, hutegemea vitendea kazi na muda uliopo, pamoja na malengo ya utafiti. Kiasi cha sampuli lengwa huwekwa kufuatana na nadharia. Husaidia kukusanya data na wakati huo huo kuzipitia na kuzichambua. Sampuli lengwa hutumika kuchagua kazi tafitiwa zinazounda sampuli kulingana na vigezo vilivyochaguliwa. Hutumika pale ambapo kazi fulani huwa ni lengwa zaidi ya nyingine.

Kupitia sampuli lengwa riwaya mbili za upelelezi za MSA: *Mzimu wa Watu wa Kale* na *Kosa la Bwana Msa* zilichaguliwa. Pia riwaya mbili za Shigongo: *Kifo ni Haki Yangu* na *Damu na Machozi* zilichaguliwa kukamilisha sampuli ya utafiti.

Sababu ya kuchaguliwa kwa waandishi hao ni ile ya kihistoria, kwani MSA ni mwandishi pekee wa awali wa riwaya ya upelelezi ya Kiswahili na Shigongo ni mwandishi wa riwaya ya upelelezi ya Kiswahili kwa wakati huu tulionao. Wameandika kazi zao katika mazingira na wakati tofauti, pia kazi zao zimesomwa na wasomaji wengi nchini Tanzania. Utunzi na ubunifu huweza kutofautiana au kushabihiana kutokana na watunzi, wakati, mazingira na mabadiliko ya kijamii.

Utafiti ulijikita kuchunguza vitabu vya waandishi hao, kwani viliweza kuwakilisha sampuli kubwa ya riwaya ya upelelezi ya Kiswahili kwa sababu ya kuwepo kwa tofauti za kimtindo katika uandishi wa kazi zao.

### 3.4 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika katika maeneo ya Mwanza, Dodoma, na Dar es Salaam. Miji yote imehusika kikamilifu katika ukusanyaji wa data za kimaktaba. Uteuzi wa maeneo hayo ya kijiografia ulitokana na sababu zifuatazo: Mwanza – urahisi wa kufikika. Hii ni kutokana na ukweli kuwa eneo hili ndiyo makazi ya mtafiti. Hapa alitembelea maktaba ya mkoa na Chuo Kikuu cha Mt. Augustino. Dar es Salaam na Dodoma – Upatikanaji wa vyanzo mbalimbali vya kimaktaba kama vile ripoti za tasnifu na vitabu kuhusu MSA na Shigongo na maandiko yao. Maeneo yaliyolengwa ni pamoja na; makavazi ya Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

### 3.5 Zana na Njia za Kukusanyia Data

Zana zilizotumika kukusanyia data katika utafiti huu ni kalamu, penseli, karatasi, kompyuta, vinyonyeo pamoja na mwongozo wa kusoma tasnifu, majarida na vitabu ambavyo ni vyanzo mbalimbali vya data. Zana hizi ziliteuliwa kutumika katika utafiti huu kutokana na asili na kiini cha utafiti huu.

Karatasi, kalamu na penseli zilitumika kwa ajili ya kunukuu data zilizopatikana kutoka katika tasnifu na vitabu mbalimbali, kwa ajili ya kutumika wakati wa uchambuzi na uunganishaji wa data. Data hizo ni zile za msingi na upili. Kompyuta na kinyonyeo zilitumika kwa ajili ya kuchapia kazi na kuhifadhi kumbukumbu. Vitabu na makala vilikuwa mahsusi kwa ajili ya kuvisoma na kukusanya data mbalimbali za msingi na za upili zilizosaidia kuelezea tofauti za kimtindo katika riwaya ya upelelezi ya Kiswahili kati ya MSA na Shigongo.

### 3.6 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhibiti Wake

Mtafiti aliomba ruhusa katika mamlaka zilizohusika ili aruhusiwe kukusanya data za kimaktaba katika maeneo na taasisi zao.

Data za maktabani zilikusanywa kwa kutumia mwongozo wa usomaji ulioandaliwa. Mwongozo huo uliwasaidia watafiti wakati wa kusoma tasnifu, vitabu majarida na vielelezo mbalimbali ili kupata data zinazohusiana na utafiti huu.

#### 3.6.1 Uchakataji na Uunganishaji wa Data

Uchakataji wa data ni ukokotoaji na upimaji wa data kwa kutafuta uhusiano wa ruwaza uliopo kati ya makundi ya data (Kothari 2004:186). Kufanya hivyo kunasaidia kujua kama yaliyoonekana yanathibitisha au kupima nadharia tete. Uchakataji data ni msingi wa kujibu maswali ya utafiti.

Uchakataji wa data ulitumia mkabala usio wa kiidadi katika kueleza ulinganisho wa mtindo katika riwaya ya upelelezi ya Kiswahili. Mkabala huu hutumia uchambuzi wa data kwa njia ya maelezo na kuhusisha sehemu tatu; yaani kutambua, kukusanya na kufikiri. Mchakato unaonesha kuwa mtafiti hatambui, hakusanyi, hafikiri na kuandika ripoti tu, bali mchakato huo una hali ya kujirudia rudia na ni endelevu.

Seidel (1998) anaufafanua mchakato huo kama ifuatavyo: kutambua vitu. Mtafiti anatakiwa kufahamu vitu anavyotakiwa kuvitambua na jinsi ya kuvitambua. Anaendelea kueleza kuwa kuna hatua mbili za kutambua vitu. Kwanza ni kwa kuangalia, kuandika maelezo, kurekodi mahojiano, na kuweka data pamoja. Ukifanya hivyo, unatengeneza rekodi ya vitu ulivyovitambua kisha unaitilia mkazo na kutambua vitu vinavyotakiwa. Unafanya hivyo kwa kusoma au kusikiliza rekodi yako mara nyingi. Ukishatambua vitu husika, kinachofuata ni kukusanya. Kuhusu kufikiri kinachofanyika ni kuangalia ukaribu wa uliyoyakusanya. Lengo ni kuangalia hisia, ruwaza, uhusiano wa data ndani na nje ya data zilizokusanywa na kufanya ugunduzi wa jumla kuhusu tukio unalotafiti.

Baada ya kusoma vitabu teule vya riwaya ya upelelezi ya Kiswahili vya MSA na Shigongo na kukusanya data, tumechambua data hizo kwa kueleza ili kubainisha tofauti za kimtindo katika riwaya ya upelelezi ya Kiswahili.

## 3.7 Changamoto za Utafiti

Mambo yafuatayo ni changamoto kwa mtafiti katika kuyafikia malengo yake. Kwanza, uhaba wa fedha za kugharimikia shughuli mbalimbali kwa mfano, safari za mtafiti kufuata ushauri kwa msimamizi, ukusanyaji wa data, uchambuzi wa data pamoja na uunganishaji na uandishi wa ripoti. Pili, ugumu wa upatikanaji wa vitabu na majarida yanayohusu kazi za MSA na Shigongo.

## 3.8 Hitimisho

Sura hii imezungumzia mpango wa utafiti, ukusanyaji wa data, walengwa wa utafiti ambao wamejumuisha jamii ya watafitiwa na sampuli ya watafitiwa. Pia eneo la utafiti, zana na njia za kukusanyia data zimebainishwa. Mchakato wa ukusanyaji wa

data na udhibiti wake pamoja na changamoto za utafiti zimefafanuliwa. Sura inayofuata itazungumzia uwasilishaji wa data na uchambuzi wake.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii data zilizokusanywa zimewasilishwa, kuchambuliwa na kujadiliwa kulingana na malengo ya utafiti. Uwasilishaji wa data umefanywa kwa kutumia mbinu ya ufafanuzi kulingana na malengo mahususi ya utafiti. Data za msingi kutoka katika sampuli yetu ya riwaya ya upelelezi ya Kiswahili zilitumika kueleza tofauti za kimtindo. Katika kufanya hivyo data za upili kutoka katika maandiko na machapisho mbalimbali yanayohusiana na taaluma ya mtindo na riwaya ya upelelezi zimesaidia kwa kiwango kikubwa.

Mjadala umegawanyika katika sehemu tatu zinazoakisi malengo na maswali ya utafiti huu. Katika sehemu ya kwanza mawazo ya jumla katika riwaya teule za *Mzimu wa Watu wa Kale, Kosa la Bwana Msa, Kifo ni Haki Yangu na Damu na Machozi* yametolewa. Sehemu ya pili imejadili kwa kina matumizi ya lugha, uumbaji wa wahusika, mtiririko wa matukio, mandhari na dhamira katika kazi teule za MSA na Shigongo. Pia tofauti za kimtindo zilizojitokeza kati ya riwaya za MSA na Shigongo na sababu zilizochangia waandishi hawa kutumia mtindo tofauti katika kuumba fani katika riwaya zao zimefafanuliwa. Baadhi ya athari za waandishi wengine kwa waandishi hawa zimebainishwa pia. Sehemu ya mwisho ni muhtasari wa yaliyojadiliwa katika sura hii.

## 4.1 Kazi Teule za MSA

MSA ni mwandishi mahiri wa riwaya ya upelelezi ya Kiswahili. Madumlla (2009) anamwelezea MSA kama baba wa riwaya pendwa kwa sababu ndiye mwanzilishi katika uandishi wa riwaya ya upelelezi ya Kiswahili. Katika riwaya zake zikiwemo

*Mzimu wa Watu wa Kale* na *Kosa la Bwana Msa* anazungumzia mambo mbalimbali yanayojitokeza kila siku katika jamii ya Waswahili.

### 4.1.1 Mzimu wa Watu wa Kale: Mawazo ya Jumla

*Mzimu wa Watu wa Kale* ni riwaya inayojadili maswala mbalimbali ya maisha katika nyanja za kiuchumi, kijamii, na kiutamaduni. Katika riwaya hii, mwandishi amewachora wahusika wake kwa namna ambayo wanaishi katika uhalisia. Hivyo riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* imejengwa katika misingi ya kiyakinifu. Jina la riwaya, *Mzimu wa Watu wa kale* linaonesha sura ya pahala au mazingira ya kiitikadi. Dhamira kuu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ni upelelezi wa kifo cha Bwana Ali Bomani. Kifo chake kinasababisha utata mkubwa juu ya nani ni muuaji. Kisa kinaonekana kuwa changamano hasa kwa sababu kinahitaji majibu kuhusu kwa nini kauliwa, wapi, wakati gani, na pahala gani kiwiliwili chake kimefichwa. Je, kichaka au mahali kiwiliwili cha Bwana Ali kilipofichwa, panasadifu sifa za mzimu unaozungumziwa? Na kwa nini paitwe mzimu wa watu wa kale?

Bwana Msa anafanikiwa kumtambua muuaji na kisa cha kifo cha Bwana Ali. Uwezo wa Bwana Msa wa kuunganisha matukio kwa kutumia falsafa yake ya ukweli kinzani ya Kinyume cha mambo ndio uliomsaidia kujua ukweli wa tukio zima la mauaji. Falsafa hii ya kinyume cha mambo inathibitishwa na mawazo ya Najum katika ukurasa wa 3 ambapo mwandishi anasema:

> Najum alikiri kwamba, elimu kama ile aliyonayo Bwana Msa hakosi aliipata katika kile kitabu chake kiitwacho *Kinyume cha Mambo*, kisichomtoka mfukoni na anachokisoma popote anapopata nafasi……

Mwandishi amebainisha wazi kuwa Bwana Ali kauawa kwa sababu ya dhuluma, na mahala panapoitwa mzimu ni mahala walipofia wageni saba kwa pamoja, na ambapo

baadaye watu wakapajengea hofu ambayo waliishika na kuisadiki miaka nenda rudi katika maisha yao.

Mwandishi, katika *Mzimu wa Watu wa kale*, ameweza kuelezea utamaduni wa Wazanzibar na utamaduni wa jamii ya Waswahili kwa jumla. Anaonesha maana ya yale yatendekayo katika jamii hizi na namna yanavyotendeka katika maisha ya kila siku ya Wazanzibar. Mwandishi anazungumzia mawazo ya kifalsafa ambayo yanafungamana na utamaduni wa jamii anayoizungumzia. Kwa mfano, mapenzi na ndoa, uaminifu, uongozi, malezi na makuzi, imani na itikadi za kijadi, dini, urafiki, lugha, maisha na kifo, pia uzalendo.

Falsafa ya kinyume cha mambo imetumika kuonesha kwamba maisha au mambo sivyo yalivyo kama tunavyoyaona juujuu. Katika kushadidia falsafa yake, mwandishi anatumia misemo kama: "Shibe kamwamini njaa, na kwa hivyo kampa chakula amwekee – lakini njaa alipomwona shibe kaondoka alikiangamiza chakula chote tumboni mwake" *(uk 2)*. Dhana ya kinyume cha mambo imeoneshwa pia kupitia watu wenye uwezo wanavyoshindwa kutumia vizuri uwezo wao na mwisho kuishia katika aibu na mateso. Kwa mfano, Bwana Ali ni mtu mwenye uwezo wa mali na fedha, lakini ni bahili anasema:

> Lakini alivyokuwa yeye ni mtu bahili sana hakuweza kujilisha kwa namna tumbo lake linavyohitaji" (uk 6). Pia (uk 7) anasema hakuona vibaya, mbele yao wenyewe – alifoka na kumlaumu mwanawe kwa nini akaja na wageni, tena wawili angalau si mmoja … Ati anasema atanikata urithi au atauza mali yake yote.

Tunapoiangalia jamii yetu katika mtazamo huu wa kinyume cha mambo, tutaona kuwa ndiyo hali halisi inayoitawala jamii kwa wakati huu tulionao. Yaani, falsafa hii potofu ndiyo inayoonekana mwafaka kwa maisha ya sasa. Kwani watu wengi

wamegeuza mambo maovu kuwa mazuri na kitu cha kawaida katika maisha yao ya kila siku.

Kuhusu suala la malezi MSA anaonesha wazi jamii ya zama zilizopita ilivyolipa umuhimu suala la malezi ya watoto. Kwa kumtumia mhusika Bwana Ali na mkewe Kipwerere, ameonesha namna walivyomlea Ahmed kama mtoto wao japo anataka kumkata urithi na kuuza mali yake yote. Hii ni kwa sababu jamii ya zamani ilithamini utu wa mtu, tofauti na ilivyo sasa.

MSA kwa upande mwingine, anaamini katika mizimu na uganga. Hapa, mwandishi anataka kutuonesha namna jamii ya zamani ilivyothamini miungu na uganga. Anaonesha namna Waafrika walivyoienzi falsafa yao. Kwani kabla ya majilio ya wakoloni na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia Waafrika walitambikia mizimu pindi wapatapo shida mbalimbali. Mwandishi anashadidia hili anaposema:

> Mambo yalipokithiri, wazee wake walifika kwa waganga kutazamia, nao kila mmoja alisema lake. Wengine walisema kuwa amerogwa na wachumba waliokuwa wakimtaka wakamkosa. Wengine walisema kuwa amedhurika katika kile kichaka cha ‘Mzimu wa Watu wa Kale’ … (uk: 10).

Nukuu hii inaonesha ni kwa namna gani Waafrika walienzi falsafa yao, hususani kufanya matambiko kwa miungu na mizimu yao.

Kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii, MSA anamchora mwanamke kama pambo kwa wanaume, anayetegemea kuolewa ili kuendesha maisha na asiye na sauti kwa mumewe. Kwa mfano, Kipwerere pamoja na tatizo alilokuwa nalo alisubiri ruhusa ya mumewe kupewa ng’ombe kwa ajili ya matibabu. Mwandishi anasema:

> Na kwa hiyo, kila dhofu lihali likizidi kumkondesha Kipwerere, wazee wake humshika mumewe Bwana Ali, atoe ng’ombe mmoja ili apewe chano mtoto wao, apate kupumzika lakini Bwana Ali huzidi kuwapa ahadi za mbele tu, mwaka baada ya mwaka, mpaka leo (uk: 10).

Kwa jumla riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* inajadili maisha ya kila siku ya Wazanzibar na Waswahili kwa ujumla. Pia inaonesha matabaka yaliyokuwepo kabla ya uhuru na hata mara tu baada ya uhuru. Kwamba waliomiliki njia kuu za uchumi walikuwa ni wageni hasa Wahindi na Waarabu. Waafrika walikuwa ni waajiriwa tena wanaolipwa ujira mdogo tofauti na wageni. Kwa mfano, boi wa Baniani, Inspekta Sefu, Kurwa na Masanja wanawakilisha tabaka la Waafrika walioajiriwa kwa ujira mdogo.

### 4.1.2 Kosa la Bwana Msa: Mawazo ya Jumla

Kama ilivyo katika *Mzimu wa Watu wa Kale*, MSA katika *Kosa la Bwana Msa* anazungumzia maisha katika Nyanja za kisiasa, kijamii, kiuchumi na kitamaduni. Anaonesha maisha ya mwanadamu katika uhalisia wake, hapa anatuonesha namna ndoa za siri zinavyotawala maisha yetu ya kila siku. Hali hii inajitokeza hadi katika dini za waliojiwekea mipaka ya mke mmoja na mume mmoja. Maelezo ya mwandishi katika *Kosa la Bwana Msa* yanaonesha uwepo wa ndoa za siri, anasema:

> Bibiye, nikwambie nini … "Nimemwona kwa macho yangu haya, kesho nitatiwa pamba, Bwana Mdogo aliteremka katika gari lake mbele ya nyumba moja yenye bustani mbele yake, kijumba kizuri hicho chenye mkato wa kisasa na mbele yake bustani yenye miwaridi na miasumini … mtoto, kinda, mzuri wa kuteua, anayeweza kukaa pamoja na wanawake alfu … (asionekane) … ila yeye tu. Mtaratibu wa namna yake (uk 3).
> Baadala ya kuaminika, Tunu alionekana mzushi …. "Haiwezekani kuwa … unajifundisha kuzuwa … Vipi Ahmed aniache mimi hapa aende akakae na kadimu, kidiku huko shamba … (uk 4).

Katika *Kosa la Bwana Msa*, mwandishi ametumia mbinu ya kinyume cha mambo kuwakumbusha wanadamu kwamba dunia ina miujiza, yaani haiendi kama tunavyoitarajia iende kila siku. Kwa mfano, anaposema: "Kihunzi kimefanya mapinduzi – maiti anatembea, sijui wahai hawaonekani, anaonekana maiti tu (uk

104)". Kauli hii ni kinyume cha mambo kwa sababu kwa kawaida mwenye uwezo wa kufanya mapinduzi ni binadamu tena aliyejitayarisha kikamilifu. Isitoshe, kihunzi si kitu chenye uhai kwa hiyo hakiwezi kufanya mapinduzi. Pia ni miujiza katika dunia hii tuliyomo maiti kutembea. Dhana hii bila shaka inafafanua kitu cha ndani zaidi ambacho kwa hakika hakionekani, lakini kinatokea.

Motifu ya safari imetumiwa na mwandishi kuonesha kuwa maisha ya mwanadamu ni safari ndefu yenye kutawaliwa na vikwazo, mitihani ya ghilba na vionjo vya misiba ambayo huishia kifo kisicho na ubaguzi. Mwandishi anatuonesha kuwa usawa wa binadamu upo kwenye kifo peke yake, kwani kifo hakijali fahari na uwezo alionao binadamu kifedha. Kwa mfano, katika *Kosa la Bwana Msa* mwandishi anamtumia mhusika Bi Shinuna ambaye alifikiri pesa na mali ni kila kitu katika maisha ya binadamu na mwisho anaishia kufa katika ajali katika harakati za kutaka kumuua mumewe. Pia mwandishi anamtumia mhusika Seyyid Ahmed bin Soud kutuonesha jinsi maisha yanavyopanda na kushuka. Seyyid Ahmed alikuwa na uwezo wa mali na kifedha lakini maisha yalimgeukia akawa dhalili hata kufikia kulazwa hospitali ya wendawazimu na kuishia kuwa mtu wa chini anayehitaji msaada.

Aidha, mwandishi anaikumbusha jamii kuwa ubaya haulipi siku zote na mwisho wake huwa ni mbaya. Anamtumia mhusika Bi Shinuna, mke wa Seyyid Ahmed anayepanga mipango ya kumuua mumewe na hafanikiwi badala yake anakufa yeye mwenyewe. Mwandishi anasema:

> Hatujawahi kuisikia kesi ya maharamia wawili waliotaka kumuua Seyyid Ahmed bin Soud huko maili tatu bado kufika Chwaka, jana ilipita ajali kubwa ya gari la Bi Shinuna, mke wa Seyyid Ahmed bin Soud, mahali pale pale alipotaka kuuliwa mumewe, katika ajali hiyo Bi Shinuna, Tunu, mtumishi wake na Shwuwari, dereva wa gari hilo, wote wamepotea,… (uk: 114).

Dondoo hii inaonesha ni kwa namna gani wale walioshiriki kufanya ubaya walivyoishia pabaya. Majambazi waliokodiwa na Bi Shinuna wamekamatwa na polisi. Tunu na Bi Shinuna wote wamekufa katika ajali.

Mwandishi pia anaionesha jamii kwamba mtenda mema hulipwa kwa wema au haki ya mtu haipotei bure bali inaweza kucheleweshwa tu. Anawatumia wahusika Jamila na Seyyid Ahmed waliooana huku Seyyid Ahmed akitumia jina la Bwana Ali Soud hivyo Bwana Msa kudai kuwa hiyo si ndoa halali. Pamoja na Jamila kuolewa na Bwana Azizi (mume wa pili) na kuzaa nae mtoto, mwishoni wanarudiana na mumewe wa kwanza baada ya mume wa pili kufariki, kisha kuombana msamaha na Seyyid Ahmed.

Kimsingi riwaya ya *Kosa la Bwana Msa* inajadili maisha ya kila siku ya binadamu katika jamii zetu tunamoishi. Suala la ndoa za siri linatawala maisha ya binadamu wa sasa katika jamii na si kwa watu wa kawaida tu bali hata kwa wale wanaojiita viongozi wa dini wanadiriki kuoa kwa siri. Pia, suala la kufanyiana ubaya kati ya mume na mke ni jambo ambalo linajitokeza mara kwa mara. Aidha, mume kumdhuru mkewe au mke kumdhuru mume limekuwa ni jambo la kawaida kwa maisha ya sasa.

### 4.1.3 Matumizi ya Lugha Katika kazi za MSA

Katika utafiti huu, suala la mtindo tumelishughulikia tukiwa na maana ya ubunifu na uvumbuzi katika lugha. Namna anavyopangilia maneno, uteuzi wa maneno, mtiririko wa matukio, matumizi ya tamathali za usemi, namna anavyotumia lugha kuchora wahusika wake, kubainisha dhamira na mandhari.

#### 4.1.3.1 Uteuzi wa Msamiati

MSA ni mahiri katika kuteua msamiati katika uandishi wa riwaya zake. Mara zote huteua msamiati ambao haujazoeleka katika matumizi ya watu ya kila siku, hii

husababisha baadhi ya wasomaji wa kazi zake kuona riwaya zake ni ngumu kuzielewa. Huu umekuwa ni mtindo pekee katika uandishi wa riwaya ya upelelezi unaomfanya aonekane yuko tofauti na waandishi wengine wa riwaya ya upelelezi ya Kiswahili.

Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale,* kwa mfano, mwandishi ametumia maneno au msamiati mwingi ambao haujazoeleka katika matumizi ya kila siku. Mwandishi anaposema:

> Bwana Msa – naye ndiye aliyekuwa wa tatu wao – aliyefuata rubaa, ingawa yeye hasomi tena skuli, alikuwa akikaa kitako kizingitini kwa kuingilia ndani, anasoma kitabu chake, *Kinyume cha Mambo* (uk: 8).

Neno *rubaa* kwa namna lilivyotumiwa na mwandishi si rahisi kueleweka kwa msomaji wa kawaida kwa sababu ni neno gumu, halijazoeleka katika matumizi ya kila siku. Msomaji mwingine angeweza kufikiri ni jina la mtu wakati lina maanisha hali ya watu kuwa pamoja au kufuatana.

Pia mwandishi anaposema:

> …Katika kifurushi kilichokuwa karibu yake alitoa pachori**,** pakanga, udi na ubani wa makaburini**,** kusi na mea; alipokwisha vitia vyote pamoja katika moto… (uk: 11-12).

Maneno; *pachori, pakanga, kusi* na *mea* pia hayajazoeleka katika matumizi ya kila siku, hivyo ni msamiati mgumu kwa msomaji. Mwandishi ametumia neno *pachori* na *pakanga* akimaanisha aina ya mimea, yenye majani yanayotoa harufu nzuri, yanatumika kwa mafusho. *Kusi* ni mzizi wa mmea fulani, unaotumiwa kwa mafusho. *Mea* ni aina ya gundi laini inayonukia, hutumika kufukizia.

Aidha, mwandishi ametumia maneno, *viburuji* na *visugodi* anaposema:

> Stesheni yenyewe kilikuwa kibanda cha matofali ya saruji, kimejengwa juu ya *viburuji* vinne.
> Katika yaliyozidisha pambo la stesheni yetu, mlangoni, kwa roshani, askari wawili wamekaa juu ya bao

> lililowekwa pembeni pa mlango wa kuingilia ndani – mmoja wao katika wao anasinzia, yu hoi kwa usingizi, na wa pili, yumo kumpiga mwenziwe kwa *visugodi* vya mkono kila mara anaposinzia na kuanguka juu yake (uk: 49).

Maneno *viburuji* na *visugodi* ni msamiati mgumu, si rahisi kwa msomaji kuelewa mara moja anaposoma riwaya hii. Mwandishi kwa neno *viburuji* alimaanisha mapengo yaliyochongwa juu ya ukuta wa ngome au boma, wakati *visugodi* alimaanisha vifundo vya mikono vinavyokuja kwa kuikunja mikono katikati baina ya makwapa na viganja. Yapo pia maneno kama muwele (mgonjwa) uk.11, sijahi (kelele) uk.12, mnoga (tumbaku) uk.33 na wastiri (wanunuzi) uk.51.

Hayo ni baadhi ya maneno kati ya mengi ambayo ameyatumia mwandishi katika kuwasilisha ujumbe alioukusudia uwafikie wasomaji wake. Maneno ambayo kimsingi ni magumu kwani hayajazoeleka katika matumizi ya kila siku.

Kwa upande wa riwaya ya *Kosa la Bwana Msa,* MSA ametumia pia msamiati mgumu ambao haujazoeleka katika matumizi ya kila siku kwa kiasi kikubwa. Baadhi ya maneno magumu yaliyotumiwa na mwandishi ni pamoja na *ghamu*, *dahiliya*, *marish-marish*, *ajinabi* na *isimu* kwa kuyataja machache. Mwandishi anaeleza kwamba Jamila kasoma katika skuli ya *Dahiliya* iliyokuwapo hapo Forodhani, mjini (uk: 17).

> … Niwie radhi, Shekhe, basi jambo hili ndilo la kunipigia simu mimi nije upesi *marish-marish* baada ya kuweka simu chini tu? (uk: 19).
> Jamila alisita kidogo, Vipi mimi namfuata mtu huyu *ajinabi*, simjui mwanzo wala mwisho (uk:24).
> Jamila ni *isimu* ya uzuri (uk:38).
> Baada ya nusu saa aliyoipitisha katika hamu na *ghamu*… (uk: 95).

Mwandishi ametumia neno *marish-marish* kwa maana ya haraka haraka, Dahiliya kwa maana ya shule ya bweni, *ajinabi* kama mgeni au mtu usiyefahamiana naye, *isimu* kama jina na *ghamu* kama majonzi. Msamiati huu mgumu ni kati ya baadhi ya

maneno ambayo hayajazoeleka kutumiwa katika matumizi ya kila siku, na hivyo kumfanya msomaji aone kazi za riwaya za MSA ni ngumu kueleweka.

Kimsingi MSA katika riwaya zake zote, uteuzi wake wa msamiati ni tofauti na waandishi wengine wa riwaya ya upelelezi ya Kiswahili kwa sababu hutumia maneno magumu ambayo hayajazoeleka katika utumizi wa lugha wa kila siku.

**4.1.3.2 Matumizi ya Sinonimu**

Kwa maana finyu sinonimu ni maneno au vifungu vya maneno vyenye maana sawa; hata hivyo katika maana pana sinonimu ni maneno ambayo maana yake inapishana au kuingiliana katika miktadha fulani na kutengana katika miktadha fulani. Katika riwaya za MSA sinonimu zinatumika kwa maana hii. Riwaya hizi zimeandikwa kwa mtindo wa uandishi ambapo neno moja au fungu la maneno aghalabu hutumiwa pamoja na sinonimu zake katika ufafanuzi wa jambo. Aghalabu sinonimu hizo zinatumiwa katika sentensi moja au aya moja. Sinonimu zinapotumiwa pamoja, zinaunganishwa kwa matumizi ya ‘na’, ‘au’ na ‘wala’. Matumizi ya sinonimu ni sifa moja bainifu ya kazi za MSA. Kwa mfano, katika riwaya zake ametumia mifano ya sinonimu zifuatazo:

| **Neno** | **Sinonimu** | |
|---|---|---|
| **Ukurasa** | | |
| Kustua | Kuroga | 4 |
| Kuzindua | Kuzingua | 4 |
| Pachori | Pakanga | 11 |
| (*Mzimu wa Watu wa Kale*) | | |
| Kidimu | Kidiku | 11 |
| Haraka | Wahaka | 43 |
| Bwana | Mume | 53 |

| | | |
|---|---|---|
| Bibi | Mke | 53 |
| (*Kosa la Bwana Msa*) | | |

Mwandishi ametumia sinonimu hizi kuonesha dhana zinazokaribiana katika miktadha tofauti ili kufafanua jambo alilolikusudia.

#### 4.1.3.3 Matumizi ya Antonimu

Matumizi ya maneno na vinyume vyake yana uwezo mkubwa wa kulifafanua jambo ili liweze kueleweka vizuri zaidi. Hii ni kwa kuwa maana ya neno moja haieleweki vizuri bila ya kuzingatia maana za maneno mengine. Ukweli ni kwamba uwili – kinzani ni mojawapo ya kanuni zinazotawala miundo ya lugha. Hii inaashiria kuwa maisha ya binadamu hujaribu kuuelewa ulimwengu anamoishi kwa kutenganisha ukweli wa mazingira yake kwa kutumia uwili-kinzani. Katika riwaya za MSA matumizi ya antonimu au kinyume yanadhihirika kama ifuatavyo:

| **Neno** | **Antonimu** | **Ukurasa** |
|---|---|---|
| Mwangaza | Kizani | 3 |
| Kustua | Kuzindua | 4 |
| Kuroga | Kuzingua | 4 |
| Njaa | Shibe | 5 |
| (*Mzimu wa Watu wa Kale*) | | |
| Wahai | Maiti | 104 |
| (*Kosa la Bwana Msa*) | | |

Mwandishi ametumia maneno yenye kinyume katika kufafanua dhana mbalimmbali alizokusudia katika riwaya zake.

#### 4.1.3.4 Matumizi ya Tamathari za Semi

Tamathari za semi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti au zinazofanana au ni usemi wenye kupanua, kupuuza au

kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalum iliyokusudiwa na mtunzi au mzungumzaji (Senkoro 1982; Mulokozi na Kahigi 1979:32; Gibbe 1980; Msokile 1992 na Omari 2010:2). Tamathali nzuri huyakinisha na kuipa uhai halisi zaidi dhana inayoelezwa. Aidha, huburudisha na kuzindua akili ya msomaji na kuacha athari ya kudumu katika hisia na mawazo yake. Zipo tamathali nyingi zinazotumiwa na waandishi wa kazi za fasihi kama vile; tafsida, sitiari, tashbiha, tashihisi, lakabu, mbaalagha, dhihaka, taswira, majazi, taniaba na tabaini kwa kuzitaja baadhi. Katika utafiti huu tunashughulikia tamathali zifuatazo: tabaini, tashibiha, Sitiari, tashihisi, uteuzi wa visawe, lugha ya mtaani, kuchangaya lugha. Tamathali hizi zimeteuliwa kwa sababu zimejitokeza kwa kiasi kikubwa katika riwaya za MSA ambaye ni mwandishi wa riwaya ya upelelezi ya awali katika fasihi ya Kiswahili.

#### 4.1.3.4.1 Tabaini

Tabaini ni tamathali ya usemi ambayo kwayo mawazo yanakinzana sana. Hutumiwa katika sentensi ili kuleta msisitizo wa mawazo yatolewayo. (Senkoro 1982; Khatibu 1999: 76; Wamitila 2003: 209; TUKI 2004: 389). Tabaini hutambulishwa kwa kuwepo na mawazo yanayokinzana. Pia hutumika katika kuremba lugha.

MSA katika uandishi wa riwaya zake ametumia mbinu hii ya tabaini kuonesha msisitizo katika jambo analolizungumzia. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, mwandishi ametumia maneno *kustua* na *kuroga* yenye maana ya kumfanyia mtu uharibifu au jambo ambalo sio zuri, lakini *kuzindua* na *kuzingua* ni kumfanyia mtu jambo zuri. Mwandishi anayatumia maneno haya akitegemea msomaji atakuwa makini ili kuelewa mwandishi ana maana gani. Anatumia maneno yenye kinyume cha mambo ili kumpa mstuo msomaji, kwani anafahamu ni kwa kiasi gani kila neno kwa muda upi linafanana na kutofautiana na jingine.

Aidha, mwandishi ametumia maneno yanayokinzana, yaani maneno ambayo ni kinyume kiasi kwamba ukitazama juu juu, utaona kama upuuzi, lakini ukizingatia utaona kuna maana ya msingi, anasema:

> Bwana Msa maneno yake makubwa anapotaka kumfahamisha mtu jinsi ubongo wake unavyofanya kazi yalikuwa, "ukitaka kujua asili ya mwangaza, ingia kizani", au "ukitaka kujua raha ya mtu aliyesoma tazama taabu ya mtu asiyesoma (uk: 3).

Kimsingi mwandishi anataka kumuonesha msomaji kwamba mtu hujifunza kwa kuangalia matatizo yaliyomo katika jamii yake inayomzunguka.

Katika *Kosa la Bwana Msa* uk 53, mwandishi anatumia maneno yanayokinzana lakini yenye ukaribu wa maana. Neno *bibi* na *mke* yanakaribiana kimaana, lakini katika mazingira na utamaduni wa mwandishi maneno haya yana maana iliyo kinyume. *Bibi* ni mwanamke anayeishi na mwanaume bila kufunga ndoa wakati *mke* ni mwanamke aliyefunga ndoa. Hali kadharika kwa *bwana* na *mume* ni maneno yanayokaribiana kimaana lakini yana maana iliyo kinyume kama ilivyo kwa *bibi* na *mke*. Watu wanaoishi kama *bwana* na *bibi* huishi bila ya ndoa, jambo ambalo kimsingi halikubaliki kidini na kimila katika jamii ya mwandishi. Na watu wanaoishi kama *mke* na *mume* wanakubalika kidini na kisheria. Mwandishi ametumia maneno hayo ili kuweka msisitizo wa jambo alilotaka jamii ilitambue, hasa dhana ya ndoa halali kulingana na utamaduni wa jamii husika.

Pia kwa kumtumia mhusika bi Shinuna anasema:

> Nitajie mwingine! Ndio pale ulipoona kuwa polisi wamefaulu kuuzuia mpango wangu usiangue, wewe ukanijia mbio mbio na bashasha zako za uzembe, na lugha sijui mwanzo wala mwisho ati, kihunzi kimefanya mapinduzi; Nini kihunzi? Ukaniingia kwa masihara ya utani kuja kunikejeli – sijui, maiti anatembea; sijui, wahai hawaonekani, anaonekana maiti tu (uk: 104).

Katika dondoo hii mwandishi anatumia maneno yanayokinzana kuonesha msisitizo katika jambo analolizungumzia. Jambo la msingi ambalo mwandishi analisisitiza

hapa ni kuwa dunia haiendi kama tunavyotarajia sisi. Kwani katika hali ya kawaida kihunzi ni kitu kisicho na uhai, na maiti haitembei. Hivyo, mwandishi anataka kusisitiza kuwa jamii yetu imetawaliwa na matendo ambayo ni kinyume, kila lililo baya linaonekana kuwa ni zuri na kila lililo zuri linaonekana kuwa ni baya.

#### 4.1.3.4.2 Sitiari

Sitiari ni usemi ambao huhusisha vitu viwili visivyo na uhusiano wa moja kwa moja bila kutumia viunganishi. Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo inaeleza sifa za kitu fulani kwa kukifananisha na kingine; inahusisha vitu viwili ambavyo ni tofauti kabisa kimaumbile (Mulokozi na Kahigi (1979); Lakoff na Johnson (1980); Lakoff na Turner (1989); omari (2006). Mulokozi na Kahigi (1979:38) wanafafanua kwamba sitiari ina sehemu tatu, yaani kizungumzwa, kifananishi na kiungo. Wanaendelea kusema kuwa binadamu katika uhusiano wake na binadamu wenzake na katika mwingiliano wake na mazingira yake, hujifunza kuumba dhana dhahania kwa kuhusisha vitu vinavyomzunguka, kuviona au kuvisikia. Kwa mfano, mtu anaweza kusema, Jane ni malaika; akiwa na maana kuwa Jane anazo sifa, tabia na matendo ambayo kwa kawaida tungeyahusisha na malaika. Sifa hizo zinaweza kuwa urembo, uaminifu, upole n.k. Kwa hiyo, kizungumzwa ni Jane, kifananishi ni malaika na kiungo ni zile sifa na tabia za malaika.

Dhima ya sitiari ni kumfikirisha mtu aende mbali zaidi kuhusu jambo fulani. Wamitila (2003: 202) anaelezea kuwa sitiari hutumika kulenga hisia au picha fulani. Kwa mfano, unapomwita mtu fulani nguruwe inawezekana akawa na sifa zinazofanana na za mnyama huyo kama vile uchafu, ulafi n.k.

MSA, katika riwaya zake, ametumia tamathali hii japokuwa si kwa kiasi kikubwa sana. Kwa mfano, katika *Mzimu wa Watu wa Kale* mwandishi anasema: “Yule bibi, hapana shaka, alikuwa na wasiwasi tangu hapo. Wakati mwingi huambiwa, ‘Roho ni

bao,’ yaani huona yatakayokuja *kabla ya hayajatokea (uk: 14).”* maneno *roho* na *bao* hayana uhusiano wa moja kwa moja, isipokuwa sifa bainifu za neno *bao*; ambazo ni kutabiri matendo yajayo. Kwa vile wakati mwingine kutokana na hali au matendo ya mtu kutabiri hali ya baadaye ndio maana roho inaelezwa kuwa inaweza kutabiri mambo yajayo kama ilivyo katika bao.

Katika *Kosa la Bwana Msa,* mwandishi pia ametumia sitiari. Kwa mfano, uk. 11 mhusika Bi Shinuna anapogombana na Jamila anasema: *“Sasa wewe ndicho kidimu cha shamba aliyeninyang’anya mume wangu?”* kwa sababu Bi Shinuna anaamini kuwa Jamila ni hawara wa mumewe, anafananisha tabia za Jamila na ‘kidimu’ au ‘kidiku’. Kidimu ni kuku mwenye manyoya yaliyokunjika kwa juu yakawa kama yamesimamisha ncha zake; au anafananishwa na kuku ‘kishingo’, yaani kuku aliyekosa kuota manyoya shingoni. Kidiku ni kitu ambacho kimebaki, kisicho na thamani. Hivyo, anamuona jamila kama mabaki ambayo hayana thamani.

Aidha, katika uk. 26 mwandishi anasema: *“Naona umefuatana na Bwana Msa. Hupajui hapa wewe – yeye ndiye aliyekuleta nini? Umempata wapi jini huyu?* Hapa Bwana Msa na jini ni vitu viwili ambavyo ni tofauti kimaumbile. Anafananisha sifa za jini na tabia ya Bwana Msa. Kutokana na ukweli kwamba Bwana Msa anaujuzi wa kutatua matatizo ya watu, hasa yanayoonekana kama yameshindikana kwa binadamu wa kawaida ndio maana anafananishwa na jini. Pia katika uk. 108 mwandishi ametumia sitiari anaposema:

> “Unaniambia mimi kinyesi?
> “Kwani tangu hapo hujijui mwenyewe kama wewe ni kinyesi, mpaka nilipokupigia mimi mbiu masikioni mwako?”

Hapa mtu anafananishwa na kinyesi, kwa kupewa sifa za kinyesi, labda ni mchafu, anatoa harufu n.k.

#### 4.1.3.4.3 Tashihisi

Senkoro (1982: 14) anadai kuwa tamathali hii pia huitwa fasili ya binadamu. Anaendelea kusema kuwa huvipa uwezo wa kibinadamu vitu visivyo na sifa hizo. Mwandishi katika riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale ametumia tamathali hii anaposema: "… palizuka kichaka hicho, pakawa na miti inayogombania nafasi" (uk: 19). Katika hali ya kawaida miti haiwezi kugombana, hivyo miti imehuishwa na kupewa uwezo wa kibinadamu.

#### 4.1.3.4.4 Tashibiha

Tashibiha ni tamathali inayoonesha ulinganisho wa moja kwa moja na hutambulishwa kwa viunganishi; 'kama', 'mithili', mithili ya, n.k. Muhamed Said Abdulla ametumia tashibiha katika riwaya zake. Kwa mfano, mwandishi anaposema:

> …, na mara alikurupuka asisimame ila mpaka pale alipokuwapo Bwana Msa; jicho linamwenda kama saa …
> Kijana Yule wa Kiswahili alikuwa kipandikizi cha mtu, mweusi wa rangi, macho mekundu kama pilipili hoho…
> Kinywa chake kilikuwa kipana na mdomo wake wa chini ulikuwa na tabia ya kuanguka mara kwa mara na kuelemea kilambamchuzi…, lakini kidevu chake safi kama yai.
> Sura yake hasa ilishabihi picha ya simba jike…, lakini hata sauti yake pia ilikuwa kama inatoka kinywani mwa simba (uk: 43).

Mwandishi anafananisha mzunguko wa jicho na mwendo wa saa, rangi ya macho na rangi ya pilipili, kidevu kutokuwa na uchafu kumefananishwa na yai, pia sauti yake inafananishwa na ya simba. Hapa anahusianisha vitu viwili visivyofanana kwa kutumia viunganishi.

### 4.1.3.5 Matumizi ya Mchezo wa Maneno

MSA ametumia vizuri maneno yanayofanana na yanayokaribiana kimaana. Kwa kutumia visawe au maneno haya ameweza kuelezea kwa umahiri na ufasaha jambo

alilolikusudia kutegemeana na utamaduni wa mwandishi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale,* mwandishi ametumia maneno yaliyokaribiana maana kutofautisha maneno hayo. Huu ni ufundi mkubwa wa kutumia lugha ambao mwandishi ameuonesha. Wakati mhusika Bwana Msa alipomshitua mhusika Najum katika harakati zake za kutafuta kitabu cha *Kinyume cha Mambo,* akiwa tayari kachomwa na kitu asichokifahamu alipomtembelea Bwana Msa nyumbani kwake. Na kumbe ilikuwa ni sindano iliyoachwa kwenye mfuko wa shati ulioshonwa upande, anasema:

> Ahlan, Najum! Nimekustua au nimekuzindua? Ikiwa nimekustua itakuwa nimekuroga, lakini, ikiwa nimekuzindua, itakuwa nimekuzingua. Bali ilivyokuwa hapo ulipochutama pana zindiko langu, na litayari kumzuga mtu ye yote atakayejitia umbeya, hapana shaka kwamba kutokea kwangu hivi sasa nikasimama mbele yako namna hii, kumekuzingua (uk: 4).

Dondoo hii inaonesha ni kwa jinsi gani anavyoweza kutumia maneno yanayokaribiana kimaana kuonesha tofauti za maneno hayo. Hii inatokana na ukweli kwamba neno kustua lina maana ya kuogofya na hasa kwa mtu ambaye alikuwa ametopea katika fikra, anapostuliwa huwa anarudi katika hali yake ya kawaida lakini kwa kubabaika. Kuzindua ni kuirudisha akili kuwa katika hali ya umakini. Hivyo, maneno hayo yamehusishwa na kuroga na kuzingua. Kuroga ni kumfanyia mtu jambo ili awe anatenda mambo bila ufahamu au kujielewa. Kuzingua ni kumfanyia mtu dawa ili atokane na matatizo yaliyosababishwa na kurogwa na arudie hali yake ya kawaida. Ndio maana mwandishi kupitia mhusika mkuu Bwana Msa anasema; “ikiwa nimekustua itakuwa nimekuroga lakini ikiwa nimekuzindua, itakuwa nimekuzingua”.

Vile vile, katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa,* mwandishi ametumia maneno yanayofanana maana kuelezea dhana zinazofuatana. Kwa mfano, wakati Jamila anatoroka Chwaka kwenda mjini kwa Mwatenga, aliondoka kwa haraka huku

akijificha kwa sababu hakupenda watu wengine wafahamu anakoenda. Mwandishi anasema kwamba: “Jamila alisahau kuchukua alipoondoka kwake kwa haraka na wahaka, hasa chupa ya maziwa na podari ya mtoto.” (uk: 43)

Wahaka ni hali ya kuwa na wasiwasi. Hivyo, hali ya wasiwasi na haraka vilisababisha Jamila kusahau vitu vya muhimu kwa mwanae kama maziwa na podari. Uteuzi wa maneno haraka na wahaka, umesadifu mazingira ya hali ya wasiwasi kwa kitendo alichokifanya Jamila. Hapa mwandishi ametumia lugha yenye mapigo na vina inayomvuta msomaji, kufanya hivi kunahitaji ubunifu na umahiri wa hali ya juu sana wa matumizi ya lugha.

Katika uk. 53 mwandishi anasema:

> Ulipotoka chumbani kwako, hukufanya jambo lolote ila kwenda kuwakagua wao kwanza, na huko ni kuwaamkia; na kuamkiana kunazaa kusuhubiana, kupendana na kuheshimiana.

#### 4.1.3.6 Matumizi ya Vilugha

Vilugha ni lugha ambayo kimuonekano ni kama Kiswahili lakini si lugha sanifu, inawakilisha kundi fulani la watu. Lengo la kutumia vilugha ni kumfanya msomaji abaini aina ya mhusika anayezungumziwa, lugha anayoitumia na tabaka au kabila analoliwakilisha. Kutokana na vilugha, msomaji huweza kubaini kuwa mhusika ni mtu wa shamba, mtu asiyejua vema Kiswahili kutokana na asili yake. Kimsingi, vilugha hulenga makundi maalum katika jamii. MSA ametumia mbinu hii katika riwaya zake ili kufikisha ujumbe alioukusudia kwa hadhira yake.

Katika riwaya yake ya *Mzimu wa Watu wa Kale* mwandishi anawatumia wahusika Mmanga, na Baniani kudhihirisha matumizi ya vilugha. Mwandishi anawatumia wahusika Bwana Msa na Inspekta Sefu, pale walipowatembelea Mmanga na Baniani kwa ajili ya kuwahoji kutokana na mauaji ya Bwana Ali. Bwana Msa na Inspekta

Sefu wanakutana na watu hawa ambao kupitia mazungumzo yao, wanaonekana dhahiri si raia wenye asili ya Tanzania.

Anapoulizwa na Inspekta Sefu kuhusu mgeni wake aliondoka wakati gani? Mmanga alijibu:

> Sigyjui mimi wakti maondoka; sinaona yeye wakti matoka, lakin wakti Imagharibi. Mimi naona haiku bas; mangojea mangojea we alashan ya shakula lakin haij- hata saa sita fil-leil nafunga mlango yangu, nalala. Wlau kama yeye mgyeni haba, laakin si mtoto mdogo, Ya nini nashughulika mimi? (uk: 52).

Pia Sefu alipokuwa anamuuliza swali Seti B. Sumatra (Baniani), kuhusu Bwana Ali, kuwa alienda kwake kufanya nini? Baniani alijibu:

> Aa… ile iko biashara. Mimi nunua mali ake ote, mpa elpu hamsini, chukua rishit yake, baki yake elpu kumi, iko agana kuja chukua leo- hapana apa- kwenda majini ote bili, dukani yangu. Laakin paka shasha mimi gojea, gojea tu, hapana kuja yeye (uk: 62).

Licha ya kuonesha kuwa wazungumzaji hawa wanaongea lugha ambayo sio sanifu, mwandishi anataka kutujuza kwamba katika jamii kuna matabaka. Na si matabaka tu, bali anataka kutueleza kuwa tabaka la wenye nacho ni wageni ambao asili yao si Tanzania. Hii ni kutokana na ukweli kwamba wakati mwandishi anaandika riwaya hii miaka ya 1960 njia kuu za uchumi zilikuwa hazimilikiwi na wenyeji. Wamiliki wengi walikuwa ni Wahindi na Waarabu, hususani Zanzibar.

Aidha, mwandishi anataka kutuonesha unyonyaji uliofanywa na wageni kwa wenyeji. Tunaona namna Baniani anavyonunua mali yote ya Bwana Ali kwa pesa kidogo tu (sh.60, 000/=), na hata baada ya kugundua kuwa Bwana Ali kauawa anadiriki kuipekua maiti na kuchukua pesa za Bwana Ali.

Kwa upande wa *Kosa la Bwana Msa*, mwandishi ametumia vilugha kuonesha matabaka ya watu na asili ya watu. Kwa kuwatumia wahusika Shoka na Joka anataka kuonesha tabaka la vijana wa mtaani wasio na kipato ambao wanaendesha maisha

yao kwa bahati nasibu tena kwa njia zisizo halali kama ujambazi. Kwa mfano, mwandishi anasema:

> "Shoka," aliita Joka.
> "Yes, Jok," alijibu Shoka.
> Unathink wewe ana kazi gani yule safari hii? Aliuliza Joka. Unaweza kuijaji wewe mwenyewe katika ile ile kazi ya kwanza; lakini kazi ya safari hii, aonavyo bibi mwenyewe, imezidi utaf, ndiyo maana ya kutupa kama tulivyoambiwa hapa – miguu yetu.

Dondoo hii inaonesha matumizi ya lugha isiyo sanifu, ametumia lugha ya mtaani kuonesha kuwa watumiaji wa lugha hii ni vijana na ambao hawajasoma pia ni tabaka la wasio nacho.

Pia ametumia vilugha kuonesha asili ya mtu, kwa mfano, anamtumia Aziz anapojibu swali la Mwatenga kuhusu wapi pazuri Unguja ama Dubai? Anajibu kwa kusema:

> Lakini mimi makwisha kwambia Dubai bora. Sasa mimi tasema nini enh, shemeji ma- Mana – tanga? Mimi nasema I'ley mimi naona maslaha nayo, na Dubai imenyanyua mimi juu kwa juu. Bila shaka Dubai nzuri zaidi kuliko Unguja mahali mazaliwa mimi (uk: 69).

Mwandishi ameitumia dondoo hii kuonesha watu wasio na asili ya Tanzania lakini pia anaonesha kwamba wanajiweza kiuchumi, yaani ni tabaka la juu.

### 4.1.4 Uumbaji wa Wahusika Katika Riwaya za MSA

Mhusika ni kiumbe anayepatikana katika kazi ya kifasihi na ambaye anafanana na binadamu na ana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa ambazo hutambulishwa na mazungumzo na matendo yake. Kazi zinazoegemezwa katika mitazamo ya kihalisia zinamsawiri mhusika kwa namna inayokaribiana sana na binadamu katika ulimwengu wa kawaida (Wamitila 2003).

Naye Senkoro (1982), anafasili wahusika kama watu ama viumbe waliokusudiwa na mwandishi wawakilishe tabia za watu katika kazi za fasihi. Wahusika hawa hubebeshwa tabia za binadamu walio katika jamii halisi.

Hivyo tunaweza kusema, wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya fasihi. Viumbe hawa ni wa mawazoni wanaoumbwa na mwandishi na kujitokeza katika kazi ya fasihi. Msanii huwabuni kutokana na maisha ya jamii yake kulingana na kile anachotaka kukifafanua. Katika kazi za fasihi zenye mtazamo wa kihalisia wahusika wake huwa wanakaribiana sana na binadamu halisi.

Wahusika hujengwa kutokana na mambo mbalimbali kama, dhana fulani ya kimaisha kwa mfano, wema, utu, ujasiri, ulaghai, uadilifu, utiifu n.k. pia huweza kujengwa kutokana na tabia ya mtu ambaye mwandishi amempeleleza au kumsikia akihadithiwa au kusoma mahali. Mhusika pia katika kazi ya fasihi anaweza kumwakilisha mwandishi mwenyewe.

Uumbaji wa wahusika katika riwaya za upelelezi za MSA ni wa kipekee sana. Katika riwaya za MSA mhusika mkuu anajirudia, yaani anamtumia mhusika Bwana Msa ambaye ni mpelelezi wa kujitegemea katika kazi zake zote. Mhusika mkuu ameumbwa juu ya wengine wote, anawatawala japokuwa si kwa wazi, kwani Bwana Msa ana sifa ya kuwa kielelezo chenye ukamilifu. Wahusika wengine wamenyimwa na msanii kuendelea kiakili na kisaikolojia ili kuweza kubadili mifumo yao ya fikra na utendaji wao. Inaonyesha jinsi wasivyopewa nafasi ya kutafakari mambo, wamefungiwa minyororo ya wajibu usiobadilika, wanabaki walivyo kutoka mwanzo wa riwaya hadi mwisho. Mabadiliko yanayojitokeza ni ya nje tu kama umbo, mavazi, sauti, chakula lakini si mabadiliko ya ndani ambayo yanahusu akili na maendeleo ya kisaikolojia.

Pia mhusika mkuu katika riwaya zake humwakilisha mwandishi mwenyewe kutokana na sifa za mhusika huyo kushabihiana na mwandishi. Kwa mfano, mhusika mkuu katika riwaya za *Mzimu wa Watu wa Kale, Duniani Kuna Watu, Kisima cha Giningi, Siri ya Sifuri, Kosa la Bwana Msa,* na *Mwana wa Yungi Hulewa,* kwa

kuzitaja chache zimetumia mhusika mkuu Bwana Msa ambaye ndiye mwandishi wa riwaya hizo kutokana na sifa za mhusika huyu kushabihiana na mwandishi mwenyewe. Kwa mfano, uvutaji wa kiko, jina Bwana Msa vinashabihiana na mwandishi.

MSA pia katika riwaya zake hupendelea kutumia mhusika shinda. Mhusika huyu yupo kati kati ya wahusika bapa na mviringo. Huwategemea wahusika bapa na duara ili aweze kujengeka, anaendeshwa na mawazo ya wahusika wengine. Kwa mfano, mhusika 'Najumu' ambaye huendeshwa na mawazo ya wahusika wengine anajitokeza katika riwaya nyingi za MSA.

Katika riwaya za MSA wahusika wapelelezi wamekwezwa kuliko wahusika waharifu, kwa mfano, katika riwaya zote za MSA zikiwemo *Mzimu wa Watu wa Kale, Duniani Kuna Watu, Kosa la Bwana Msa, Kisima cha Giningi, Siri ya Sifuri,* kwa kuzitaja chache, mhusika Bwana Msa amepewa uwezo na udadisi mkubwa katika kumng'amua mharifu kuliko jeshi la polisi ambalo linawakilishwa na mhusika inspekta Sefu.

Vile vile, MSA ametumia wahusika bapa katika riwaya zake, hawa ni wahusika ambao hawabadiliki wala hawalingani na maisha halisi. Wahusika hawa hufuata mstari mmoja wa matendo na tabia zilizokusudiwa na mwandishi. Kwa mfano, wahusika kama Bwana Msa, Najumu, na Inspekta Sefu ni wahusika bapa kwa sababu katika riwaya zote za MSA hawabadiliki. Kwa kutumia wahusika hawa mwandishi ameweza kuwasawiri vizuri wahusika wake. Kupitia matendo yao ameweza kumulika vipengele mbalimbali kama wema, udadisi, ubaya, uvivu, kutowajibika, tamaa, wivu n.k. alivyokusudia kuvionesha katika kazi yake.

#### 4.1.5 Msuko wa Matukio Katika Riwaya za MSA

Msuko wa matukio au ploti ni mfuatano wa visa vinavyojenga riwaya na sababu zake. Baadhi ya wahakiki wa kazi za fasihi huyaita matukio haya vitushi, matukio haya ndio hujenga migogoro katika riwaya. Msuko unaathiri kwa kiasi kikubwa maendeleo ya kimuundo ya matendo ya wahusika ndani ya riwaya. Mwandishi wa riwaya ana uhuru na wakati mwingi wa kuweza kuunda msuko changamano. Matukio na matendo yanatazamiwa kuoana na kuingiliana, kimantiki na kwa namna ya kujenga taharuki.

Katika kuwasilisha mawazo aliyoyakusudia mwandishi kwa hadhira, MSA anatumia msuko wa matukio ambao unaweza kumchanganya msomaji. Mtiririko wa matukio ndani ya riwaya zake si wazi kama ulivyo katika riwaya za Shigongo, hii ni kutokana na ukweli kwamba matukio ndani ya riwaya zake yamejisokota kiasi kwamba ni vigumu kubaini nini kinachoendelea. Wakati mwingine msomaji anaweza kufikiri kuwa kuna miujiza inatendeka ndani ya riwaya hiyo kulingana na vitendo vinavyojitokeza. Kwa mfano, matukio kama muungurumo wa sauti za nyani na kima ndani ya mzimu wa watu wa kale, kutoonekana kwa kichwa cha Bwana Ali, kuchomwa na sindano kwa Najum na matukio mengine mengi yaliyojitokeza ndani ya riwaya za MSA.

MSA pia, katika uandishi wa riwaya zake anatumia msuko wa matukio au ploti kwa namna mbalimbali, kwa mfano, katika riwaya yake ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ameunda msuko wa matukio kwa kuzingatia hatua nne. Yaani utangulizi, ambapo huwatambulisha wahusika wanaoongelewa katika sehemu hiyo kwa kutumia vichwa vya habari. Pili, utata ambao hutokea pale ambapo tendo fulani kuu huekekea upande mmoja kisha ghafla likageuka na kuelekea upande mwingine. Kwa mfano, katika *Mzimu wa Watu wa Kale* tunaona utata au mgeuko pale ambapo Najum anaona mtu

aliyeegemea kaburi na miguu yake kainyoosha mbele. Kichwa chake amekipakata mapajani hali amekiwekea mikono yake yote miwili, kisha wanagundua kuwa kile si kichwa bali amepakatishwa boga pasipo kujua kichwa chake kiko wapi. Hatua ya tatu ni upeo, upeo ni kilele cha matendo katika riwaya ambapo kunakuwepo na hali ya wasiwasi kwa msomaji. Kilele kizuri ni kile kinachotosheleza matarajio na kuyageuza kwa utoshelevu matukio katika riwaya. Kwa mfano, katika *Mzimu wa Watu wa Kale* upeo ni pale ambapo maiti ya Bwana Ali inagundulika kuwa haina kichwa na muuaji hajulikani. Nne, ni mshuko, katika sehemu hii msuko hufunuliwa na tunapata suluhisho la mgogoro uliokuwepo katika riwaya. Kwa mfano, hatua ya kugundulika kwa kichwa na muuaji wa Bwana Ali pamoja na sababu za kuuawa kwake. Hatua ya mwisho ni matokeo ambapo mwandishi huhitimisha matukio katika riwaya yake. Kwa mfano, MSA anahitimisha matukio katika *Mzimu wa Watu wa Kale* kwa kuelezea namna alivyoweza kuyajua na kuyapindua matukio yaliyotokea kwa kutumia falsafa yake ya kinyume cha mambo.

Kwa upande wa *Kosa la Bwana Msa* mwandishi ametumia msuko wenye hatua tatu, kwanza ni mgeuko au utata, pili ni upeo na mwisho ni mshuko au ufumbuzi. Kwa ujumla mwandishi ametumia misuko yenye hatua tatu au nne katika kazi zake. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, ametumia msuko wenye hatua nne wakati katika *Mwana wa Yungi Hulewa*, *Duniani Kuna Watu* na *Siri ya Sifuri* ametumia msuko wenye hatua tatu.

### 4.1.6 Mandhari Katika Riwaya za MSA

Mandhari hurejelea wakati maalum na mahali fulani ambapo matendo yeyote yanayojitokeza katika kazi ya fasihi hufanyika. Mandhari huonesha mazingira na wakati kama ni asubuhi, usiku, jioni au mchana tendo limefanyika.

MSA katika uandishi wa riwaya zake anatumia mandhari ya Zanzibar na viunga vyake hususani kabla ya uhuru. Kwa mfano, ametumia miji kama Kikwajuni, Mnazi Mmoja, Baraste, Jongomeo, Dunga, na Unguja katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Pia majina ya miji kama Shangani, Pemba, Zanzibar, na Kazole katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*. Miji kama Unguja, Forodhani, Mikunguni katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa* pamoja na maeneo ya shambani vinaashiria mandhari ya Zanzibar. Hii ni kutokana na ukweli kwamba mwandishi ameathiriwa na mazingira aliyozaliwa na kukulia. Pia uteuzi wa wahusika katika riwaya zake umerandana na mandhari aliyoitumia. Kwa mfano, uteuzi wa majina yenye itikadi za dini ya Kiislamu ni kutokana na utumiaji wa mandhari ya Zanzibar, kwani katika maeneo haya Waislamu ni wengi kuliko Wakristo.

### 4.1.7 Dhamira Katika Riwaya za MSA

Dhamira katika kazi za MSA zimelenga kuelezea namna watu walivyoishi kipindi kabla ya uhuru na mara tu baada ya uhuru. Mwandishi anaonesha namna Wazanzibar na Waafrika kwa ujumla walivyoishi kwa kuthamini falsafa ya Mwafrika hasa kwa kuomba miungu na mizimu yao pale walipopatwa na matatizo. Kwa mfano, anamtumia mhusika Kipwerere kushadidia dhamira hii pale aliposhikwa na maradhi na wazazi wake wakaona ni vizuri kutambikia mizimu kwa sababu waliamini kuwa karogwa. Kwa mfano, mwandishi anaposema:

> Mambo yalipokithiri, wazee wake walifika kwa waganga kutazamia, nao kila mmoja alisema lake. Wengine walisema kuwa amerogwa na wachumba waliokuwa wakimtaka wakamkosa. Wengine walisema kuwa amedhurika katika kile kichaka cha *'Mzimu wa Watu wa Kale'* … (uk: 10).

Mwandishi pia anaonesha matabaka yaliyokuwepo kipindi cha ukoloni na mara baada ya uhuru. Matabaka hayo ni Wazungu, Waasia na Waarabu ambao walimiliki

njia kuu za uchumi na Waafrika ambao walichukuliwa kama watwana waliofanya kazi kwa wenye nacho. Hata wale walioajiliwa hawakuwa na nafasi za juu. Mwandishi anawatumia wahusika Kulwa na Masanja ambao walifanya kazi za kulima na kuangalia mifugo kwa Bwana Ali katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Pia katika *Kosa la Bwana Msa* matabaka haya yanaoneshwa kupitia watumishi wa ndani wa mhusika Jamila na Bi Shinuna.

Katika kujadili nafasi ya mwanamke katika jamii, mwandishi anaonesha namna wanawake hasa Wazanzibar walivyoishi kabla na mara tu baada ya uhuru. Kwamba mwanamke aliishi kwa kumtegemea mwanaume, hakuwa na uhuru wa kujiamulia juu ya maisha yake. Mwandishi anawatumia wahusika Kipwerere katika *Mzimu wa Watu wa Kale* na Jamila na Mwatenga katika *Kosa la Bwana Msa*. Kwa mfano, pamoja na kwamba Jamila na Mwatenga ni wasomi wanategemea kuolewa ili kuendesha maisha yao.

Mwandishi pia ameonesha watu walivyoishi kwa utu japokuwa kulikuwa na mapungufu ya hapa na pale katika maisha. Kwa mfano, suala la yatima walilipa uzito, yatima walilelewa kwa upendo mkubwa bila manyanyaso kutoka kwa waliowalea. Mhusika Alfred katika *Mzimu wa Watu wa Kale* kwa mfano, alilelewa na Bwana Ali kama mwanae kiasi cha watu kutokujua kama si mtoto wake.

Kimsingi katika kujadili dhamira mwandishi kwa kutumia mandhari ya Zanzibar ameonesha namna watu wa zamani walivyoishi na kutatua matatizo yaliyojitokeza katika jamii zao.

## 4.2 Kazi Teule za Shigongo

Shigongo amejitokeza kuwa mwandishi na msambazaji wa riwaya ya upelelezi ya Kiswahili ndani ya nchi na hata nje ya nchi kupitia vitabu na magazeti kama *Uwazi, Risasi, Championi, Ijumaa na Ijumaa Wikienda* ambayo hutolewa kila wiki. Riwaya

zake zimejikita katika kuiangalia jamii ya sasa namna ilivyobadilika kutokana na ongezeko la maovu, athari za sayansi na teknelojia pamoja na wakati. Katika riwaya zake zikiwemo *Rais Anampenda Mke Wangu*, *Kifo ni Haki Yangu* na *Damu na Machozi* anazungumzia matatizo kama mauaji, ubakaji, wizi, unafiki, usaliti na mengine mengi ambayo yamekithiri katika jamii ya sasa.

### 4.2.1 Kifo ni Haki Yangu: Mawazo ya Jumla

*Kifo ni Haki Yangu* ni riwaya inayojadili masuala mbalimbali ya maisha katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii. Katika riwaya hiyo, mwandishi amewachora wahusika wake kwa namna wanavyowakilisha maisha ya sasa. Mwandishi kupitia riwaya zake, amefanikiwa kuonesha matukio mbalimbali yanayoshadidia hali ya sasa ilivyo katika jamii.

Katika *Kifo ni Haki Yangu,* mwandishi amezungumzia suala la maadili katika jamii. Anaonesha namna maadili yalivyomomonyoka katika jamii. Amewatumia wahusika Mzee Msangi, Padri Petro, Padri William na watoto wa bi Veronika kuonesha uozo uliomo ndani ya jamii tunayoishi. Anaonesha ubakaji ulivyokithiri katika jamii na hakuna hatua zinazochukuliwa kwa wahusika. Kupitia mhusika Camilla mwandishi anasema:

> … Mimi ni sawa na mjuukuu wako lakini umeniharibu vibaya sehemu zangu za siri na sijui kama kuna mwanaume atakayetaka kunioa…
> “Hayo si masuala yangu! Lala chali” Mzee Msangi alisema hayo kwa ukali, akimsukuma Camilla kitandani na kumwingilia tena. Hakumfanyia kama kawaida ya watu wengine wanavyofanyiwa katika tendo la ndoa (uk: 4).
> … Watoto wale hawakujali ugonnjwa aliokuwa nao Camilla. Walimwingilia kila siku bila huruma, tena usiku na mchana. Alikuwa bado ni mtumwa wa ngono hata mahali alipokimbilia… kazi yao ikawa ni kumbaka Camilla bila kuchoka. Japo alilia, akiomba msaada, hapakuwa na mtu wa kumsaidia (uk: 12-13).

Kuhusu suala la malezi ya watoto, anaona malezi ya watoto ni jukumu la wazazi wote wawili na jamii kwa ujumla. Mfano anafafanua kwa kumtumia mhusika Camilla ambaye anafiwa na mama yake pasipo kumjua baba yake na kupelekwa kituo cha kulelea watoto. Mwandishi anasema, "Mama yangu hakuweza kuiona siku iliyofuata. Hakutoka katika chumba cha upasuaji akiwa hai,..." (uk: 2). Hapa mwandishi anataka kutujuza kuwa mtoto Camilla angelelewa na wazazi wake asingekutwa na madhira yaliyompata maishani mwake. Hata Mzee Msangi baada ya kumchukua kituo cha kulelea watoto na kutimiza wajibu wake kama mzazi, bado Camilla angekua vizuri. Hapa mwandishi anaonesha namna jamii ya sasa ilivyokosa utu na uaminifu tofauti na jamii ya zamani. Hili limechangia matatizo yote yaliyomkuta Camilla. Mwandishi anasema:

> ... Mzee Msangi alifoka, papohapo akawaamuru wanaume alioingia nao ndani wapande kitandani. Wote wawili wakatii amri hiyo. Walimweka katikati yao, bila kujali alikuwa mtoto mdogo kiasi gani, wakaanza kumwingilia kwa zamu (uk: 9)

Dondoo hii inaonesha ni kwa jinsi gani maadili yalivyomomonyoka. Watu wazima kumbaka mtoto mdogo si utu na ni hatari kwa jamii. Mwandishi anaonesha namna binadamu walivyogeuka wanyama kwa binadamu wenzao.

Mbali na hilo, mwandishi pia anaionya jamii kuhusu kuwalea yatima, hasa wale wanaochukua jukumu la kuasilisha watoto kutoka katika vituo vya kulelea watoto. Anaonesha namna wanaoasilisha watoto wanavyoweza kuwaharibu watoto hao. Kwa mfano, mwandishi anasema:

> Pamoja na ukatili aliofanyiwa na Mzee Msangi, Camilla hakuwa na mahali pengine pa kwenda ... Ukatili wa Mzee Msangi ulimchosha. Hakutaka tena kuwa mtumwa wa ngono, kazi aliyoifanya kwa miaka kumi (uk: 4).

Suala la unyonyaji na umaskini limezungumziwa pia. Mwandishi, kwa kumtumia mhusika Bibi Veronika, anaonesha watu wenye uwezo kama Mzee Msangi

wanavyowatumikisha watu wa hali ya chini bila kujali maslahi yao. Matokeo yake kuishi katika lindi la umaskini uliokithiri.Tunaweza kuliona hili katika maongezi ya Bibi Veronica na Camilla. Mwandishi anasema:

> Walipofika eneo la Mtoni kwa Azizi Ali, walishuka na kutembea hadi mtaa wa Ntomoko, nyumba namba 26, ilikuwa nyumba ndogo ya mbavu za mbwa.
> "Hapa ndipo nyumbani kwangu, mjukuu wangu na hiki ndicho kibanda changu nilichojenga baada ya kufanya kazi kwa Mzee Msangi miaka zaidi ya thelathini"
> Wanangu wanaishi hapa peke yao. Nilishindwa kuwalipia ada za shuleni, hivyo wanakaa tu nyumbani nikiwatunza (uk: 11).

Nukuu hizi zinaonesha maisha aliyokuwa akiishi Bibi Veronika na watoto wake yalivyozungukwa na umaskini japokuwa amefanya kazi kwa tajiri kwa muda mrefu.

Aidha, mwandishi amezungumzia suala la ukosefu wa elimu ya afya na uzazi kwa vijana. Mwandishi anaonesha namna vijana wanavyofanya ngono zembe na ubakaji bila kujali afya zao. Kwa mfano, mwandishi anaposema:

> Usiku ule hakulala. Alibadilishwa kutoka kwa mvulana mmoja hadi mwingine, akifanyishwa tendo la ndoa bila ridhaa yake…
> "Jamani lakini mimi ni mgonjwa!"
> "Tuko tayari kuingia ubia kwenye hayo maradhi yako, ili mradi tule uroda!"

Nukuu hii inaonesha namna vijana wanavyoishi bila kujali afya zao kwa kuendekeza ngono zembe.

Mtunzi pia ametumia motifu ya safari ili kuelezea urefu wa safari ya maisha ya mwanadamu hapa duniani, na vikwazo mbalimbali ambavyo mwanadamu huyo anakabiliana navyo. Safari ya mhusika Camilla ni safari iliyotawaliwa na mambo mengi ya ajabu, na ya kutisha kiasi cha kukatisha tamaa. Miongoni mwa mambo hayo ni kubakwa na wanaume wengi, kutembea kwa miguu umbali usio wa kawaida, kulala katika mashimo ya maji taka. Urefu wa safari ya mhusika Camilla na misukosuko anayoipata, unajidhihirisha katika usemi uliozoeleka katika maisha

halisi ya mwanadamu kuwa "maisha ni safari ndefu". Kwa mfano, mwandishi anasema;

> Mvua kubwa ilikuwa ikinyesha. Mvua hiyo ndiyo iliyomrejeshea Camilla fahamu zake. Alishangaa kujikuta amelala chini kwenye dimbwi la maji. (uk: 14).
> …zilikuwa ni dawa za usingizi! Moyo wake uliingiwa na hofu kuwa huenda dawa hizo zilitumika kumpa usingizi na kisha watu kumwingilia. (uk: 22).
> "Hivi kwa nini mmenikeketa bila mimi mwenyewe kutaka? (uk: 46).
> Alilala kichakani akiwa ametandika khanga moja… (uk:128).

Pamoja na kwamba dondoo hizi zinatueleza safari ya maisha ya mwanadamu katika uhalisia wake, ni mfano wa safari ndefu ambayo inakumbwa na vikwazo vya kila aina.

Mwandishi pia ametumia motifu ya ajali ili kuwasilisha mawazo yake. Katika riwaya hii, tunaona kuwa mafanikio au kutokea kwa jambo lolote lile ni matokeo ya ajali. Motifu hii inaonesha ni kwa jinsi gani mwanadamu anaendesha maisha yake pasipo malengo, bali kwa kutegemea kudra za mwenyezi Mungu. Ni katika ajali hizo ambamo mhusika Mathew amejikuta amesonga mbele kutoka katika hatua moja kwenda hatua nyingine, au sehemu moja kwenda sehemu nyingine pasipo kujielewa ni kwa namna gani amefika mahali alipo. Mwandishi analithibitisha hili kwa kuelezea namna Mathew alivyotupwa chooni na mama yake kisha kuokolewa na baadae kuasiliwa na Mzee Douglas na mkewe. Kisha kupelekwa nchini Marekani ambako alifanikiwa kwa kiasi kikubwa, sababu iliyomfanya amuokoe mama yake na kitanzi.

Kwa upande wa nafasi ya mwanamke katika *Kifo ni Haki Yangu*, mwandishi anamchora mwanamke kama mtu anayepambana na ugandamizaji wa wanaume. Japokuwa pia anamchora kama chombo cha starehe. Kwa kumtumia mhusika Camilla, anaonesha namna alivyoamua kupambana na wanaume waliomtesa kwa

kuwakata uume wanaume 521 na kuwaua. Japokuwa halikuwa suluhisho sahihi, lakini lengo la mwandishi lilikuwa kuonesha ujasiri wa mwanamke katika kutetea haki yake. Hii ni kutokana na mabadiliko yaliyopo katika jamii ya sasa, mwanamke ana uhuru zaidi kuliko zama zilizopita. Ndio maana hata Camilla ameweza kuwaadhibu wanaume waliomuonea. Camilla anasema: *"Ninachohitaji mimi ni kumuua huyu mshenzi, kisha niukate uume wake na kuuweka kumbukumbu!"*

Aidha, upande wa dini anaona dini haiwezi kumsaidia mwanadamu, anafikiri mwanadamu anao uhuru wa kutenda anavyofikiri, si kwa sababu ya dini. Kwani hata viongozi wa dini si mifano mizuri kwa jamii inayowazunguka. Mwandishi anasema:

> … Padri William, au Dk. William kama alivyoitwa na wengi, alikuwa shoga na aliianza tabia hii akiwa na umri wa miaka kumi na mitano nchini kwao Uingereza (uk: 29).
> Camilla hakuyaamini macho yake alipomwona Padri Petro akimwingilia kimwili… (uk: 33).

Dondoo hizi zinazonesha namna watumishi wa Mungu wasivyo waaminifu na wanafanya kinyume na mafundisho wanayotoa. Hapa mwandishi anataka kuionesha jamii namna maadili yalivyomomonyoka ndani ya jamii zetu tunamoishi.

Kwa jumla, tunaweza kusema kuwa riwaya ya *Kifo ni Haki Yangu* inazungumzia namna maisha ya sasa katika jamii yalivyo. Kimsingi jamii ya sasa imetawaliwa na matendo maovu, kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, ubakaji, utumiaji wa madawa ya kulevya na mmomonyoko wa maadili kwa ujumla. Mwandishi anaonesha namna watenda maovu wasivyochukuliwa hatua, kwa maana ya kwamba serikali haiwajibiki, hasa kwa wale wenye uwezo ndani ya jamii. Mwandishi pia anaonesha uzembe wa vyombo vya dola katika jamii. Anamtumia mhusika Camilla namna anavyofanikiwa kuwachenga polisi hadi kuua idadi kubwa ya wanaume bila kukamatwa. Vile vile mwandishi anamtaka mwanamke kuwa jasiri, asibweteke na kubaki analalamika bali achukue hatua za kujitetea dhidi ya wanaume.

### 4.2.2 Damu na Machozi: Mawazo ya Jumla

*Damu na Machozi* ni riwaya inayoshabihiana kwa kiasi kikubwa na riwaya ya *Kifo ni Haki Yangu.* Kufanana kwa riwaya hizi kunajitokeza kifani na kimaudhui. Kama ilivyo katika *Kifo ni Haki Yangu*, riwaya ya *Damu na Machozi* inaongelea matatizo ambayo yanajitokeza katika jamii. Tatizo la biashara ya dawa za kulevya na madhara yake kwa jamii linajadiliwa kwa kina. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, tatizo hili limeshamiri sana katika jamii yetu ya sasa na kusababisha madhara makubwa hasa kwa vijana ambao ndio tegemeo kwa taifa.

Ni riwaya inayosimulia maisha ya Wilbert na Isabella. Isabella ambaye anakuwa mwafrika wa kwanza kujinyakulia taji la urembo wa dunia katika mashindano yaliyofanyika nchini Australia. Lakini mara baada ya mashindano hayo, ananusurika kufa kwa ajali ya gari iliyopangwa na Imelda, mwanamke ambaye anampenda sana Wilbert. Anafanikiwa kumrubuni na wanafunga ndoa, lakini baada ya kuzaa naye watoto wawili mapacha (Everine na Evarist) anamsaliti mumewe na kuolewa na Gideon. Mwanaume ambaye anajishughulisha na biashara ya dawa za kulevya na kusababisha familia ya Wilbert isambaratike. Mwishoni Wilbert na Isabella wanaungana tena baada ya kuoana na kuamua kumtumikia Mungu. Hadithi inaendelea na masahibu yanayomkuta Evarist baada ya dada yake Everine kufariki kutokana na dawa za kulevya walizowekewa na Gideon baada ya kufanyiwa upasuaji wakiwa hawajitambui.

Akizungumzia suala la dawa za kulevya, mwandishi anaionesha jamii namna dawa za kulevya zinavyoleta hasara na madhara makubwa kwa jamii. Anaonesha zinavyosababisha vifo kwa watu wasio na hatia, lakini pia kuwasababishia uharibifu wa akili, anasema:

> …“Ninaomba mnisaidie chakula.” Sauti ya mwanamke huyu iliwashangaza na kuwaduwaza kabisa. Iliwachukua sekunde chache sana kuthibitisha kwamba, mwanamke huyo aliyevaa matambara mwenye nywele timutimu na dalili zote za kuchanganyikiwa alikuwa ni Imelda! (uk: 198).
> …“Mmepokea mzigo siyo?”…
> “Pakueni mzigo wote huo na uhifadhiwe halafu mazishi yafanyike leo hiihii!...
> “Tunawazika wakiwa hai?” Mjumbe aliuliza.
> “Wewe unajali nini hao ni watoto wako?” Gideon alijibu… (uk: 231).

Dondoo hizi zinaonesha ni kwa jinsi gani watu wenye uchu wa pesa wanavyoharibu maisha ya watu wengine kiasi cha kusababisha mauaji ili kujipatia pesa.

Mbali na kuzungumzia dawa za kulevya, mwandishi pia amezungumzia usaliti na unafiki katika jamii. Anawatumia wahusika Gideon na Mohamed Azray kuonesha namna watu ambao wanaheshimika mbele za macho ya watu wanavyofanya usaliti kwa kuleta madhara makubwa ndani ya jamii kutokana na shughuli haramu wanazoziendesha, anasema:

> Haiwezekani hawezi kuwa Gideon, wanamsigizia.”… kwa nje Gideon alionekana mtu mwema aliyekuwa tayari kumsaidia mtu yeyote… Hakuna mtu aliyefahamu siri ya utajiri wake, taarifa za kujihusisha na madawa ya kulevya ziliwastua wengi na watu walionekana kuwa tayari kumtetea hadi mwisho (uk: 244).

Dondoo hii inaonesha namna watu waovu wanavyoaminika katika jamii. Pia, kwa Mohamed Azray aliyeweza kuikopesha hata serikali ya Pakstani na kuonekana mwaminifu machoni pa watu alikuwa mfanyabiashara ya madawa ya kulevya na anayehusika na ugaidi. Katika uk. 257 anasema:

> … “Siyo rahisi hakuna mtu hata mmoja awezaye kuingia ndani ya ngome hii… Wewe si mtu wa kwanza kujificha hapa ndani, gaidi wa kimataifa Don, alijificha humu ndani miaka kumi na mitano bila kukamatwa…

Vilevile amezungumzia suala la imani ya dini katika jamii. Ameonesha umuhimu wa binadamu kumtegemea Mungu katika maisha yao yote. Ameonesha kuwa

kumtegemea Mungu ndilo suluhisho la matatizo yote yanayomkabili binadamu. Anawatumia wahusika Wilbert na Isabella ambao pamoja na matatizo na masahibu mengi yaliyowapata katika maisha yao walimtegemea Mungu na mwisho wa yote walipata ushindi.

Tunaweza kuhitimisha kuwa mwandishi wa riwaya ya *Damu na Machozi* anazungumzia namna biashara ya madawa ya kulevya inavyosababisha madhara katika jamii. Mwandishi anaitaka jamii ipige vita jambo hili kwani linaharibu vijana ambao ni tegemeo kwa taifa. Mwandishi pia anaonesha wazi kuwa usaliti ni jambo baya ndani ya jamii kwa sababu huleta maafa mengi. Anaonesha namna usaliti wa Imelda kwa Wilbert ulivyoisambaratisha familia, lakini pia usaliti wa Gedion na Mohamed Azray kwa nchi zao ulivyoleta madhara kiasi cha kusababisha mauaji ya watu wasiokuwa na hatia.

### 4.2.3 Matumizi ya Lugha katika Riwaya za Shigongo

Katika uandishi wa riwaya zake, Shigongo ametumia lugha kwa namna ya pekee pia, kwani kazi zake zimesheheni matumizi ya uwili- lugha (tafsiri), rejesta za aina mballimbali pamoja na dhana zinazoashiria sayansi na teknolojia ili kufisha mawazo aliyoyakusudia kwa wasomaji.

#### 4.2.3.1 Matumizi ya Tafsiri

Mwansoko na wenzake (1996:1) wanaeleza kuwa, tafsiri ni zoezi la uhaulishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine. Fasihi iliyotafsiriwa ni matini iliyohaulishwa katika maandishi kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine.

Hivyo, tafsiri ni dhana inayotumika kuelezea maneno kutoka katika lugha chanzi kwenda katika lugha lengwa bila kubadili maana iliyokusudiwa na mwandishi wa matini chanzi.

Shigongo katika uandishi wa riwaya zake zote anatumia mbinu ya tafsiri, yaani kuandika sentensi au vifungu vya maneno kwa Kiingereza kisha kutafsiri kwa Kiswahili. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kifo ni Haki Yangu* kupitia mazungumzo ya mzee Douglas na mwanae mwandishi anasema:

> "Douglas speaking. May I know who is on the other end!" (Doglas anaongea. Naweza kujua nani yuko upande wa pili?").
> "It's me, Brad! Morning, dad!" (Ni mimi Brad! Habari za asubuhi, baba?)
> "Morning, how are you, son? (Nzuri, hujambo, mwanangu?).
> "I'm fine, and you?" (Mi sijambo, na wewe?)… uk: 68

Vilevile, katika mazungumzo ya Mathew na mlinzi wa MacLennan, mwandishi ametumia mbinu hii ya tafsiri kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Mwandishi anasema:

> "Can I help you?" (Naweza kukusaidia?).
> "Yes, I need your help. I wouid like to know if Mr and Mrs MacLennan still dwell in this house?" (Ndiyo, nahitaji msaada wako. Ningependa kufahamu kama Bwana na Bibi MacLennan bado wanaishi katika nyumba hii!)… (uk: 238).

Hivi ni baadhi ya vifungu vya maneno kati ya vifungu vingi katika riwaya ya *Kifo ni Haki Yangu* ambavyo mwandishi ametumia mbinu ya tafsiri. Mwandishi ametumia mbinu hii kwa sababu za msingi mbili. Kwanza kuonesha kuwa wanaozungumza si watumiaji asilia wa lugha ya Kiswahili, yaani si raia wa Tanzania. Pili, kwa mujibu wa maelezo yake mwenyewe anatafsiri lugha ya Kiingereza ili kuwapa mwanya watu ambao hawajui lugha hiyo ili waweze kujifunza.

Katika riwaya ya *Damu na Machozi* mwandishi ametumia tafsiri kwa lengo na nia ya kuonesha kuwa wazungumzaji si watumiaji asilia wa lugha ya Kiswahili. Pia ametumia tafsiri ili kuwapa mwanya watu ambao hawajui lugha ya Kiingereza kujifunza lugha hiyo. Kwa mfano, kupitia wahusika mbalimbali mwandishi anasema:

> "Why did you kill our children?' (Kwa nini uliwaua watoto wetu?"). Aliuliza Wilbert.
> "Who are you?" (We ni nani?"). Imelda alijibu.
> "I'm Wilbert!" (Mimi ni Wilbert!)…(uk: 150).

Pia, katika mazungumzo ya Wilbert na Mchungaji Warren mwandishi ametumia mbinu ya tafsiri. Anasema:

> "Your church is growing very fast Wilbert!" (Kanisa lako linakua haraka sana Wilbert)…
> "Thanks to the Lord!" (Shukrani kwa Mungu!).
> "How old are you?" (Una umri gani hivi sasa?")…uk: 271

Nukuu hizi ni baadhi tu ya vifungu vya maneno yaliyotafsiriwa kati ya vingi ambavyo mwandishi amevitumia. Na mbinu hii inaonekana kumtambulisha mwandishi huyu kati ya waandishi wengi wa riwaya ya upelelezi ya Kiswahili.

#### 4.2.3.2 Matumizi ya Rejesta

Rejesta (pia rejista au sajili) ni matumizi ya lugha kulingana na muktadha maalum. Miktadha tofauti husababisha aina mbalimbali za lugha. Baadhi ya vipengele vya miktadha hiyo ni mada, eneo la matumizi ya lugha, uhusiano baina ya wahusika, umri, jinsia, wakati, na kadhalika.

Mifano ya rejesta za lugha ni lugha ya mazungumzo, lugha ya sheria, lugha ya biashara, lugha ya sayansi, na lugha ya dini, kwa kuzitaja chache (Massamba 2004).

Mwandishi, Shigongo ametumia rejesta mbalimbali katika uandishi wa riwaya zake zikiwemo; rejesta ya mahakamani, hospitalini, kanisani na mtaani ili kuonesha namna lugha inavyotumika katika sehemu mbalimbali. Katika riwaya ya *Kifo ni Haki Yangu* kwa mfano, mwandishi ametumia rejesta ya mtaani, hospitalini, kanisani na mahakamani. Kwa mfano, kupitia mazungumzo ya vijana wa mitaani mwandishi ametumia rejesta ya mtaani, sanasema:

> Bibie , eleweka basi!"… "Masela hatujaburudika kwa muda mrefu…

> "Oyaaa! Miwayaa! Miwayaa, washikaji! Shangazi ameongea jambo muhimu sana. Kesho si mbali, tusubiri" (uk: 85).

Katika nukuu hizi mwandishi ametumia lugha ya mtaani kuonesha kuwa wanaoitumia ni vijana ambao hawajaenda shule na wanajihusisha na madawa ya kulevya.

Mwandishi pia kupitia mazungumzo ya daktari na mgonjwa anaendelea kusema; "Hizi ni Doxycline, utakunywa moja asubuhi na moja jioni, hizo nyingine nyeupe utakunywa kutwa mara tatu" (Uk. 20). Hapa anaonesha lugha inayotumiwa na daktari katika kumpa maelekezo ya kunywa dawa mgonjwa.

Aidha, mwandishi ametumia rejesta ya kanisani katika maongezi ya sista Flora na Baba Askofu wakati anataka kumsaidia Camilla kuhusu kujiunga na mafunzo ya usista. Mwandishi anatujuza kwa kusema:

> "Tumsifu Yesu Kristo, Baba Askofu!" Sista Flora alimwamkia huku akiinamisha kichwa chake chini.
> "Milele Amina, Sista Flora! Naona umeniletea mgeni?"…

Vile vile, mazungumzo ndani ya mahakama kati ya jaji, mwendesha mashtaka na wakili Mathew yanadhihirisha matumizi ya rejesta ya mahakamani katika riwaya ya Kifo ni Haki Yangu.

> "Mheshimiwa Jaji, kuna shahidi mmoja hakutoa ushahidi wake mara ya mwisho, ningeomba tuanze naye ili mahakama yako tukufu iweze kumsikiliza!"…
> "Mheshimiwa Mathew, naomba uulize maswali!" jaji aliingilia kati.
> "Sina swali zaidi, mheshimiwa jaji…

Kwa upande wa riwaya ya *Damu na Machozi*, mwandishi ametumia rejesta ya mahakamani, mtaani, kanisani na hospitalini.

> "Shahidi nambari tatuuu." Hakimu aliita, ni msichana aliyewapokea Wilbert na Imelda waliporejea hotelini usiku wakitokea disko, aliongozwa hadi kizimbani na kuapishwa…
> "Kwa sababu hiyo naiahirisha kesi hii mpaka tarehe 17 mwezi ujao, mshitakiwa ataendelea kukaa rumande

> mpaka siku hiyo. Dhamana yake bado imefungwa" (uk: 44 – 45).

Katika kuonesha mazungumzo ya watu wanaoishi mitaani na kutumia madawa ya kulevya, ametumia lugha ya mtaani. Kwa mfano, mwandishi kwa kumtumia mhusika Imelda anasema:

> "Yes! Mshikaji gani ananiita?" Ilikuwa sauti ya kukwaruza iliyotoka katika koo la mwanamke huyo (uk: 150).

Ametumia rejesta ya kanisani katika kuonesha imani aliyokuwa nayo Wilbert kwa Mungu, na namna nguvu ya Mungu inavyoweza kufanya miujiza kwa mambo yanayodhaniwa kuwa yameshindikana.

> "Katika jina la Yesu mwachie, ewe kifo na nguvu zako zote mwachie binti huyu. Mungu baba, muumba wa mbingu na nchi mfungue Isabella ili mapenzi yako yatimizwe! (uk: 174).

Katika kuonesha baadhi ya huduma muhimu zinazotolewa hospitalini ametumia rejesta ya hospitalini.

> "Labda apewe chanjo?" Mmoja wa wauguzi aliuliza.
> "Chanjo gani?" Daktari alijibu kwa swali.
> "Si TT?" Muuguzi alijibu.
> "Nafikiri unaongelea Tetanus Toxoid au?" Daktari aliuliza.
> "Ndiyo." Muuguzi alijibu (uk: 180).
> "Mapigo yake yanazidi kushuka! Leteni haraka chupa ya maji ya Normal Saline, pamoja na mirija yake tumwekee katika mishipa. Pia leteni mashine ya hewa ya Oxygen. BP yake ni 60/50 hii ni hatari sana kwa maisha yake" (uk: 261).

Nukuu hizi zinaonesha maendeleo yanayojitokeza katika huduma za afya nchini. Upatikanaji wa vifaa na vitendea kazi vinavyohitajika hospitalini kwa ajili ya maradhi mbalimbali umeongezeka tofauti na zamani.

#### 4.2.3.3 Matumizi ya Dhana za Sayansi na Teknolojia

Shigongo katika uandishi wa riwaya zake anaonesha mchomozo wa maendeleo ya sayansi na teknolojia. Uteuzi wa baadhi ya maneno unafafanua namna sayansi na teknolojia inavyotawala ulimwengu wa sasa bila kujali nchi zilizoendelea na

zinazoendelea. Matumizi ya msamiati unaoashiria vyombo vya usafiri kama magari ya aina mbalimbali, ndege, vyombo vya habari mfano, matumizi ya simu, matumizi ya silaha kama bastola na bunduki za aina mbalimbali, aina za madawa kwa kutaja dhana chache kunadhihirisha wazi kuwa maendeleo ya sayansi na teknolojia yametawala ulimwenu wa sasa.

Katika riwaya ya *Kifo ni Haki Yangu* mwandishi ameteua msamiati kadhaa unaoashiria ongezeko la matukio, huduma, vifaa na bidhaa zitokanazo na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Kwa mfano, baada ya Shumeka kuelezwa siri ya Padri Petro kumficha Camilla na Padri William wakiwa safarini kuelekea Arusha, asubuhi alikimbilia katika kibanda cha simu kupiga simu. Mwandishi anasema:

> "Naomba Dar es Salaam."
> "Namba?" Mhudumu wa simu aliuliza.
> "2184757. Dakika moja shilingi ngapi?"
> "Hamsini."
> "Haya nipigie" (uk: 32).

Pia, mawasiliano baina ya askari katika msako wa mtu (Camilla) anayekata sehemu za siri za wanaume na kuwaua wanatumia simu.

> "Hallo!"
> "Hallo! Shikamoo, Afande!"
> "Marahaba nani?"
> "Hapa ni Arusha Polisi Mkoa!"...(uk: 230).

Dondoo hizi zinaonesha huduma zitokanazo na maendeleo ya sayansi na teknolojia zinavyotumika kurahisisha mawasiliano baina ya mtu na mtu, au hata kurahisisha utendaji wa kazi kama polisi wanavyotumia simu katika harakati za upelelezi wa mhalifu Camilla.

Matumizi ya maneno yanayomaanisha vifaa na bidhaa zitokanazo na maendeleo ya sayansi na teknolojia yameshamiri katika kazi za Shigongo. Hii ni kuonesha namna TEHAMA inavyorahisisha mawasiliano kati ya mtu na mtu au jamii moja na nyingine. Yote haya yanajitokeza katika riwaya zake kwa sababu wakati ambao ameandika kazi zake dunia imetawaliwa na utandawazi. Pia matumizi ya vitu kama,

kamera, viwanja vya ndege, TV uk. 71 na 322, magazeti kama The East African Punch uk. 124.

Pia matumizi ya neno SMG uk. 66 na 236, ambalo ni aina ya silaha yanaashiria namna dunia ilivyotawaliwa na mapigano ya kivita.

Kwa upande wa riwaya ya *Damu na Machozi* mwandishi ametumia vyombo vya mawasiliano kama kituo cha televisheni cha M2M uk. 415, redio na TV uk. 398, aina za magari kama Land Cruiser uk.381 na 385, Toyota Chaser uk 406, silaha kama bunduki aina ya SAR, aina za madawa kama Cocaine uk. 257, Anti Tetanus Serum uk. 180 na Dicrofenag uk. 408. Maneno yote haya yanatokana na athari za sayansi na teknolojia.

### 4.2.4 Uumbaji wa Wahusika Katika Riwaya za Shigongo

Shigongo katika uandishi wa riwaya zake hutumia wahusika mviringo, hawa ni wahusika ambao humkaribia sana binadamu halisi kwa ulinganifu wa wasifu na tabia zao. Wahusika hawa huaminika na kukubalika katika kipimo cha ukweli na uhalisia wa maisha. Wahusika mviringo hukua na kubadilika katika hatua zao za maisha kitabia na kihisia. Wahusika hawa huwa na sehemu ya uzuri na ubaya. Kwa mfano, wahusika kama Kabula, Camilla, Mzee Msangi, Gedion na wengine wana uzuri na ubaya kulingana na matendo wanayoyafanya.

Wahusika wahalifu katika kazi za Shigongo mara nyingi ni wakwezwa kwa sababu wamepewa uwezo usio wa kawaida, na hubadilika kimsimamo kadri riwaya inavyoendelea. Kwa mfano, katika *Kifo ni Haki Yangu*, Camilla ni katili. Anafanya mauaji ya watu 521, anauwa pasipo huruma mpaka alipokamatwa na kufungwa maisha. Camilla amepewa uwezo wa kufanya mambo makubwa ambayo kwa hali ya kibinadamu ni vigumu kuyatenda. Kwa mfano, kuua watu wengi katika mikoa tofauti nchini Tanzania bila kukamatwa, kubakwa na kulawitiwa na wanaume zaidi

ya mmoja akiwa mtoto mdogo na kuweza kutembea kwa miguu masafa marefu, na pia alikuwa na magonjwa ya zinaa aliyoambukizwa na kipigo juu. Mwandishi anaeleza kwa kusema:

> Wote wawili wakatii amri hiyo. Walimweka Camilla katikati yao, bila kujali alikuwa mtoto mdogo kiasi gani, wakaanza kumwingilia kwa zamu (uk: 9).
> Watoto wale hawakujali ugonjwa aliokuwa nao Camilla. Walimwingilia kila siku bila huruma, tena usiku na mchana (uk: 13).

Hata hivyo, Camilla baada ya kukamatwa anabadili msimamo na kujutia maovu yote aliyotenda hasa la kumkata sehemu za siri askari mpelelezi Richard, mwanaume ambaye hakuwahi kumtendea uovu wa aina yoyote.

Madumulla (2009) anadai kuwa wahusika wakwezwa huchorwa kwa lengo la kuwa kielelezo na watetezi wa haki dhidi ya unyanyasaji na uonevu. Ingawa kwa utetezi wa Camilla unaweza kuwa ni kinyume na haki za binadamu kwa kuwa anaua binadamu.

Uumbaji wa wahusika wakuu katika riwaya za Shigongo hutofautiana kati ya riwaya moja na nyingine, yaani hutumia majina ya wahusika wakuu tofauti kwa kila riwaya. Pia ametumia wahusika wa kimapinduzi, hii ni kutokana na hali halisi ya kimapinduzi ambayo inajitokeza katika jamii tuliyomo.

Usawiri wa wahusika katika riwaya za Shigongo hutegemea matendo yao katika kuonesha mambo na matatizo mbalimbali yanayoikabili jamii ya sasa. Kwa mfano, wahusika katika *Kifo* ni *Haki Yangu* wamesawiriwa kuonesha mauaji yalivyokithiri katika jamii ya sasa, ubakaji, wivu, usaliti, unafiki na mengine mengi ambayo yanajitokeza katika jamii tunamoishi. Mhusika Camilla katika riwaya ya *Kifo ni Haki Yangu* kwa mfano, amesawiriwa na mwandishi kuonesha namna wanawake wanavyoonewa na kunyanyaswa katika jamii, pia namna mauaji yalivyogeuka kuwa ni jambo la kawaida lisiloshangaza ndani ya jamii. Mhusika mzee Msangi

amesawiriwa na mwandishi kuonesha unafiki ndani ya jamii, ubakaji na usaliti unavyojitokeza katika jamii. Katika *Damu na Machozi* mhusika kama Gedion amesawiriwa na mwandishi kuonesha watu wanafiki ndani ya jamii bila kusahau wahusika ambao ni wema pia wamesawiriwa kupitia matendo yao. Kwa mfano, Richard, Isabela na Wilbert.

Kimsingi mwandishi Shigongo anawaumba wahusika wake kwa kuangalia matukio ambayo yametawala ulimwengu wa sasa hasa baada ya athari za wakati na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Uumbaji wa wahusika katika riwaya zake unawakilisha kikamilifu hali halisi ya maisha katika jamii ya sasa.

**4.2.5 Mtiririko wa Matukio Katika Riwaya za Shigongo**

Shigongo katika uandishi wa riwaya zake anatumia mtiririko wa matukio ambao si changamano sana kama ilivyo kwa MSA. Katika riwaya zake zote matukio yanaendelezwa bila utata japokuwa anatumia muundo rejeshi, ni rahisi kwa msomaji kubaini tukio fulani limefanywa na nani bila utata wowote. Kwa mfano, mauaji ya wanaume kukatwa sehemu za siri katika *Kifo ni Haki Yangu* yanajulikana nani kayafanya bila utata wowote. Watoto Everine na Evarist kutekwa na kuwekewa madawa ya kulevya tumboni katika *Damu na Machozi* inafahamika ni nani alifanya hivyo. Kimsingi matukio na matendo yote ndani ya riwaya zake yako wazi.

Pia ametumia msuko ambao hautambulishi wahusika katika kazi zake, anaanza na matukio yanayoelezea mgeuko au utata ambao hutokea pale ambapo tendo fulani kuu huelekea upande mmoja kisha ghafla likageuka na kuelekea upande mwingine. Kwa mfano, matukio ya wanaume kukatwa sehemu za siri kila kukicha, kisha mtuhumiwa kukamatwa kabla hajakamilisha idadi ya wanaume aliyoikusudia. Pia katika *Damu na Machozi* hajaanza kwa kutambulisha wahusika wanaozungumziwa,

bali ameeleza matukio yanayoonesha utata moja kwa moja kisha hatua nyingine kufuata.

Hatua ya pili ni upeo, upeo ni kilele cha matendo katika riwaya ambapo kunakuwepo na hali ya wasiwasi kwa msomaji. Kwa mfano, kitendo cha mhusika Camilla katika riwaya ya *Kifo ni Haki Yangu* kumkata sehemu za siri mkuu wa upelelezi kunaleta hali ya wasiwasi kiasi cha kufikiri kwamba muuaji hawezi kukamatwa. Pia kitendo cha mhusika Isabella katika Damu na Machozi kupoteza fahamu kwa miaka mingi kunaleta wasiwasi kwamba hawezi kupona tena. Pia kitendo cha mhusika Evarist kukamatwa na Gedion, ambaye ni jambazi, muuza madawa ya kulevya kunaleta wasiwasi kama hatauawa.

Tatu, ni mshuko, katika sehemu hii msuko hufunuliwa na tunapata suluhisho la mgogoro uliokuwepo katika riwaya. Kwa mfano, migogoro yote kupata suluhisho katika riwaya za *Damu na Machozi* na *Kifo ni Haki Yangu.* Tukio la kukamatwa kwa Camilla kunaleta suluhisho la utata uliojitokeza katika riwaya ya *Kifo ni Haki Yangu,* pia kuuawa kwa Gedion, ambaye ni kiongozi wa kundi la majambazi, wauza madawa ya kulevya kunaleta suluhisho la migogoro ndani ya riwaya ya *Damu na Machozi.*

### 4.2.6 Mandhari Katika Riwaya za Shigongo

Riwaya za upelelezi za Shigongo zinatumia mandhari mchanganyiko, kwa maana kuwa, hutumia mandhari ya Tanzania baada ya uhuru hususani kuanzia miaka ya 2000 na nje ya nchi. Kwa mfano, matumizi ya majina ya miji kama New York na Los Angeles nchini Marekani, pia majina ya nchi kama Canada, Urusi, Asia na Australia katika riwaya ya *Kifo ni Haki Yangu*. Matumizi ya majina ya miji kama Sydney nchini Australia, Baghdad nchini Pakistani na nchi ya Slovenia katika riwaya

ya *Damu na Machozi*. Hii inaonesha wazi kuwa riwaya zake hutumia mandhari changamano kwani huhusisha mazingira ya nchi mbalimbali.

Mwandishi anatumia mandhari changamano kuonesha namna utandawazi ulivyoshamiri na kuifanya dunia kuwa kama kijiji. Hii inasaidiwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia yaliyopelekea kuvumbuliwa kwa vyombo vya usafiri kama ndege vinavyomsaidia binadamu kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa urahisi na kwa muda mfupi.

#### 4.2.7 Dhamira Katika riwaya za Shigongo

Dhamira katika riwaya ya upelelezi ya Shigongo imelenga kuonesha namna wakati unavyopelekea mabadiliko katika jamii hasa baada ya maendeleo ya sayansi na teknolojia. Mwandishi anaonesha maisha ya sasa yalivyobadilika kimaadili na hata kimazingira. Kupitia riwaya zake za *Rais Anampenda Mke Wangu*, *Kifo ni Haki Yangu na Damu na Machozi*, mwandishi anaonesha namna jamii ilivyojaa uozo. Kwa mfano, anaonesha namna mauaji yalivokithiri ndani ya jamii, usaliti, ubakaji, matumizi ya dawa za kulevya na aina zote za uovu ndani ya jamii. Kimsingi haya ndiyo mambo yanayosumbua jamii nyingi hususani katika bara la Afrika.

Suala la mmomonyoko wa maadili amelijadili kwa kirefu sana. Kwa mfano, watu wazima kufanya ngono na watoto wa umri wa watoto au wajukuu zao ni jambo la kawaida kwa sasa. Mwandishi kwa kumtumia mhusika Mzee Msangi katika riwaya ya *Kifo ni Haki Yangu* anaonesha namna maadili yalivyomomonyoko ndani ya jamii kwa sababu anambaka mtoto Camilla akiwa na umri sawa na mjukuu wake. Ndani ya jamii wanawake wanabakwa ovyo bila ridhaa yao. Kwa mfano, kitendo cha mtumishi wa Mungu, Padri Petro kumnywesha dawa za kulevya kisha kumbuka Camilla inaonesha mmomonyoko wa maadili ndani ya jamii tunamoishi.

Mwandishi anaonesha namna mauaji yalivyokithiri ndani ya jamii ya sasa, Kwa mfano, kitendo cha mzee Msangi kuua watu wengi bila kukamatwa ili kulinda uozo anaoufanya ni dhahiri kuwa utu ndani ya jamii tunayoishi umekwisha. Watu wenye pesa wanafanya wanavyotaka, wako juu ya sheria kwa sababu vyombo vya dola haviwagusi ili kuwachukulia hatua zinazostahili.

Suala la utumiaji wa madawa ya kulevya na namna jamii inavyoathirika na jambo hili pia vimejadiliwa. Kwa tamaa ya pesa na madaraka watu wako tayari kuua na kuwadhuru binadamu wengine. Kwa mfano, mhusika Gedion katika *Damu na Machozi* anafikia hatua ya kuua hata watoto wadogo anaowatumia kama vyombo vya kusafirishia madawa ya kulevya ili apate pesa.

Uwajibikaji ni suala lililojadiliwa kwa kina sana na Shigongo kupitia riwaya zake. Anaonesha namna serikali kupitia vyombo vyake vya dola isivyowajibika, watu wenye pesa wanatumia vyombo hivi kwa manufaa yao binafsi huku vikiwagandamiza wanyonge. Kwa mfano, kitendo cha wahusika Mohamed Azray na Gedion kutetewa na vyombo vya dola bila kufanya uchunguzi juu ya tuhuma zinazotolewa dhidi yao inaonesha kutowajibika ipasavyo kwa vyombo hivi.

### 4.3 Tofauti za kimtindo Kati ya MSA na Shigongo

MSA na Shigongo wametofautiana kimtindo katika uumbaji wa fani ndani ya riwaya zao kutokana na namna ya utumiaji wa lugha, ujengaji wa taharuki, uumbaji wa wahusika, mtiririko wa matukio, utumiaji wa dhana zinazoashiria sayansi na teknolojia na mandhari katika kuwasilisha jambo walilolikusudia kwa hadhira.

#### 4.3.1 Matumizi ya Lugha

MSA ana uhodari mwingi katika kutumia lugha, na uhodari huu ndio umempa umaarufu hasa katika upande wa riwaya pendwa hata kuitwa baba wa riwaya pendwa. Kwa mfano aelezapo wasifu wa Bwana Ali, “tumbo lake lililokuwa

likimpinga kwa kufura kwake lilikuwa likimkera…kwa kuchururika kila wakati kwa kelele" (uk: 7). Matumizi ya misemo, vitendawili na methali pia yanadhihirisha umahiri wake katika kutumia lugha. Kwa mfano anaposema:

> Ukitaka kujua asili ya mwangaza, ingia kizani au ukitaka kujua raha ya mtu aliyesoma tazama taabu ya mtu asiyesoma (uk: 3).
> 'Popoo mbili zavuka mto' (uk: 30).
> …bora kukawia, akafika, kuliko kulala…njiani (uk: 6).

Yapo pia matumizi ya maneno ya Kiarabu hapa na pale (Kwa mfano ukurasa wa 4, 22, 24 na kadhalika). Matumizi ya lafudhi ya Kiarabu na Kihindi yametumika kuonesha msisitizo wa aina na asili ya wahusika aliowatumia mwandishi. Kwa mfano anaposema: "Baniani, hali amejikaza, akajibu, "Yeye marudi jia iyo iyo Rashta" (uk: 63).

MSA pia ametumia tamathali za usemi katika riwaya yake ya *Mzimu wa Watu wa Kale.* Kwa mfano: ukurasa wa 3, weusi wa Bwana Msa unafananishwa na masizi, ukurasa wa 25, kiza ndani ya Muzimu wa watu wa kale kinafananishwa na uwanda wa ahera. Ukurasa wa 29, mwendo wa Bwana Msa na Najumu unafananishwa na mwendo wa kaa. Ametumia pia sitiari (uk: 2), na balagha (uk: 24).

Tamathali hizi zimetumika ili kujenga maudhui ya riwaya hii kwa kutupa taswira ya hali mbalimbali kwa njia inayomvuta msomaji.

MSA pia anatofautiana na Shigongo katika uteuzi wa msamiati. MSA tumeona kwamba anatumia msamiati mgumu. Kwa maana ya maneno ambayo kimsingi hayajazoeleka kutumika katika matumizi ya lugha ya kila siku katika lugha ya Kiswahili.

Kwa upande wa Shigongo ni tofauti, kwani ametumia lugha ya kawaida iliyo na uhaba wa matumizi ya lugha kama tamathali za semi, nahau na taswira. Hata hivyo Shigongo anachanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Hutumia Kiingereza hasa pale kunapotokea mazungumzo baina ya wageni kutoka nchi za ughaibuni,

wanafunzi wa vyuo vikuu, madaktari na jamii ya wasomi ambao wanahusiana na masuala ya kimataifa. Kwa mfano, mwandishi anasema: *"I have called to apologize, 'cause I wont be there for your birthday party! I love you, dad, with all my heart. Wish you all the best! Lots of love from Alice as well!"* (uk: 68).

(Tafsiri )

(Nimekupigia kuomba msamaha, kwa sababu sitakuwepo kwenye sherehe yako ya kuzaliwa! Nakupenda baba, kwa moyo wangu wote na ninakutakia kila la kheri. Alice pia anakusalimia)

**4.3.2 Ujenzi wa Taharuki**

Taharuki imetumiwa na waandishi wote wawili kumfanya msomaji aendelee kuvutiwa na usomaji huku akiwa na matumaini ya kutokea kwa tukio la kusisimua huko mbeleni. Kwa mfano, katika *Kifo ni Haki Yangu* taharuki inajengwa kupitia mhusika Camilla jinsi anavyoendelea kumuua kila mwanaume aliyewahi kumsaliti ama kumtendea ubaya kimapenzi.

Katika *Mzimu wa Watu wa kale* taharuki imejengwa kupitia mhusika Bwana Ali hasa baada ya maiti yake kupatikana ikiwa haina kichwa huku imepakatishwa boga. Hapa mwandishi ametumia taharuki kwa namna ya pekee ikilinganishwa na riwaya ya *Kifo ni Haki Yangu.* Hii ni kutokana na tofauti za msuko wa matukio ndani ya riwaya hizi. Mwandishi wa *Mzimu wa Watu wa Kale na Kosa la Bwana Msa* anamchora mhusika mkuu Bwana Msa kiasi cha kufikiriwa kuwa ni jini kwani mauaji na upelelezi vinafanyika kwa kificho kiasi cha kujenga taharuki kubwa kwa msonaji. Tofauti na mwandishi wa *Kifo ni Haki Yangu* na *Damu na Machozi* ambaye pamoja na kutumia taharuki matukio ya mauaji yanafanyika kwa wazi zaidi na ni rahisi kwa msomaji kuelewa aliyefanya uhalifu huo. Tofauti hizi zinajitokeza kwa sababu ya wakati, kawaida fasihi husawiri mambo yanayojitokeza katika jamii. Kipindi cha

nyuma matukio ya mauaji hayakujitokeza kwa wingi kama sasa. Ndio maana mauaji katika kazi za MSA hayajaonekana kwa uwazi sana na hata yalivyojitokeza ni kwa kificho. Tofauti na katika kazi za Shigongo ambapo mauaji ni mengi na ni ya wazi zaidi. Hii ina maana kuwa jamii ya sasa ni tofauti na jamii ya zamani, mauaji katika jamii yamekuwa ni kitu cha kawaida. Hivyo hata fasihi ya sasa inaendana na mabadiliko yanayojitokeza ndani ya jamii ya sasa.

### 4.3.3 Uumbaji wa Wahusika

Uumbaji wa wahusika wakuu katika kazi za MSA na Shigongo unatofautiana. Katika riwaya za MSA mhusika mkuu anajirudia, yaani anamtumia mhusika Bwana Msa ambaye ni mpelelezi wa kujitegemea katika kazi zake zote. Tofauti na Shigongo ambaye anatumia majina tofauti kuumba wahusika wake wakuu.

Tofauti nyingine ni kwamba, wahusika katika kazi za Shigongo mara nyingi ni wakwezwa kwa sababu wamepewa uwezo usio wa kawaida, na hawabadiliki kimsimamo toka mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Kwa mfano, katika *Kifo ni Haki Yangu*, Camilla ni katili. Anafanya mauaji ya watu 521, anauwa pasipo huruma mpaka alipokamatwa na kufungwa maisha. Camilla amepewa uwezo wa kufanya mambo makubwa ambayo kwa hali ya kibinadamu ni vigumu kuyatenda. Kwa mfano, kuua watu wengi katika mikoa tofauti nchini Tanzania bila kukamatwa, kubakwa na kulawitiwa na wanaume zaidi ya mmoja akiwa mtoto mdogo na kuweza kutembea kwa miguu masafa marefu, na pia alikuwa na magonjwa ya zinaa aliyoambukizwa na kipigo juu. Shigongo anasema:

> Wote wawili wakatii amri hiyo. Walimweka Camilla katikati yao, bila kujali alikuwa mtoto mdogo kiasi gani, wakaanza kumwingilia kwa zamu (uk: 9).
> Watoto wale hawakujali ugonjwa aliokuwa nao Camilla. Walimwingilia kila siku bila huruma, tena usiku na mchana (uk: 13).

Pia kitendo cha mhusika Gedion na wenzake kujaza madawa ya kulevya katika matumbo ya watoto wadogo Everine na Evarist kisha kuwazika wakiwa na hali mbaya ni kitendo ambacho si cha kawaida katika hali ya kawaida. Kwani katika hali ya kawaida isingekuwa rahisi kwa Evarist kupona katika tukio kama hilo. Aidha, kitendo cha Evarist akiwa haoni kuachwa katika msitu wa Mahands na kina Karl Peters na wenzake, pori ambalo lilijaa wanyama wakali na binadamu hawakuruhusiwa kuingia pia ni tukio ambalo katika hali ya kawaida ni jambo la kushangaza. Mwandishi anasema:

> … baada ya wanyama wengi kuzaliana, hasa wale wakali kama samba, chui, pamoja na nyoka wa kila aina kama koboko, chatu na wengine, serikali ikapiga marufuku kwa mtu yeyote kuingia kwenye msitu huo kufuatia matukio ya watu wengi kuuawa na wanyama (uk: 330).

Madumulla (2009) anadai kuwa wahusika wakwezwa huchorwa kwa lengo la kuwa kielelezo na watetezi wa haki dhidi ya unyanyasaji na uonevu. Ingawa kwa utetezi wa Camilla unaweza kuwa ni kinyume na haki za binadamu kwa kuwa anaua binadamu.

Katika kazi za MSA wahusika hawajakwezwa sana kwa sababu mpelelezi wa kujitegemea Bwana Msa anatimiza wajibu wake kama mpelelezi japo ametumia udadisi na akili nyingi hadi kumpata mhalifu. Matendo yanayofanyika hapa si ya kuajabia sana kama ilivyo katika kazi za Shigongo. Hii inaonesha wazi kuwa maisha ya zama hizi yana matukio mengi ambayo si ya kawaida katika maisha ya binadamu kuliko yalivyokuwa zama zilizopita. Kwa mfano zama zilizopita jamii hazikuwa na matendo maovu kama ubakaji, utumiaji wa madawa ya kulevya, mauaji na uovu mwingine mwingi kama ilivyo katika jamii ya sasa, ndio maana hata kazi za fasihi zinatofautiana kulingana na wakati.

### 4.3.4 Utumiaji wa Dhana za Kisayansi na Teknolojia

Kutokana na uchambuzi uliofanywa wa kazi za riwaya ya upelelezi za MSA na Shigongo, imebainika wazi kuwa kuna tofauti katika mtindo wa utumiaji dhana zinazoashiria sayansi na teknolojia. Mwandishi wa riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* na *Kosa la Bwana Msa* hajabainisha wazi dhana za kisanyansi kama ilivyo kwa mwandishi wa *Kifo ni Haki yangu* na *Damu na Machozi*. Hii ni kutokana na ukweli kwamba miaka ya 1960 wakati MSA anaanza kuandika riwaya zake hapakuwa na matumizi ya huduma, vifaa na bidhaa zitokanazo na maendeleo ya sayansi na teknolojia kama ilivyo sasa. Riwaya nyingi za Shigongo zinatumia dhana za kisayansi na teknolojia kwa sababu wakati huu kwa mfano, TEHAMA imeshamiri ulimwenguni kote. Vifaa kama simu, TV, Redio, kompyuta, DVD, CD, vinyonyeo na wavuti hutumika katika suala zima la mawasiliano baina ya watu tofauti na zamani.

Vita na machafuko baina ya mataifa, nchi na nchi, kabila moja na jingine vinapelekea katika utengenezaji wa silaha mbalimbali. Ongezeko la uharibifu wa mazingira linachangia ongezeko la magonjwa baina ya watu na hivyo kuchangia utengenezaji wa madawa kwa ajili ya binadamu. Japokuwa baadhi ya madawa yanatumika vibaya na hivyo kuleta madhara kwa binadamu, kwa mfano, madawa kama cocaine kutokana na kutumiwa vibaya yameleta madhara makubwa kwa vijana ndani ya jamii.

Kwa jumla dhana nyingi za kisanyansi zinazojitokeza katika riwaya za Shigongo zinaonesha namna utandawazi ulivyoenea duniani tofauti na zamani ambapo kazi za *Mzimu wa Watu wa Kale* na *Kosa la Bwana Msa* zilipoandikwa.

### 4.3.5 Mtiririko wa Matukio

Mtiririko wa matukio unatofautiana katika riwaya za MSA na Shigongo kwani, MSA anatoa maelezo juu ya aliyefanya kosa kwa kificho kiasi kwamba msomaji asipokuwa makini si rahisi kubaini ni nani aliyetenda kosa hilo. Tofauti na Shigongo ambaye tangu mwanzo wa hadithi mkosaji hujulikana kwa urahisi. Tofauti inayojitokeza hapa ni kwamba MSA anjitahidi kufuata kanuni za uandishi wa riwaya pendwa, mojawapo ya kanuni zikiwa ni kutoa taarifa kidogo kidogo pamoja na msomaji kupewa upeo wa kufikiri mkubwa kuliko mhusika bwege.

### *4.3.6 Uumbaji wa Mandhari*

Mandhari katika riwaya za upelelezi za MSA inatofautiana na ile ya riwaya za upelelezi za Shigongo. MSA hutumia mandhari ya Tanzania hususani Zanzibar na viunga vyake wakati Shigongo hupendelea kutumia mandhari changamano, yaani nchi ya Tanzania pamoja na nje ya nchi. Kwa mfano, matumizi ya nchi kama Misri katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu*, Pakistani katika *Damu na Machozi* Marekani katika *Kifo ni Haki Yangu* kwa kuzitaja chache.

### *4.3.7 Uwasilishaji wa Dhamira*

Fasihi kama kioo cha jamii huakisi mambo yanayojitokeza katika jamii ambayo mwandishi anaandikia. Waandishi wa zama hizi na hata zama zilizopita wanaandika kazi zao kutegemeana na mambo yanayojitokeza katika jamii japo wanatofautiana namna ya uwasilishaji. MSA na Shigongo wanatofautiana kuwasilisha dhamira zao kama ifuatavyo:

#### *4.3.7.1 Dhana ya Mapenzi na Ngono*

MSA anaijadili dhana ya mapenzi na ngono kwa staha, na ametumia lugha ya picha yenye mvuto. Kwa mfano anaposema: "…, akaja Bwana Ali aliyekuwa mmoja

katika wale watu waliokuwa wakimtazama Kipwerere siku zile kwa jicho la matamanio …" (uk: 9).

Hii ni kwa sababu zama zilizopita suala la ngono na mapenzi halikujadiliwa waziwazi kuepuka kwenda kinyume na maadili ya jamii.

Katika kujadili dhana ya ngono na mapenzi Shigongo anaonesha tofauti zaidi kwa kutamka waziwazi maneno ambayo hapo awali yasingeweza kutamkwa kwa kuhofia maadili katika jamii. Kwa mfano anaposema:

> …, ndipo Camilla alipoamua kutimiza lengo lake la kuweka kumbukumbu ya mzee Msangi kwa kuukata uume wake na kuondoka nao. … Anastahili kifo hiki! … Lazima uume wake niubanike kabla sijaondoka nao hapa!" ( uk: 83).

Hii inaonesha ni namna gani fasihi ya zama hizi inavyosawiri maisha ya sasa. Kwani maadili katika jamii yamemong'onyoka tofauti na zamani. Vitendo vya ubakaji kwa mfano vimekuwa ni jambo la kawaida tofauti na zamani. Kwa mfano, kupitia wahusika Camilla na Mzee Msangi Shigongo anasema:

> "… Mimi ni sawa na mjuukuu wako lakini umeniharibu vibaya sehemu zangu za siri na sijui kama kuna mwanaume atakayetaka kunioa"
> "Hayo si masuala yangu! Lala chali" Mzee Msangi alisema hayo kwa ukali, akimsukuma Camilla kitandani na kumwingilia tena. Hakumfanyia kama kawaida ya watu wengine wanavyofanyiwa katika tendo la ndoa (uk: 4).

Dondoo hizi zinaonesha namna mapenzi na ngono yanavyojadiliwa kwa uwazi zaidi na waandishi wa zama hizi kuliko zama zilizopita. Hii ni kwa sababu maadili katika jamii ya sasa yamemomonyonyoka zaidi kuliko zamani.

#### 4.3.7.2 Malezi

MSA anaonesha wazi jamii ya zama zilizopita ilivyolichukulia umuhimu suala la malezi ya watoto. Kwa kumtumia mhusika Bwana Ali na mkewe Kipwerere, ameonesha namna alivyomlea Ahmed kama mwanae japo anataka kumkata urithi na

kuuza mali yake yote. Hii ni kwa sababu jamii ya zamani ilithamini utu wa mtu tofauti na sasa.

Kwa upande wa Shigongo amezungumzia kwa jumla mambo yanayoizunguka jamii ya leo. Kuhusu suala la malezi ya watoto, anaona malezi ya watoto ni jukumu la wazazi wote wawili na jamii kwa ujumla. Mfano anafafanua kwa kumtumia mhusika Camilla ambaye anafiwa na mama yake pasipo kumjua baba yake na kupelekwa kituo cha kulelea watoto. Mwandishi anasema; "Mama yangu hakuweza kuiona siku iliyofuata. Hakutoka katika chumba cha upasuaji akiwa hai,..." (uk: 2). Hapa mwandishi anataka kutujuza kuwa mtoto Camilla angelelewa na wazazi wake asingekutwa na masahibu yaliyompata maishani mwake. Hata Mzee Msangi baada ya kumchukua kituo cha kulelea watoto na kutimiza wajibu wake kama mzazi bado Camilla angekua vizuri. Hapa mwandishi anaonesha namna jamii ya sasa ilivyokosa utu na uaminifu tofauti na jamii ya zamani. Hili limechangia masahibu yote yaliyomkuta Camilla.

Mbali na hilo mwandishi pia anaionya jamii kuhusu kuwalea yatima. Hasa wale wanaochukua jukumu la kuasilisha watoto kutoka katika vituo vya kulelea watoto. Anaonesha namna wanaoasilisha watoto wanavyoweza kuwaharibu watoto hao. Mfano mwandishi anasema:

> Pamoja na ukatili aliofanyiwa na Mzee Msangi, Camilla hakuwa na mahali pengine pa kwenda ... Ukatili wa Mzee Msangi ulimchosha. Hakutaka tena kuwa mtumwa wa ngono, kazi aliyoifanya kwa miaka kumi (uk: 4).

**4.3.7.3 Nafasi ya Mwanamke**

MSA anamchora mwanamke kama pambo kwa wanaume, anayetegemea kuolewa ili kuendesha maisha na asiye na sauti kwa mumewe. Kwa mfano, Kipwerere pamoja

na tatizo alilokuwa nalo alisubiri ruhusa ya mumewe kupewa ng'ombe kwa ajili ya matibabu.

Shigongo kwa upande wake, anamchora mwanamke kama mtu anayepambana na ugandamizaji wa wanaume. Japokuwa pia anamchora kama chombo cha starehe. Kwa kumtumia mhusika Camilla anaonesha namna alivyoamua kupambana na wanaume waliomtesa kwa kuwakata uume wanaume 521 na kuwaua. Japokuwa halikuwa suluhisho sahihi lakini lengo la mwandishi lilikuwa kuonesha ujasili wa mwanamke katika kutetea haki yake. Hii ni kutokana na mabadiliko yaliyopo katika jamii ya sasa, mwanamke ana uhuru zaidi kuliko zama zilizopita ndio maana hata Camilla ameweza kuwaadhibu wanaume waliomuonea.

#### 4.3.7.4 Suala la Dini

Shigongo anaona dini haiwezi kumsaidia mwanadamu, anafikiri mwanadamu anao uhuru wa kutenda anavyofikiri si kwa sababu ya dini. Kwani hata viongozi wa dini si mifano mizuri kwa jamii inayowazunguka. Mwandishi anasema:

> … Padri William, au Dk. William kama alivyoitwa na wengi, alikuwa shoga na aliianza tabia hii akiwa na umri wa miaka kumi na mitano nchini kwao Uingereza (uk: 29).
> Camilla hakuyaamini macho yake alipomwona Padri Petro akimwingilia kimwili… (uk: 33).

Dondoo hizi zinazonesha namna watumishi wa Mungu wasivyo waaminifu na wanafanya kinyume na mafundisho wanayotoa.

MSA kwa upande mwingine, anaamini katika mizimu na uganga. Hapa mwandishi anataka kutuonesha namna jamii ya zamani ilivyothamini miungu na uganga. Anaonesha namna Waafrika wanavyoenzi falsafa yao. Kwani kabla ya maajilio ya wakoloni na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia Waafrika walitambikia mizimu pindi wapatapo shida mbalimbali. Mwandishi anashadidia hili anaposema:

> Mambo yalipokithiri, wazee wake walifika kwa waganga kutazamia, nao kila mmoja alisema lake. Wengine walisema kuwa amerogwa na wachumba waliokuwa wakimtaka wakamkosa. Wengine walisema kuwa amedhurika katika kile kichaka cha 'Mzimu wa Watu wa Kale' … (uk: 10).

Suala la dini limejadiliwa na waandishi hawa kwa namna tofauti. Hii ni kutokana na wakati, pamoja na mabadiliko yanayojitokeza ndani ya jamii. Zamani Waafrika waliitegemea miungu na mizimu katika kutatua shida mbalimbali. Ndiyo maana hata kazi za fasihi za wakati huo zinajadili masuala yanayohusu mizimu na miungu. Tofauti na jamii za sasa zinafuata dini zilizoletwa na wageni. Hata fasihi ya sasa inaonesha matokeo ya dini zilizoletwa na wageni hao.

### 4.4 Sababu za Kutofautiana Kimtindo Kati ya MSA na Shigongo

MSA na Shigongo wametofautiana kimtindo katika uumbaji wa fani ndani ya riwaya zao, hii ni kutokana na sababu za msingi zifuatazo:

#### 4.4.1 Athari za Wakati

Waandishi MSA na Shigongo wameandika kazi zao katika vipindi tofauti. Suala la utumizi wa lugha kwa mfano, limeathiriwa na wakati. Shigongo katika kazi zake anaonesha wazi namna jamii ya sasa ilivyoathiriwa na usasa (Uzungu), na mwingiliano wa mataifa ya nje ulivyo mkubwa kuliko zamani. Pia watunzi wa kazi za fasihi sasa wana uhuru mkubwa katika kusana kazi zao, kwani hawafungwi na sheria zozote ndio maana ni rahisi kusana kazi zao kwa namna wapendavyo. Tofauti na waandishi wa zamani ambao waliongozwa na kanuni katika kuandika kazi za fasihi, kwa mfano MSA katika uandishi wa kazi zake anatumia kanuni na umakini mkubwa katika kusana kazi zake tofauti na sasa watunzi hawana muda wa kukaa na kufikiria maneno magumu badala yake hutumia lugha ya kawaida ya mawasiliano.

Suala la dini limejadiliwa na waandishi hawa kwa namna tofauti. Hii ni kutokana na wakati, pamoja na mabadiliko yanayojitokeza ndani ya jamii. Zamani Waafrika waliitegemea miungu na mizimu katika kutatua shida mbalimbali. Ndiyo maana hata kazi za fasihi za wakati huo zinaonesha mambo yanayohusiana na miungu na mizimu. Kwa mfano, suala la kutambikia mizimu katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*. Tofauti na jamii za sasa zinafuata dini zilizoletwa na wageni, hata fasihi ya sasa inaonesha matokeo ya dini hizo, kwa mfano, kutawala kwa dini ya Kikristo katika riwaya za Shigongo na Uislamu katika riwaya za MSA.

### 4.4.2 Athari za Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia

Maendeleo ya sayansi na teknolojia yamesababisha mabadiliko makubwa katika fasihi. Uumbaji wa dhamira, mandhari na wahusika katika kazi ya fasihi huweza kuathiriwa na maendeleo haya. Kwa mfano, uwepo wa maendeleo ya sayansi na teknolojia umesababisha uwepo wa dhamira ya mauaji ya kutumia silaha za moto kama bunduki na mabomu katika riwaya za shigongo tofauti na MSA mauaji yanafanyika kwa kutumia jambia, silaha ambayo ni ya zamani tofauti na bunduki na bomu. Hii inasababisha ongezeko la mauaji ndani ya jamii tofauti na zamani.

Mandhari pia inatofautiana kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Mwandishi Shigongo katika riwaya zake ameweza kutumia mandhari ya nchi za nje kwa sababu ya uvumbuzi wa vyombo vingi vya usafiri kama ndege, ambavyo vinamrahisisishia mtu kusafiri nchi mbalimbali na kwa wakati mfupi. Tofauti na kazi za MSA mandhari inazungukia Tanzania hususani Zanzibar na viunga vyake.

Vile vile maendeleo ya sayansi na teknolojia yameleta mabadilko katika uteuzi wa zana za kiisimu. Kwa mfano, katika riwaya za MSA hakuna matumizi makubwa ya dhana zinazoashiria usayansi, hii ni kutokana na ukweli kuwa wakati anaandika riwaya zake hapakuwepo na maendeleo makubwa ya kisayansi na teknolojia na

hivyo misamiati kama hiyo haikutumika. Tofauti na wakati Shigongo anaandika riwaya zake kulikuwepo na maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia hivyo msamiati mwingi ulioashiria dhana za kisayansi kutumika.

### 4.4.3 Athari za Mmomonyoko wa Maadili

Katika riwaya za Shigongo suala la ngono limejadiliwa kwa uwazi sana, watoto, wanawake wanabakwa bila msaada kutoka katika jamii inayowazunguka. Hata asasi za dini ambazo ndilo tegemeo la binadamu kwa kiasi kikubwa zinaenda kinyume. Kwa mfano, mwandishi anawatumia Mzee Msangi, Padri Petro na Padri William kubainisha kuwa maadili ndani ya jamii yetu yamemomonyoka. Kwani Padri Petro anambaka Camilla baada ya kumnywesha madawa ya kulevya na Padri William anafanya mapenzi kinyume cha maumbile na dreva wake. Mzee Msangi anambaka Camilla akiwa bado mtoo mdogo sawa na mjukuu wake.

Hii inaonesha wazi kuwa maisha ya zama hizi yana matukio mengi ambayo si ya kawaida katika maisha ya binadamu kuliko yalivyokuwa zama zilizopita. Kwa mfano zama zilizopita jamii hazikuwa na matendo maovu kama ubakaji, utumiaji wa madawa ya kulevya, mauaji na uovu mwingine mwingi kama ilivyo katika jamii ya sasa, ndio maana hata kazi za fasihi zinatofautiana kulingana na matukio yanayojitokeza ndani ya jamii.

Shigongo na MSA wametofautiana katika matumizi ya kejeli. Shigongo anatumia kejeli na dhihaka ili kukosoa jamii, zikiwemo asasi za dini pamoja na Serikali. Kwa mfano, anawatumia wahusika Padri Petro na Padri William ambao wanategemewa na jamii lakini wanafanya maovu yasiyotegemewa. Hii ni kejeli kwa sababu watu ambao wanaaminiwa na kundi kubwa wanafanya maovu chini ya mwamvuli wa dini. Hapa mwandishi anaifundisha jamii kuwa uamuzi wa mtu kuamua lipi afanye na lipi asifanye lipo ndani ya mtu mwenyewe. Kwa mfano, anasema:

> "Sijui nitakushukuru vipi, Padri Petro!"
> "Kwa nini?"
> "Umenisaidiasana kupona ugonjwa wangu"
> "Usijali, kusaidia watu ni kazi yangu. Namwakilisha Mungu duniani!" (uk: 20).

Pia kitendo cha Jeshi la Polisi kumtafuta Camilla bila mafanikio huku akiendelea kuua mamia ya watu bado ni kejeli kwa Serikali. Wakati mwingine aliwachenga kwa kujifanya jini na wao wasing'amue. Mwandishi anasema: "Pamoja na kuwa na silaha askari na wanajeshi waliogopa jini na kutimua mbio" (uk: 229). Hapa mwandishi anaonesha watu wenye vyeo na nafasi serikalini wasivyotimiza wajibu wao. Kwa upande wa MSA anatumia kejeli na dhihaka kama mbinu inayomrahisishia kazi yake ya upelelezi hasa anapoongea na boi wa Baniani. Mwandisi anasema: "Akageuza sauti yake akaifanya ya kitoto, "Aa! Unatutisha wenzio hivyo! Hatukufanya kitu, sisi tunacheza na wewe tu; ngojea nikakuchongee kwa mama. Mama'ngu mkali we!" (uk: 45).

### 4.4.4 Athari za Kimazingira

MSA katika kazi zake za *Mzimu wa Watu wa Kale* na *Kosa la Bwana Msa* ametumia taharuki kiasi ikilinganishwa na riwaya za Shigongo za *Kifo ni Haki Yangu na Damu na Machozi.* Hii ni kutokana na mauaji mengi kutokea katika riwaya za *Kifo ni Haki Yangu* na *Damu na Machozi* ukilinganisha na *Mzimu wa Watu wa Kale na Kosa la Bwana Msa.* Tofauti hizi zinajitokeza kwa sababu ya athari za kimazingira na wakati pia, kawaida fasihi husawiri mambo yanayojitokeza katika jamii. Kipindi cha nyuma matukio ya mauaji hayakujitokeza kwa wingi kama sasa. Ndio maana mauaji katika *Mzimu wa Watu wa Kale na Kosa la Bwana Msa* hayajaonekana sana na hata yalivyojitokeza ni kwa kificho. Tofauti na katika *Kifo ni Haki Yangu* na *Damu na Machozi* ambapo mauaji ni mengi na ni ya wazi zaidi. Hii ina maana kuwa jamii ya sasa ni tofauti na jamii ya zamani, mauaji katika jamii

yamekuwa ni kitu cha kawaida. Hivyo hata fasihi ya sasa inaendana na mabadiliko yanayojitokeza ndani ya jamii ya sasa.

**4.5 Waandishi Walioathiri Uumbaji wa Fani Katika Kazi za MSA**

Katika uumbaji wa wahusika MSA ameathiriwa na waandishi wa nje na ndani ya nchi kwa mfano, utoaji wa majina ya wahusika wakuu yanayojirudia ameathiriwa na mwandishi na mwanahabari wa Kiingereza Ian Fleming ambaye katika riwaya zake pamoja na hadithi fupi alizowahi kuandika katika uandishi wake (1953 – 1964), mara zote amemtumia mhusika mkuu James Bond ambaye anamchora kama shujaa. Mfano wa kazi zake ni kama; *Casino Royale (1953), Live and Let Die (1954), Diamonds are Forever (1956), na The Man with The Golden Gun* (1965) kwa kuzitaja chache. Ndani ya nchi ameathiriwa na waandishi kama Elvis Msiba ambaye katika kazi zake zote amemtumia mhusika Willy Gamba ambaye ni mpelelezi machachari. Mfano wa vitabu vyake ni kama; *Njama, Hujuma, Kikomo na Kikosi cha Kisasi* kwa kuvitaja vichache. Pia ameathiriwa na mwandishi Ben Mtobwa ambaye naye katika kazi zake hupendelea kumtumia mhusika Joram Kiango kama mhusika mkuu. Kwa mfano, katika riwaya ya *Roho ya Paka, Salamu Toka Kuzimu, Zawadi ya Ushindi, Malaika wa Shetani, Najisikia Kuua Tena na Tutarudi na Roho Zetu* kwa kuzitaja chache.

Athari za waandishi hawa haziishii katika uumbaji wa wahusika peke yake bali hata katika ujenzi wa taharuki kwa msomaji. Taharuki inayojitokeza katika kazi za Ian Fleming, Elvis Msiba na Ben Mtobwa ni sawa na ile inayojitokeza katika kazi za MSA. Kwa mfano, si rahisi kutabiri ushindi kwa mhusika James Bond, Willy Gamba na Joram Kiango anapokabiliwa na kundi la maadui. Namna anavyopambana na kujiokoa huleta utata kiasi cha msomaji kushindwa kuelewa nini kilichotokea kama ilivyo kwa mhusika Bwana Msa katika kazi zote za MSA.

### 4.6 Waandishi Walioathiri Uumbaji wa Fani Katika Kazi za Shigongo

Kimsingi kazi za Shigongo zimeathiriwa na waandishi wakongwe wengi wakiwemo wa nje ya nchi na ndani ya nchi katika suala zima la uumbaji wa fani. Katika uumbaji wa mandhari kwa mfano, Shigongo ameweza kutumia mazingira ya kitaswira, majina ya nchi kama Pakistani, Irani, Misri, Afrika ya Kusini, China, Australia, India na Amerika katika riwaya alizowahi kuandika. Nchi ambazo kimsingi mwandishi anaweza kuwa hajawahi kuziona kwa kuzitembelea. Hii ni kutokana na ukweli kwamba mwandishi ameweza kusoma na kuyaelewa mazingira ya mandhari hayo kupitia wavuti. Kwa mfano, katika riwaya ya *Rais Anampenda Mke Wangu*; mwandishi ametumia mandhari ya Misri na nchi ya kitaswira (Sokomoni) ambayo inaweza kufananishwa na Tanzania. Katika riwaya ya *Kifo ni Haki Yangu;* mwandishi ametumia mandhari ya Amerika. Katika riwaya ya *Kutoka China na Penzi la Kweli* ametumia mandhari ya China, pengine hii inajitokeza kutokana na ukweli kwamba suala la bidhaa za China kutawala Tanzania linajitokeza. Pia katika riwaya ya *Damu na Machozi* ametumia mandhari ya Pakistani kwa kuzitaja chache. Mtindo huu wa kutumia mandhari ya kubuni na nchi ambazo ni ngeni ameathiriwa na mwandishi wa Kijerumani Karl May (1842 – 1912) ambaye naye katika uandishi wake aliweza kuelezea mazingira ya nchi za kigeni kwa ufanisi bila kuwahi kuzitembelea nchi hizo isipokuwa kwa kusoma habari zinazohusiana na mazingira ya nchi hizo.

Uumbaji wa wahusika wakwezwa katika kazi za Shigongo umeathiriwa na baadhi ya waandishi kama Elvis Musiba na Faraji Katalambula ambao anawaita ‘wazee wetu’. Hii ni kutokana na ukweli kuwa wahusika hawa hupewa uwezo wa kufanya matendo yasiyowezekana kwa binadamu wa kawaida. Kwa mfano, mhusika Willy Gamba kupigana na majasusi zaidi ya mia yaliyosomea ukomandoo akiwa peke yake na

mwisho anaibuka mshindi katika riwaya ya *Njama*. Hapa mhusika Camilla katika riwaya ya *Kifo ni Haki Yangu* anafananishwa na mhusika Willy Gamba ambao kimsingi wana fanya matendo ambayo si ya kawaida kwa binadamu wa kawaida.

### 4.7 Hitimisho

Sura hii ikiwa ni uwasilishaji na uchanganuzi wa data, imebainisha tofauti za kimtindo kati ya waandishi MSA na Shigongo katika kuumba fani katika riwaya zao, sababu zinazopelekea kuwepo kwa tofauti hizo kimtindo, pamoja na mifano ya waandishi wanaoathiri uumbaji wa fani katika riwaya za MSA na Shigongo. Sura inayofuata, mtafiti atazungumzia hitimisho la utafiti huu kwa kuelezea muhtasari pamoja na mapendekezo ya utafiti huu.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Utafiti huu umefanyika ili kulinganisha mitindo iliyotumika katika riwaya za upelelezi za MSA na Shigongo. Ili kukamilisha utafiti huu, usomaji na uchambuzi wa kina wa kazi za MSA na Shigongo ulifanyika ili kubaini mitindo waliyoitumia. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani ambao ulikwenda sambamba na usomaji wa vitabu, juzuu, makala na tasnifu mbalimbali zilizohusu mada hii. Sura hii inatoa muhtasari wa tasnifu, inafanya majumuisho ya utafiti huu pamoja na kutoa mapendekezo ya tafiti zijazo kufuatia majumuisho yaliyotolewa.

## 5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Sura ya kwanza imejadili usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, hali kadhalika maswali ya utafiti, umuhimu wa tatizo la utafiti, mawanda ya utafiti pamoja na nadharia ya utafiti vimejadiliwa. Tatizo lililojitokeza na kubainika katika sura hii ni kutokushughulikiwa kwa kazi za MSA na Shigongo kwa pamoja katika kazi moja na hivyo kufanya ulinganisho wa pamoja.

Sura ya pili imejaribu kuonesha kwamba dhana ya mtindo ni tata. Zimekuwa zikitolewa fasili mbalimbali kulingana na mitazamo ya watu mbalimbali. Kwa mfano, (Enkvist (1973), Leech na Short (1981), Senkoro (1982), Mulokozi (1989), Haynes (1995), Kahigi (1997), na Wamitila (2002) kwa kuwataja wachache. Suala hili la mtindo limekuwa likishughulikiwa si tu na wanafasihi bali pia na wanazuoni wengi. Mawazo yao kuhusu mtindo yamefanana au kutofautiana kabisa au kwa kiasi fulani tu.

Pia mapitio mbalimbali ya maandiko juu ya mtindo katika riwaya ya upelelezi ya Kiswahili yamepitiwa na yamejaribu kutoa mwanga juu ya mitazamo yao. S.A Mohamed (1973), Madumulla (2009), na Khamis (2011), ni baadhi ya wale wanaomuona MSA kuwa ni mwandishi anaetumia ubunifu wa hali ya juu katika riwaya zake na hasa namna anavyotumia vipengele vya matumizi ya lugha katika kuleta mvuto kwa wasomaji. Ambapo Reuster Jahn (2008) anamuona Shigongo kama mwandishi anaelenga kubadili mitizamo ya wasomaji wake. Mapengo yaliyojitokeza ni pamoja na kujadiliwa kwa kazi za wanafasihi hawa kwa pekee, na kwamba kazi zilizotangulia zimedondoandondoa tu vipengele vichache katika kazi mbalimbali za MSA na Shigongo.

Sura ya tatu inahusu mbinu na vifaa vya utafiti. Imejaribu kubainisha na kuelezea mbinu na vifaa vilivyotumika katika utafiti huu. Taarifa au data nyingi zimekusanywa maktabani. Mtafiti alizisoma kazi mbili za *Muzimu wa Watu wa Kale* na *Kosa la Bwana Msa* za MSA na *Kifo ni Haki Yangu* na *Machozi na Damu* za Shigongo kwa kuzingatia vipengele vya fani ili kupata mtindo uliokusudiwa na mwandishi. Utafiti ulifanyika katika mikoa ya Mwanza, Dodoma na Dar es Salaam. Maandiko mbalimbali yalisomwa na kuchambuliwa. Maadili na udhibiti wa data ulizingatiwa. Uchambuzi wa data za utafiti huu ulizingatia nadharia ya elimumitindo. Changamoto kubwa aliyokutana nayo mtafiti ni uchache wa maandiko yanayozungumzia suala la mtindo ikilinganishwa na masuala mengine katika jamii, pia maandiko yanayozungumzia kazi za Shigongo.

Sura ya nne ambayo hasa ndicho kiini cha utafiti huu imejaribu kuonesha yaliyojadiliwa na kutoa matokeo ya mjadala huo. Mambo makuu matatu yanayoakisi maswali yaliyouongoza utafiti huu kwa jumla yamejadiliwa. Mambo hayo ni: namna waandishi MSA na Shigongo walivyotofautiana kimtindo katika riwaya zao, sababu

zilizochangia kutofautiana kimtindo, pamoja na waandishi wengine wanaoathiri mitindo ya uandishi ya waandishi hawa. MSA anapendelea kutumia maneno magumu ambayo hayajazoeleka katika matumizi ya kawaida, ujenzi wa taharuki katika kazi zake ni wa hali ya juu kiasi cha kumfanya msomji ashindwe kuelewa nini kinachoendelea, wahusika wake wakuu wameumbwa kuchukua majukumu ambayo binadamu anaweza akafanya japokuwa wamepewa akili na udadisi mkubwa, na katika kutumia lugha hatumii maneno mengi yanayoonesha usayansi. Ilihali Shigongo anapendelea kutumia maneno rahisi ambayo yanatumika katika matumizi ya lugha kila siku, ujenzi wa taharuki ni wa kawaida unaomfanya msomaji aendelee kusoma kazi zake japo si wa kumfanya msomaji ashindwe kuelewa nani kafanya nini, ujenzi wa wahusika wakuu katika kazi zake unawakweza sana kwani wanafanya matendo ambayo si rahisi kufanywa na binadamu katika hali halisi, anatumia maneno mengi yanayoashiria dhana za kisayansi na teknolojia. Jambo kubwa linalowafanya wafanane ni maudhui inayojadiliwa inagusa jamii inayoandikiwa.

## 5.2 Utoshelevu wa Nadharia

Nadharia ya elimumitindo imejaribu kwa kiasi kikubwa kutosheleza mahitaji ya tasnifu hii. Kazi teule za riwaya ya *Muzimu wa Watu wa Kale*, *Kosa la Bwana Msa, Kifo ni Haki Yangu* na *Damu na Machozi* zimesomwa kwa makini na kwa undani kisha kuangalia namna waandishi walivyotumia ubunifu wa lugha kwa namna tofauti kama ambavyo nadharia inasisitiza ili kuweza kuvipambanua vipengele vya lugha na kuvielezea. Maana ambazo ni fiche zimefichuliwa. Kwa mfano, neno muzimu linaloipamba kazi ya *Muzimu wa Watu wa Kale* limebeba maana fiche. Muzimu kwa maana ya MSA ni mahala walipofia wageni saba kwa pamoja, na ambapo baadaye

watu wakapajengea hofu ambayo waliishika na kuisadiki miaka nenda rudi katika maisha yao.

Pamoja na mambo mengine nadharia ya elimumitindo imekidhi mahitaji ya utafiti huu pale inaposisitiza upekee wa msanii katika kutumia lugha wakati anapoelezea mtiririko wa matukio wahusika, mandhari na dhamira katika kazi ya fasihi. Namna anavyochagua vipengele vya lugha katika kazi nzima; miundo ya tungo, msamiati na matumizi ya tamathali za semi kwa jumla. Msisitizo zaidi ni katika kuangalia ubunifu katika matumizi ya lugha, namna mzungumzaji au mwandishi anavyoteua maneno kutegemeana na wakati, mazingira, na utamaduni wa jamii husika. Kwa mfano, hili linaweza kuthibitishwa kwa kurejelea katika *Muzimu wa Watu wa Kale,* mwandishi anapoelezea wasifu wa mhusika na matukio mbalimbali kwa kutumia lugha iliyosheheni misemo, vitendawili, na tamathali za usemi, mwandishi anasema:

> Kijana yule wa Kiswahili alikuwa kipandikizi cha mtu, mweusi wa rangi, macho mekundu kama pilipili hoho … lakini kidevu chake safi kama yai…lakini hata sauti yake pia ilikuwa kama inatoka kinywani mwa samba (uk.43).
> Ukitaka kujua asili ya mwangaza, ingia kizani au ukitaka kujua raha ya mtu aliyesoma tazama taabu ya mtu asiyesoma (uk: 3).
> 'Popoo mbili zavuka mto' (uk: 30).
> …bora kukawia, akafika, kuliko kulala…njiani (uk: 6).

Pia mwandishi ameweza kuonesha ubunifu wake katika kutumia maneno yanayokaribiana kimaana kuonesha matendo yanayofanyika ndani ya riwaya, mwandishi anasema:

> Ahlan, Najum! Nimekustua au nimekuzindua? Ikiwa nimekustua itakuwa nimekuroga, lakini, ikiwa nimekuzindua, itakuwa nimekuzingua. Bali ilivyokuwa hapo ulipochutama pana zindiko langu, na litayari kumzuga mtu ye yote atakayejitia umbeya, hapana shaka kwamba kutokea kwangu hivi sasa nikasimama mbele yako namna hii, kumekuzingua (uk: 4).

Nukuu hii inaonesha namna gani mwandishi alivyo na ubunifu katika kutumia lugha na kuifanya kazi yake iwe na mvuto kwa wasomaji.

Shigongo pia katika kazi zake ameonesha umahiri mkubwa katika kutumia lugha inayomvuta msomaji. Kwa mfano, matumizi ya rejesta yamepamba kazi zake zote, mwandishi anasema:

> Bibie, eleweka basi!"… "Masela hatujaburudika kwa muda mrefu…
> "Oyaaa! Miwayaa! Miwayaa, washikaji! Shangazi ameongea jambo muhimu sana. Kesho si mbali, tusubiri" (uk: 85).

Shigongo pia ametumia mbinu ya tafsiri na maneno yanayoashiria dhana za kisayansi na teknolojia. Mwandishi anaeleza:

> "Diana, do you love me?" (Diana, unanipenda?)
> "Yes, I do." (Ndiyo, ninakupenda)
> "Don't kill her with my gun! You wii put me into deep problems!" (Usimwuue kwa bunduki yangu! Utaniweka kwenye matatizo makubwa!) (uk. 307).

Maneno kama, TV uk. 71, SMG uk.66 katika Kifo ni Haki Yangu na redio na TV uk.398, Landcruiser uk.381, Toyota chaser uk. 406, SAR na Cocaine uk. 257 ni mifano ya maneno yanayoashiria dhana ya sayansi na teknolojia.

Katika nukuu hizi waandishi wanatuonesha namna wanavyoweza kutumia lugha kwa ubunifu mkubwa kueleza wasifu wa wahusika, mandhari, na mtiririko wenye kuleta mvuto kwa wasomaji.

Kutokana na ufafanuzi huo ni dhahiri kuwa nadharia ya elimumitindo imejitosheleza katika kuongoza utafiti huu.

## 5.3 Mchango Mpya wa Utafiti Huu

Kutokana na matokeo ya utafiti huu tumeona kuwa mtindo katika riwaya ya upelelezi hutofautiana kati ya mwandishi mmoja na mwingine. Mchango mpya wa utafiti huu ni kwamba waandishi chipukizi tusifungwe na kaida za uandishi, jambo la msingi ni kutumia lugha yenye kuonesha ubunifu inayomvutia msomaji na maudhui yenye mantiki inayoangazia matatizo yanayoizunguka jamii unayoiandikia.

## 5.4 Maoni na Mapendekezo

### 5.4.1 Maoni

Kwa kujikita katika data zilizochambuliwa, utafiti huu unatoa maoni yafuatayo:

Kwanza, waandishi hawa, MSA na Shigongo wameonesha mfano mzuri katika kuonesha mitindo tofauti tofauti inayoweza kutumiwa na waandishi wa kazi ya fasihi. Karibu kila kazi ya fasihi inatumia ubunifu wa lugha kwa namna mbalimbali, lakini hawa wameonesha mitindo yao kwa namna ya kipekee kabisa. Wameonesha namna mwandishi anavyoweza kuandika kazi za kifasihi hususani riwaya kwa kuzingatia mikatale iliyowekwa au kwenda kinyume na mikatale hiyo na kuleta mvuto kwa wasomaji. Mtafiti anashauri watu, na hasa tunaojiita wanafasihi kutoridhika kwa kazi zilizokwisha andikwa, nasi yatupasa kujaribu kuandika ili tufikie uwezo kama wa MSA na Shigongo ikiwezekana tuwazidi.

Pili, serikali, watu binafsi na asasi na vyombo mbalimbali vinavyohusika na usimamizi wa uchapishaji wa kazi za fasihi wasiwe vikwazo katika kufikia lengo la kuwa na kazi nyingi za kifasihi na zaidi kuibua vipaji vinavyoibuka kila siku. Kwa kufanya hivyo, wasanii chipukizi watapata moyo wa kuthubutu kuandika.

Tatu, waalimu, wanafunzi na wahadhiri wa fasihi ya Kiswahili hawana budi kuwajengea uwezo wanafunzi wao wa kuthubutu kuandika ili kuwapata akina MSA na Shigongo wengine.

Nne, mtafiti anawashauri waandishi ambao kazi zao zinasomwa wasiridhike kwa kazi walizokwishaandika, bali waendelee kuandika kwa sababu mambo yanayohitajika kuandikwa ni mengi na kamwe hayatakwisha kutokana na kwamba mambo yanazidi kuibuka kila kukicha. Kwa mfano, masuala yanayohusu matumizi mabaya ya silaha yanayosababishwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia, utandawazi, wizi na ujambazi unaosababishwa na kupanda kwa gharama za maisha,

malumbano na mauaji yanayosababishwa na wanasiasa, ambayo yote ni sehemu ya maisha ya kila siku ya mwanadamu.

Tano, mtafiti anawashauri waandishi wakongwe kutoa ushirikiano kwa waandishi chipukizi wa kazi za fasihi wanaohitaji msaada wa kimawazo ili waweze kuandika kazi zinazokubalika katika jamii. Wasijione kwamba wao wanaweza na kuwaacha waandishi chipukiza bila msaada, kwa kufanya hivyo tunaua sanaa hususani fasihi kwa sababu wanazeeka na kufa na bado jamii inahitaji waandishi wapya.

Sita, wanafasihi tuwe na moyo wa kusoma kazi ambazo tayari ni nyingi na ziko katika mazingira yetu. Kupitia kazi hizo, tunapata kuelewa mitazamo ya watu mbalimbali kuhusu mitindo katika kazi za fasihi, ni jambo zuri kufahamu wengine wanawaza nini juu ya mtindo na maana yake kwa jumla. Hii itasaidia kuibua mijadala ya kifasihi, kifalsafa na kiaaluma.

### 5.4.2 Mapendekezo Kuhusu Tafiti Zijazo

Utafiti huu ulijikita katika kulinganisha mtindo katika riwaya ya upelelezi kwa mujibu wa wanafasihi mashuhuri na mahiri: MSA na Shigongo. Mbali na mjadala katika sura iliyotangulia, utafiti huu unapendekeza maeneo zaidi yanayoweza kufanyiwa utafiti zaidi hapo baadaye kama ifuatavyo:

Kwa vile utafiti huu umebainisha tofauti za kimtindo kati ya MSA na Shigongo, utafiti wa baadaye unaweza kubainsha tofauti za kimtindo kati ya MSA na waandishi wengine au Shigongo na waandishi wengine kama zipo na sababu ya tofauti hizo.

Aidha, utafiti wa baadaye unaweza kuchunguza mada hii kupitia wanafasihi wengine hapa hapa Tanzania, au Afrika au kokote kule ulimwenguni ili kupata mawazo na mitazamo mingine mbali na hii tuliyoiona ya tofauti za kimtindo katika riwaya ya upelelezi kati ya MSA na Shigongo.

# MAREJELEO

*Method* Aggassi, J. (1982) *The Detective Novel and Scientific.* Katika wwwhobat.k/2.in.us/…pmethod.htm/ (last visited 16 – 11 – 2013)

Barry, P. (2002) *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory*. 2nd Ed. LSU, London.

Bradford, R. (1997) *Stylistics: The New Critical Idiom.* Routledge, London.

Crystal, D. na Davy, D. (1969) *Investigating English Style.* Longmans, Green and Co. Ltd, London.

Enkvist, N.E. (1973) *Linguistic Stylistics*. The Hague, Mouton.

Gibbe, A. (1980) *Shaaban Robert: Mshairi.* Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Global Publishers. N.d. About us. http://www.globalpublisherstz.com/us/ (last visited 20-05-2013

Gromov, Mikhail D. (2008a) *Swahili Popular Literature in the Recent Years*. *Swahili Forum* 15: 5-13. 2014).

Gromov, Mikhail D. (2008) *Mahojiano na Ben R. Mtobwa*. *Swahili Forum* 15: 135-140.

Hamad, A.K. (2011) *Matumizi ya Lugha Katika Riwaya za Muhamed Said Abdulla*: Makala za Semina za Kumuenzi Muhamed Said Abdulla. Chuo Kikuu cha Elimu Chukwani, Zanzibar.

Haynes, J. (1995) *Style.* Routledge, London.

http://www.globalpublisherstz.com Imetembelewa 07 Aprili 2013 saa 07:05 mchana.

Issa, A. A. (2011) *Taswira ya Mwanamke Katika Kazi za Muhammed Said Abdulla*: Makala za Semina za Kumuenzi Muhammed Said Abdulla, Chuo Kikuu cha Elimu Chukwani, Zanzibar.

Kahigi, K.K. (1997) *Structural and Cohesion Dimensions of Style: A Consideration of Some Swahili Texts in Maw* (1974). Journal of Linguistics and language of Education (New Series), Juzuu 3, uk. 1- 79.

Kamuzora, J.A.F. (2008) *Reaseach Methods for Business and Social Studies*. Mzumbe Book Project, Mzumbe.

Katalambulla, F.H.H. (1966) *Simu ya Kifo*

Khamis, A.M. (2011) *Muhammed Said Abdulla: Mwalimu wa Waandishi Zanzibar*: Makala ya Semina za Kumuenzi Mohammed Said Abdulla. Chuo Kikuu cha Elimu Chukwani, Zanzibar.

Khatibu, M.S. (1986) *Tamathali za Semi za Kiswahili*. Mulika na. 18. TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

____________ (1999) *Tamathali za Semi za Kiswahili* katika Masabo J. na Mdee, J.S. (wah.) (1999). Mulika na. 25, Taasisi ya Uchunguzi waKiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Uk. 76-91.

Kezilahabi, E. (1976) *Riwaya za Upelelezi katika Fasihi ya Kiswahili*. Jarida la Kiswahili.Tol.45/2

___________ (1981) *Ushairi na Nyimbo katika Utamaduni Wetu: Urithi na Utamaduni Wetu.* TPH, Dar es Salaam.

Kothari, C.R. (2004) *Reseach Methodology: Methods and Techniques.* New Age International Publishers, New Delhi.

Lakoff, G na Johnson, M. (1980*) Metaphor We Live By.* University of Chicago Press, Chicago.

Lakoff, G na Turner (1989) *More than Cool Reasons: A Field Guide to Poetic Metaphor*. University of Chicago Press, Chicago.

Leech, G. and Short, M. (1981) *Style in Fiction.* Longman, London.

Madumulla, J. (1988) *Riwaya ya Kiswahili katika Miaka ya Themanini.* Mulika Na.20

Madumulla, J.S. (2009) *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi.* Mture Educational Publishers Ltd, Dar es Salaam.

Mfamau, M. W. (2007) *Ukweli na Uhalisia wa Kazi za Fasihi za Bwana MSA*: Tasnifu ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, Haijachapishwa.

Mgeni, A. (1983) *The Element of Mystery in the Novel of Mohamed Said Abdulla*

Mjawiri, M. M. (2011) *Muhammed Said Abdulla: Jamii, Maisha Yake na Utajiri wa Kazi Zake:* Makala ya Semina za Kumuenzi Muhammed Said Abddulla. Chuo Kikuu cha Elimu Chukwani, Zanzibar.

Mohamed, M. (2006) *Mitindo katika Riwaya za Shaabani Robert.* Kioo cha Lugha, juz 4 uk. 1 – 12.

Muhamed, S.A. (1960) *Mzimu wa Watu wa Kale*. East African Literature Bureau. Dar es Salaam.

____________ (1968) *Kisima cha Giningi*. Evans Brothers Limited, Nairobi.

___________ (1973 )  *Duniani Kuna Watu*. EAPH, Dar es Salaam.

___________ (1984) *Kosa la Bwana Msa*. MASOMO BOOKSHOP. Dar es Salaam.

___________ (1992) *Mwana wa Yungi Hulewa*. EAEP, Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M na Kahigi, K.K. (1979) *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*.THP, Dar es Salam.

Mulokozi, M.M. (1989) *Tanzu za Fasihi Simulizi*. Mulika na. 21 TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Musokile, M. (1992) *Misingi ya Hadithi Fupi.* DUP, Dar es Salaam.

Mwansoko, H.J.M. (1991) *Mitindo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam.

Mwita, M.B (2009) *Uhakiki wa Mtindo na Maudhui katika Baadhi ya Tamthiliya za Penina Mlama.* MULIKA juz 28 uk. 104 – 128.

Nguvu, P. (2007) *Mengi unveils secret of success*. Guardian – IPP media, 27-02-2007.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi ya Kiswahili*. Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Ntarangwi, M. (2004) *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Augustana College, Rock Island.

Omari, S. (2006) *Mitindo katika Nyimbo za Kizazi Kipya.* KISWAHILI, juz 69 uk. 73.

Oriedo, E. (2000) *Fani katika Riwaya za Shaaban Robert Kusadikika, Utu Bora Mkulima na Siku ya Watenzi wote.* Hannington.

Poe, A.E. (mwaka haukutajwa) *Rules of Writing Detective Novel* katika http://www.detnovel.com/ (imepatikana 30 – 09 – 2013).

Reuster, J. U. (www.qucosa.de/fileadmin/) *Newspaper Serials in Tanzania*: *The Case of Eric James Shigongo*. Kutoka Swahili Forum 15, (2008).

Richard, B. (1997) *Stylistics:The New Critical Idiom.* Routledge, London.

Sawyer, R.J. (mwaka haukutajwa) *Scientific Fiction and Mystery Fiction* katika http://en.wikepidia.org/wiki/science-fiction#mystery-fiction (imepatikana 04 – 10 – 2013).

Senkoro, F.E.M.K (2011) *Fasihi*. KAUTTU Limited, Dar es Salaam.

_____________(1982) *Fasihi.* Press and Publish Center, Dar es Salaam.

Shigongo E.J. (   ) *Siku za Mwisho za Uhai Wangu*. Global Publishers & General Emprises Ltd, Tanzania.

_____________(2012) *Kifo ni Haki Yangu.* Global Publishers & General Emprises Ltd, Tanzania.

_______________ (2005) *Damu na Machozi*. Global Publishers & General Emprises Ltd, Tanzania.

___________ (2003) *Rais Anampenda Mke Wangu*. Global Publishers & General Emprises Ltd,Tanzania.

Simpson, P. (2004) *Stylistics: A Resource Book for Students.* Routledge, London.

TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* Toleo la Pili. TUKI, Dar es Salaam.

Wamitila, (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Kenya Litho Ltd, Nairobi.

Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Focus Publication Ltd, Nairobi.

William, J.C. (1972-73) *Mzimu wa Watu wa Kale* katika Abdilatif, A. na Jaka, R.L. (wahariri), Mulika na 3. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.